Kiswahili



Sura ya Kumbwa Upya

Na A.L. na Joyce Gill

Sura ya Kuumbwa Upya

Na
A.L. na Joyce Gill

Available from
www.gillministries.com

Vitabu vingine vya A.L. na Joyce Gill

Baraka zako za Agano
Ahadi za Mungu kwa Kila hitaji Lako
Kuandaliwa kwa Kutawala
Ondoka! Katika Jina la Yesu
Ushindi juu ya Uwongo

Vitabu katika Mwongozo Huu

Mamlaka ya Mwamini
Njia ya Kuepuka kupata Hasara
Na kuanza Kushinda

Ushindi wa Kanisa
Kupitia Kitabu cha Matendo

Msaada wa Mungu wa Uponyaji
Kupokea na Kuhudumu
Nguvu za Uponyaji za Mungu

Vipawa vya Huduma
Mtume, Nabii, Mwinjilisti,
Mchungaji, Mwalimu

Uinjilisti wa Kimiujiza
Mpango wa Mungu wa Kufikia Ulimwengu

Mbinu za Kuishi
Kutoka Agano la Kale

Sifa na Kuabudu
Kufanyika wenye Kumwabudu Mungu

Maombi
Kuileta Mbingu Duniani

Kuishi Kusiokuwa kwa Kawaida
Kupitia Kipawa cha Roho Mtakatifu

Kumhusu Mwandishi

A.L. na Joyce Gill ni wanenaji, waanzilishi na walimu wa Biblia. Huduma ya usafiri ya mitume imempeleka katika mataifa zaidi ya hamsini ya ulimwenguni, kuwahubiria umati unaozidi laki moja yeye binafsi na pia kwa mamilioni kwa redio na tuninga.

Vitabu vyao vinavyouzwa na stakabadhi vimeuzwa zaidi ya milioni mbili katika nchi ya Marekani. Maandishi yao, ambayo yametafsiriwa katika lugha nyingi, inatumika katika vyuo vya Biblia na pia katika washa mbalimbali duniani.

Kweli zenye nguvu na zibadilishazo katika Neno la Mungu hulipuka katika maisha ya wengine kupitia mahubiri ya ajabu, mafundisho, maandishi na huduma ya kanda za kuona na kusikiza.

Utukufu wa ajabu wa uwepo wa Mungu unaonekana katika washa za sifa na ibada wakati waamini wanatambua jinsi kuwa wakweli na karibu wanapomwabudu Mungu. Wengi wamegundua mbinu mpya na yenye kusisimua ya ushindi na ujasiri kupitia mafundisho yao juu ya mamlaka ya mwamini.

Waandishi hawa wamewafundisha waamini wengi kupiga hatua na kuingia katika huduma za Mungu za asili pamoja na nguvu ya uponyaji ya Mungu katika mikono yao. Wengi wamejifunza kutenda katika karama zote tisa za Roho Mtakatifu katika maisha yao ya kila siku na katika huduma zao.

A.L. pamoja na Joyce wana shada za katika Jiologia. A.L. pia amejifunza na kupata Udaktari katika Filosofia kutoka Chuo Kikuu cha Vision. Huduma zao zinaegemea juu ya Neno la Mungu, huangazia Yesu, imara katika imani na kufundisha katika mamlaka ya Roho Mtakatifu.

Huduma yao huonyesha moyo wa upendo wa Baba. Mahubiri na mafundisho yao huambatana na upako wa ajabu, ishara na maajabu, na miujiza ya uponyaji na wengi wakiangushwa chini ya nguvu za Mungu.

Ishara ya uvuvio ukijumulisha kicheko cha kitakatifu, kilio mbele za Bwana na utukufu wa Mungu na utukufu na nguvu huonekana na wengi wanaohudhuria mikutano yao.

Neno kwa Walimu na Wanafunzi

Yesu alisema, “imekwisha!” kazi ya Yesu ya ukombozi ilikamilika. Kwa nini basi, tunawaona watu wengi wakiishi katika kushindwa? Kwa nini waamini wengi wanaishi katika magonjwa? Kwa nini watu wake Mungu wako katika utumwa, kufungwa na nguvu za mapepo?

Shetani alituhadaa! Kwa muda fulani, tumepoteza ukweli kuhusu mambo mazuri ambayo yamejumlishwa katika ukombozi wetu. Mtume Paulo aliandika:

> **Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya. 2 Wakorintho 5:17**

Ufunuo wa maisha-yabadilishayo katika masomo haya ya Sura ya Kuumbwa Upya itawaweka huru waamini kutokana na hisia za kuhukumika, kuangamia, kutojisikia wa maana, kutoheshimika, na kutotosheleza ili waweze kubadilishwa katika mfano wa Kristo. Itawaachilia waamini waanze kufurahia, kutenda na kuwa na vyote walivyoumbwa kuwa, na kumiliki.

Masomo haya yataweka wazi kweli zenye nguvu za maana ya kuwa kiumbe kipya katika Yesu Kristo. Hizi ni kweli za msingi ambazo ni “lazima” kwa kila mwamini.

Kadri unavyoacha kweli za Neno la Mungu zikolee kuhusu kuumbwa upya, ndipo kweli hizi zitatoka akilini mwako hadi rohoni. Kitabu hiki basi kitatoa mwongozo kwako ili kukitumia unapowaeleza wengine kweli hizi.

Mifano kutoka maisha ya binafsi inaitajika ili kufundisha vizuri. Waandishi wameacha haya ili walimu waweze kutumia mifano na ustadi kutoka maishani mwao, au maisha ya watu ambao wanafunzi watahusiana nao. Ni bora ikumbukwe kuwa ni Roho Mtakatifu ambaye amekuja kutufundisha mambo yote, na kuwa tunaposoma, au kufundisha, ni sharti tutende katika nguvu na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Masomo haya ni bora kwa makundi, Shule za Biblia, Shule za Jumapili, na makundi ya nyumbani. Ni bora kuwa mwalimu na wanafunzi wawe na nakala ya kitabu hiki mkononi wanapojifunza. Vitabu vinapatikana kwa wingi.

Vitabu bora huandikwa ndani, kutiwa mistari, kutafakari juu yake, na pia kuviwaza. Tumeacha nafasi kwa ajili ya nakili zako na maelezo. Mpangilio umewekwa ili kujifunza haraka na kukusaidia kupata msaada tena. Mpangilio maalum humsaidia kila mtu, punde tu wanapojifunza nakala hii, kuyafundisha wengine yaliyomo.

Paulo alimwandikia Timotheo:

> **Nayo mambo yale uliyonisikia nikiyasema mbele ya mashahidi wengi, uwakabidhi watu waaminifu watakaoweza kuwafundisha watu wengine vile vile. 2 Timotheo 2:2b**

Masomo haya yameundwa kama masomo ya Biblia yanayohuzisha katika Mpango wa Kuendeleza Huduma, ambayo ni mbinu ya mpango wa kujifunza. Mawazo haya yanakusudia kuzidisha maishani, huduma na mafunzo ya wanafunzi ya baadaye. Wanafunzi wa awali, kwa kutumia nakala hii, wanaweza kuwafundisha wengine masomo haya kwa urahisi.

Orodha ya Yaliyomo

Somo la Kwanza	Kuumbwa kwa Mfano Wake	7
Somo la Pili	Mfano wetu wa Baba	16
Somo la Tatu	Mfano wetu wa Mwana	26
Somo la Nne	Mfano wa Kuumbwa Upya	37
Somo la Tano	Kuibadilisha Sura Yetu ya binafsi ya Zamani	45
Somo la Sita	Sura yetu katika Kristo	57
Somo la Saba	Haki katika Kuumbwa Upya	68
Somo la Nane	Faida za Kuumbwa Upya	75
Somo la Tisa	Wahusika Katika Asili ya Kiungu	85
Somo la Kumi	Neno la Mungu na Kumbwa Upya	97

*Unless otherwise indicated all Scripture quotations in **New Creation Image** are taken from the **New King James Version**. Copyright 1979, 1980, 1982, Thomas Nelson Inc., Publishers*

Kuumbwa kwa Mfano Wake

Utangulizi

Masomo ya *Sura ya Kuumbwa Upya* yataleta ufunuo wenye nguvu kutambua sisi ni nani katika Kristo – maana ya kuwa kiumbe kipya. Italeta uhuru wa kuwa na hisia ya hukumu, kustahili adhabu, kutokutosheleza, na kuwa chini. Itatuingiza kwa ujasiri katika ufunuo wa maisha yabadilishayo yenye maana ya kuwa katika Yesu Kristo.

Tutagundua kile Mungu alikusudia kwetu katika kazi Yake ya ukombozi. Tutajikuta tumetambulika kama:

- ➢ *Waliozaliwa mara ya pili*
- ➢ *Roho aliyeumbwa tena*
- ➢ *Kuumbwa tena upya*

Mtume Paulo aliandika maneno haya:
2 Wakorintho 5:17 Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

Kama waamini, sisi tu sehemu ya wanadamu wa ujamaa mpya, ujamaa wa "waliozaliwa mara ya pili" tukiwa na uhai wa Mungu ndani yetu. Sisi tu viumbe vipya katika Kristo. Mara nyingi katika masomo haya, waamini watatajwa kama "viumbe wapya"

Masomo haya yataleta ufunuo mpya kuhusu Yesu ni nani nasi ni nani ndani Yake.

Tukiwa na ufunuo huu wenye nguvu sisi kama waamini tutaanza kutembea katika uhuru, mamlaka, ujasiri, nguvu, na ushindi maishani mwetu na katika huduma.

Tutajikuta tukitangaza kwa ujasiri:

Ninajua mimi ni nani katika Yesu Kristo!
Mimi ni yule Yeye anasema!
Ninaweza kufanya kile anasema naweza!
Ninaweza kupata kile anasema naweza!

MWANADAMU – ALIUMBWA KWA MFANO WA MUNGU

Ili kuelewa sisi ni nani kama viumbe wapya, ni lazima tuelewe kile waume na wake walipoumbwa kwanza wawe. Ni sharti tuelewe kuwa alikuwa na kusudi na mpango alipowaumba waume na wake kwa mfano Wake na akawapa mamlaka kamili juu ya ardhi.

Mwanzo 1:26-28 Ndipo Mungu akasema, "Tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale juu ya samaki wa

baharini na ndege wa angani, juu ya dunia yote, na juu ya viumbe wote watambaao juu ya nchi."

Kwa hiyo Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake mwenyewe, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba.

Mungu akawabariki na akawaambia, "Zaeni na mkaongezeke, mkaijaze tena dunia na kuitiisha. Mkatawale samaki wa baharini, ndege wa angani na kila kiumbe hai kiendacho juu ya ardhi."

Sura na Sanamu

Tuliumbwa kwa mfano wa Mungu. Kama viumbe wapya, tunabadilishwa kwa mfano wa Mwana wake. Mfano ni sura kamili ya kitu. Kulingana na kamusi "sanamu" maana yake:

- ➢ *Kuiga au kumwasilisha mtu*
- ➢ *Kitu kionekanacho au sura ya kitu katika kioo*
- ➢ *Mtu kwa mfano wa mwingine; nakili; mwingine; au mfano wake*
- ➢ *Kuwakilisha kikamilifu*

Mungu aliumba Adamu kwa mfano wake kweli. Alimuumba awe kama Mungu mwenyewe – sura ionekanayo katika kioo ya Mungu katika mwili, katika nafsi ya Mungu, na katika roho Wake, ambayo ilikuwa hai na uhai na pumzi ya Mungu.

Mwanadamu aliumbwa ili kuwa mfano na utukufu wa Mungu hapa duniani.

1 Wakorintho 11:7a Mwanaume haimpasi kufunika kichwa chake kwa kuwa yeye ni mfano wa Mungu na utukufu wa Mungu.

Kiumbe aliye na Utatu

Mungu alisema, "hebu tumfanye mwanadamu kwa mfano Wetu." Alisema "Wetu" kwa sababu Mungu, hata ingawa yu mmoja, yu katika nafsi tatu tofauti.

- ➢ *Mungu Baba*
- ➢ *Mungu Mwana*
- ➢ *Mungu Roho Mtakatifu*

Waume kwa wake waliumbwa katika mfano Wake pia kama nafsi tatu.

- ➢ ***Sisi tu roho.***
  Roho wetu ni ufahamu wa Mungu ndani yetu ambayo inahusika na mambo ya kiroho – sehemu ndani yetu ambayo inaweza kuwa na uhusiano na ushirika na Mungu.

➢ ***Sisi ni nafsi.***
Nafsi ni sehemu yetu ambayo inahusika na akili zetu. Hii ni ufahamu, hisia na uwezo wa kuchagua. Hii ni sehemu yetu inayowaza na kufikiria.

➢ ***Tunaishi katika Mwili.***
Mwili wetu ni sehemu yetu ionekanayo – nyumba ambamo roho na nafsi zetu huishi.

Jinsi nafsi ya utatu wa Mungu ni tofauti na ya kipekee, hata hivyo Mungu mmoja, hivyo hivyo roho wetu, na mwili hujumlisha mtu aliyeumbwa na Mungu.

Mtume Paulo alitaja juu ya nafsi tatu zetu alipoandika,

1 Wathesalonike 5:23 Mungu mwenyewe, Mungu wa amani, awatakase ninyi kabisa, roho zenu, nafsi zenu na miili yenu, nanyi mhifadhiwe kikamilifu bila kuwa na lawama katika Bwana wetu Yesu Kristo.

Tunatakiwa kuwa na ufunuo kuhusu roho zetu zilizoumbwa, na kupitia ufunuo huo, Mungu atarejesha roho zetu na mili tena katika ile hali iliyokusudiwa iwe. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa "tumetakasika kabisa" na "kuhifadhiwa bila dosari kwa kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

Na Uhai wa Mungu

Tunatambua kuwa Mungu, kwa mikono Yake, aliumba Adamu kwa mfano Wake na akamvuvia pumzi Yake ya uhai.

Mwanzo 2:7 Bwana Mungu alimwumba mtu kutoka mavumbi ya ardhi akampulizia pumzi ya uhai puani mwake, mtu akawa kiumbe hai.

Uhai wa Mungu ni zaidi ya hali ya kuwa hai. Ni chanzo cha uhai wote.

➢ ***Maisha ya Zoe***

Kuna maneno mawili ya Kigiriki ya muhimu yatumikayo badala ya "uhai" katika Agano Jipya. "Psuche" ina maanisha asili au uhai wa mwanadamu. "Zoe" ina maanisha uhai na hali ya Mungu Mwenyewe. Ni uhai wa Zoe, uhai na hali ya Mungu, ambayo imewekwa ndani ya kila mwamini aliyezaliwa upya.

Hii inafurahisha aje – sisi tu hai na uhai na hali ya Mungu! Adamu na Eva walipotenda dhambi, walipoteza uhai wa Zoe lakini tunapozaliwa upya, roho zetu hufanyika hai na uhai wa Mungu.

Ni uhai wa Mungu tu ndio una nguvu za kuumba. Katika kumuumba mwanadamu, mavumbi yalifanyika hai kwa sababu uhai wa Mungu ulivuviwa ndani yake.

Yohana 1:3,4 Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu.

➢ ***Na Nuru ya Mungu***

Uhai wa Mungu ni nuru; na nuru hii, au utukufu ung'aao, ulifanyika nuru ya Adamu na Eva kabla hawajatenda dhambi.

1 Yohana 1:5 Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka kwake na kuwatangazia ninyi, kwamba Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza lolote.

Inawezekana baada ya kuanguka, Adamu na Eva walivikwa na nuru hii kutoka kwa Mungu – utukufu Wake unaong'aa.

➢ ***Na Ukamilifu wa Mungu***

Tunajua mili ya Adamu na Eva ilikuwa na afya iliyokamilika, mamlaka na nguvu kwani hii ni sehemu ya uhai wa Mungu.

Uhai na pumzi ya Mungu ilikuwa ndani ya damu kila sehemu yao, huku ikiwaacha na afya kamili na uzima wa milele. Adamu na Eva waliumbwa kuishi milele. Hawangekufa ikiwa wangeendelea kuwa na uhai wa Mungu ndani yao.

Roho (akili na, hisia) ya Adamu na Eva ilikuwa ya Mungu katika asili yake. Roho zao zilikuwa na uhai wa Mungu ndani yao, na akili yao, hisia hiari ilikuwa moja na Mungu.

Roho zao zilikuwa kamilifu – moja na Mungu.

Kupewa Utawala

Kitu cha kwanza Mungu alisema kuhusu Adamu na Eva baada ya kuwaumba kilikuwa "basi na wawe na utawala!"

Mwanzo 1:26 Ndipo Mungu akasema, "Tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale juu ya samaki wa baharini na ndege wa angani, juu ya mifugo, juu ya dunia yote, na juu ya viumbe wote watambaao juu ya nchi."

Mungu aliwapa Adamu na Eva mamlaka na utawala juu ya dunia. Mungu alibakisha mamlaka na utawala juu ya ulimwengu wote isipokuwa ardhi. Hapa, alitoa mamlaka haya kwa kiumbe kipya ambaye aliumba kwa mfano Wake.

Na Uwezo wa Kuumba

Kama vile uwezo wake Mungu uliumba dunia, Adamu na Eva walipewa uwezo kufikiria, kuamini na kuumba.

Kwa sabau dhamira yao ilikuwa sawa na Mungu, hapakuwa na hatari ya utumishi mbaya wa hali ya uhai wa uumbaji wa Mungu ndani yao kwa nia iliyo kinyume. Viumbe vyote vya

Mungu duniani vilikuwa kamilifu na bora na walishauriwa kuzidisha kile ambacho tayari kiliiumbwa kamilifu.

Mwanzo 1:28 Mungu akawabariki na akawaambia, "Zaeni na mkaongezeke, mkaijaze tena dunia na kuitiisha. Mkatawale samaki wa baharini, ndege wa angani na kila kiumbe hai kiendacho juu ya ardhi."

Kuwa na Ushirika na Mungu

Mungu alipowaumba Adamu na Eva, walikuwa na ushirika uliokamilika pamoja naye. Aliongea nao ana kwa ana. Wangeweza kumwendea Mungu kwa ujasiri. Hawakuwa na hisia za kuhukumika, lawama, au kuzushwa hadhi. Walikuwa na uhusiano kamili na Mungu.

Mungu alionyesha kuridhika kwake na Adamu alipowaleta wanyama kwake ili awape majina.

Mwanzo 2:19 Basi Bwana Mungu alikuwa amefanyiza kutoka katika ardhi wanyama wote wa porini na ndege wote wa angani. Akawaleta kwa huyu mtu aone atawaitaje, nalo jina lolote alilokiita kila kiumbe hai, likawa ndilo jina lake.

Uhuru wa Kuchagua

Mungu pia aliwapa Adamu na Eva uchaguzi – uhuru wa hiari wa kuchagua. Hakuumbwa kama mashini mfano wa mtu bila uwezo wa kuchagua kuwa na au dhidi ya Mungu. Walikuwa na uamuzi wa kutii au kutomtii Mungu.

Uamuzi huu ulitokana na agizo la Mungu kuhusu mti mmoja katika bustani ya Edeni, mti wa kujua mema na mabaya. Mungu alisema kuwa ikiwa watakula kwa mti huo, kwa hakika wangekufa.

Mwanzo 2:16,17 Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu akamwambia, "Uko huru kula matunda ya mti wowote katika bustani, lakini kamwe usile matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya,kwa maana siku utakapokula matunda yake, hakika utakufa."

KUINGIA KWA DHAMBI – MWANADAMU KUPOTEA

Maandiko yanaonyesha kuwa Adamu na Eva walichagua kutomtii Mungu. Hii ilikuwa dhambi.

Mwanzo 3:6 Mwanamke alipoona ya kuwa tunda la mti huo lilikuwa zuri kwa chakula na la kupendeza macho, tena linatamanika kwa kujipatia hekima, basi akachuma katika matunda yake, akala, pia akampa mumewe, aliyekuwa pamoja naye, naye akala.

Kupitia kwa dhambi, wanadamu wote walipata mateso sana.

Ushirika Kupotea

Mungu katika utakatifu na haki Zake hangeshirikiana na Adamu na Eva. Dhambi yao ilikuwa kizuizi kati yao na Mungu. Hukumu na kuangamia kwao kuliwafanya wajifiche kwa Mungu.

Mwanzo 3:8 Ndipo yule mwanamume na mkewe, waliposikia sauti ya Bwana Mungu alipokuwa akitembea bustanini wakati wa utulivu wa jioni, wakajificha kutoka mbele za Bwana Mungu katikati ya miti ya bustani.

Walipoteza vitu vyao vya dhamana, uhusiano na ushirika wao uliokamilika na Mungu.

Kupotea kwa Uhai wa Mungu

Wakati Adamu na Eva walikula tunda walilokatazwa, walikufa kiroho. Hawakuwa na uhai wa Mungu ndani yao.

Warumi 5:12 Kwa hiyo kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja na kupitia dhambi hii, mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi.

Nafsi zao zilikufa kiroho. Roho zao hazikufanya kazi. Pumzi ya roho wa Mungu, ambayo Mungu aliivuvia ndani ya Adamu, haikuwepo tena.

Kupotea kwa Utukufu wa Mungu

Utukufu wa Mungu ambao ulikuwa umewafunika Adamu na Eva ghafla ulitoweka.

Warumi 3:23 Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu...

Ghafla wakagundua kuwa walikuwa uchi.

Mwanzo 3:7a Ndipo macho yao wote wawili yakafumbuliwa, wakajiona kwamba walikuwa uchi.

Kupotea kwa Ufahamu wa Kiroho

Adamu na Eva walipokufa kiroho, roho zao hazikuwa hai tena kwa Mungu. Fikira zao hazikuwa sawa na Mungu tena. Ufahamu wao ukatoka kwa roho yao, ambayo sasa ilikuwa imekufa, kwa hiyo wakategemea mili yao ya asili.

Wakaanza kutumia hali yao ya asili kupitia hisia tano za mwili. Mambo ya kawaida na kweli yakawa ya kuona, sikia, nusa, onja, au gusa.

Kupoteza Afya Iliyokamilika

Mili ya Adamu na Eva haikuwa na uhai wa Mungu tena. Sasa wangekuwa na magonjwa, maradhi na kuugua. Walipotenda dhambi walianza kuzeeka na kufa kimwili.

Kupoteza Mamlaka

Adamu na Eva walipoteza mamlaka na utawala juu ya dunia. Walimpa Shetani. Sasa waliishi katika ufalme wake, bila tumaini wakiwa chini ya yule alikuja "kuiba, kuua, na kuharibu."

Kufanywa Kutokubadilishwa

Mawazo yasiyobadilishwa, na akili ya mwamini ni mawazo yasiyobadilishwa upya na Neno la Mungu, yaliyo na fikira za kiovu.

Mithali 6:16,17,18 Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana, naam, viko saba vilivyochukizo kwake: Macho ya kiburi, ulimi udanganyao, mikono imwagayo damu isiyo na hatia, moyo ule uwazao mipango miovu, miguu ile iliyo myepesi kukimbilia uovu .....

Wamejaa vitu ambavyo Mungu anachukia.

- ➢ *Kiburi*
- ➢ *Ulimi danganyifu*
- ➢ *Kumwaga damu isiyo na hatia*
- ➢ *Kupanga mbinu na hisia za uovu*
- ➢ *Kukimbilia mambo ya ujanja*

Mtume Paulo pia anaeleza kuhusu mtu asiyemja Mungu, asiye na haki.

Warumi 1:18-22 Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao, kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. Kwa maaana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo wake wa milele na asili yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru. Kwa maana ingawa walimjua Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga.

AHADI YA MKOMBOZI

Ahadi ya Kwanza

Adamu na Eva walisimama bustani ya Edeni:

- ➢ *Bila tumaini na waliotolewa uhusiano na ushirika na Mungu*
- ➢ *Bila mamlaka yao*
- ➢ *Bila ufahamu, hekima na afya*

Lakini, Mungu alivyonena na shetani, alimwahidi mwanadamu kurejeshwa kupitia mkombozi atakayekuwa mbegu ya mwanamke.

Mwanzo 3:15 Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na wake, huo atakuponda kichwa, nawe utamgonga kisigino.

Kupitia kwa Mbegu ya Ibrahimu

Ahadi ya mkombozi ilifanywa upya Mungu aliponena kuwa mataifa yote duniani yatabarikiwa kupitia Abrahimu.

Mwanzo 18:18 Hakika Abrahamu atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, kupitia kwake mataifa yote ya dunia yatabarikiwa.

Mungu alitaja tena ahadi hii kwa Isaka na Yakobo. Aliahidi kuwa mataifa yote duniani yatabarikiwa kupitia mbegu yao. Kulikuwa na Mkombozi anayekuja!

Kupitia kwa Mbegu ya Daudi

Mungu pia alitoa ahadi ya agano na Daudi kuhusu mbegu. Hii pia ilikuwa katika Mkombozi atakayokuja, Yesu Kristo.

Zaburi 89:34-36a Mimi sitavunja agano langu wala sitabadili lile ambalo midomo yangu imetamka. Mara moja na kwa milele, nimeapa kwa utakatifu wangu, nami sitamdanganya Daudi, kwamba uzao wake utaendelea milele.

Kutabiriwa na Isaya

Isaya alitabiri kuja kwa Mkombozi.

Isaya 9:6,7a Kwa maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume, nao utawala utakuwa mabegani mwake. Naye ataitwa: Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye Nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani. Kuongezeka kwa utawala wake na amani hakutakuwa na mwisho. Atatawala katika kiti cha enzi cha Daudi na juu ya ufalme wake akiuthibitisha na kuutegemeza kwa haki na kwa adili, tangu wakati huo na hata milele.

Kwa Niaba Yetu

Dhambi na mauti ilikuwa matokeo ya kuasi kwa Adamu na Eva. Ni kupitia kwa kuja kwa Adamu wa mwisho tu kwa niaba yetu, ndipo tunaweza kuwekwa huru kwa gharama hizi. Isaya 53 inatoa picha ya kuja kwa Mkombozi.

Isaya 53:4,5 Hakika alichukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa. Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.

Kupitia kazi ya ukombozi ya Masiha aliyekuja, vyote ambavyo Adamu na Eva walipoteza walipoanguka

vingerejeshwa. Kwa mara tena wanadamu wangefanyika viumbe waliotarajiwa kuwa. Kuumbwa upya kutarejeshwa!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kwa nini Adamu na Eva walikuwa na tabia ya Mungu walipoumbwa?

2. Je, Adamu na Eva walikuwea na nini ndani yao iliyowafanya kuwa tofauti na wanyama wengine walioumbwa na Mungu?

3. Orodhesha baadhi ya vitu ambavyo mwanadamu alipoteza alipoanguka ambavyo vitarejeshwa katika kuumbwa upya.

Somo la Pili

Mfano wetu wa Baba

Utangulizi

Ili kuelewa mfano wetu wa kuumbwa upya, ni sharti tuwe na ufunuo kuhusu Mungu ni nani. Kwa sababu tumeumbwa kwa mfano Wake, hatuwezi kuelewa tuliumbwa ili kuwa vipi mpaka tuwe na picha ya Baba.

Mtume Paulo aliandika, jinsi tunao utukufu wa Bwana, tutabadilishwa katika mfano huo huo. Ufunuo huleta mabadiliko.

2 Wakorintho 3:18 Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.

Katika somo hili, tutaona utukufu wa Baba. Tutapinga picha na sura ambazo huenda tumejiwekea kuhusu Baba. Tutamruhusu Roho Mtakatifu, kwa ufunuo wa Neno la Mungu, kudhihirisha picha ya kweli ya Baba wetu wa mbinguni.

Njia Tatu za Utendaji wa Roho

➢ *Yesu na Watu*

Katika njia ya Yesu na watu, wengi walipokea ufunuo mpya na walipata uhusiano wa karibu na ushirika na Yesu binafsi.

➢ *Msisimuo wa Kufanywa Upya*

Katika Msisimuo wa Kufanywa upya, wengi walipata uhusiano wa karibu na pia ushirika na Roho Mtakatifu binafsi.

Jinsi watu walivyoelekezwa na Roho Mtakatifu, waliweka kando mambo ya tenzi na kupata furaha ya Kibiblia ya kuingia katika sifa kwa Yesu.

Daudi anatueleza haya alipoandika,
Zaburi 100:4 Ingieni malangoni mwake kwa shukrani na katika nyua zake kwa kusifu, mshukuruni yeye na kulisifu jina lake.

➢ *Kumfahamu Baba*

Katika mbinu hii mpya ya utendaji wa Mungu kabla ya kurudi tena kwa Yesu, tutaingia katika uhusiano na ushirika wa karibu na Baba. Tutafanyika watu wake wanaomwabudu.

Tukiwa tukiimba, tukiinua mikono yetu, kupiga makofi, kuruka na kucheza mbele za Bwana. Lakini, sasa kuna mapendekezo ya kuingia katika uwepo wa Baba ndani ya Utakatifu wa watakatifu – kuingia ndani ya pazia.

Sio tu kuwa tumetosheka kubaki nje kwenye ukumbi, bali tunatazama kwenye uso wa Baba, kuhisi mikono Yake ya upendo kwetu, na kuwa karibu Naye katika kuabudu.

Yohana 4:23 Lakini saa yaja, tene ipo, ambapo wale waabuduo halisi,watamwabudu Baba katika roho na kweli. Watu wanaoabudu namna hii, ndio Baba anawatafuta.

Baba anawatafuta waabudio wa kweli watakaokuwa na muda kuabudu katika roho na kweli, watakaoingia mahali pa Utakatifu wa watakatifu.

BABA WETU HAPA DUNIANI

Sura yetu ya Baba wa mbinguni mara nyingi huonyeshwa na vitendo vya baba wa hapa duniani. Uhusiano wetu na baba wetu wa hapa duniani hugusia uhusiano wetu na Baba wa mbinguni.

Shughuli nyingi

Baba wengi walikuwa na shughuli nyingi kupata muda na wana wao wanapokua. Hii huenda ni kwa sababu nyingi, lakini hii imewaacha wengi na hisia kuwa "Mungu ana shughuli nyingi kando nami."

Mwenye Kutoa Adhabu kali

Baba wengine wamewapa watoto wao adhabu kali kupitia nidhamu bila upendo. Watoto hawa mara nyingi wanajihisi kuwa Baba yao wa mbinguni huwaangalia na adhabu kali, ni kama anayo fimbo mkononi Mwake akisubiri mtu avuke ya msitari.

Asiye na upendo

Wengi wamekua katika nyumba ambapo upendo ni haba mno na pia kusikilizwa na baba yao. Hata kama walijaribu sana, inaonekana hawakupata pongezi na shukrani kutoka kwa baba yao.

Kwa haya, sura ya Baba yao wa mbinguni ni moja ya kutoyakubali na kupuuza maitaji yao. Wanajihisi kuwa Mungu hawajali kuhusu mafanikio yao na kuwa Yeye kwa kweli hawapendi.

Umaskini

Wengine walitoka katika jamii ambapo baba zao aidha hawangeweza, au hawakuta, kukutana na kutosheleza maitaji ya kijamii katika maisha ya kawaida. Walikua katika maisha ya umaskini.

Watu hawa mara nyingi wanakuwa na "picha ya umaskini" ya Mungu. Wanakuwa na tatizo kuona kwamba Mungu atakutana na maitaji yao maishani.

Kunyanyazwa

Watoto wengi wameteswa na baba zao wa duniani. Wengine wameteswa kihisia, wengine kimwili, na wengine pia wameteswa kijinsia.

Haya yamewazuia kummwamini kabisa Baba wa mbinguni au kupokea upendo Wake mkuu. Wajihisi kuhukumika mbele za Mungu au hukasirika naye, na wanashindwa kumtegemea maishani kabisa.

BABA WETU WA MBINGUNI

Upendo

Mbali na kuteswa, kukataliwa, au kudhulumiwa tulizopata kutoka kwa wazazi wetu wa duniani, ni sharti tuwasamehe, na kupokea uponyaji kutoka kwa Mungu ili tutambue, kupokea, na kufurahia upendo wa ajabu wa Baba wetu wa mbinguni.

1 John 3:1a Behold what manner of love the Father has bestowed on us, that we should be called children of God!

Mtume Paulo aliandika kuwa hakuna kitakachotutenga na upendo wa Baba.

Warumi 8:38,39 Lakini katika mambo haya yote tunashinda, naam na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua kwa hakika ya kuwa wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo wala yatakayokuja, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine chochote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Baba anayo furaha kwa ajili Yetu

Badala ya baba asiyejali na mkali, tunaye Baba wa mbinguni anayetupenda sana mpaka ana furaha kwetu na pia akiimba.

Nabii Zefania anaeleza kuhusu Mungu kwa njia hii:
Sefania 3:17 Bwana Mungu wako yu pamoja nawe, yeye ni mwenye nguvu kuokoa. Atakufurahia kwa furaha kubwa, atakutuliza kwa pendo lake, atakufurahia kwa kuimba.

Neno la Kiebrania la Zefania lililotumika kufurahi lina maana ya msingi “kuimba” au ‘kuruka kwa furaha” Mungu ana furaha tele kwetu kama wanawe, Yeye huruka juu na chini na kucheza katika njia ya kuonyesha furaha kuu.

Je, ni sura tofauti iliyoje ya Baba! Mungu hana shughuli nyingi hata atusahau. Yeye hakasiriki, mwenye nidhamu bila upendo. Yeye hataki kutuadhibu. Yeye anayo furaha juu yetu. Anaruka kwa furaha kwa ajili yetu!

Mioyo Hugeuka kwa Baba

Leo, kama vile katika Agano la Kale, Mungu anawatumia manabii kugeuza mioyo ya watoto kwa baba zao.

Malaki 4:5,6a "Tazama, nitawapelekea nabii Elia kabla ya kuja siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana. Ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.

Mungu anageuza mioyo ya watoto, waume kwa wake, kwa baba zao wa duniani na mioyo ya Watoto wa Mungu kwa Baba wao wa mbunguni.

VIZUIZI VITATU KATIKA USHIRIKA

Dhambi

Adamu na Eva walikuwa na ushirika bora na Mungu hadi wakati walipotenda dhambi. Mungu mtakatifu na mwenye haki hangekuwa na ushirika pamoja na dhambi.

Wakati wa wokovu, dhambi zetu husamehewa na kuondolewa. Uhusiano wetu, na ushirika wetu na Mungu huanza. Tunapotenda dhambi, hata kama uhusiano wetu na Mungu huendelea, ushirika wetu Naye huvunjika. Ushirika huu unaweza tu kurejeshwa tunapokiri dhambi zetu Kwake.

1 Yohana 1:9 Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote.

Kukataliwa

Wengi hukataliwa na baba zao wa duniani. Labda walikuwa matokeo ya uzazi au mimba isiyopangiwa. Labda baba alitaka sana mtoto wa jinsia ya kinyume, au kama mtoto, hawakufikia kiwango cha matakwa ya baba yao.

Mtu awe aliteswa katika kukataliwa au hisia za kukataliwa, yeye huwa na mawazo tele na kusononeka maishani mwake.

Watu hawa hujihisi kuwa hata Baba yao wa mbinguni pia huwakataa. Wanakuwa na ugumu kukubali upendo Wake na kukubalika. Kuna kitu ambacho huwazuia wasifikie uhusiano wa binafsi na wa karibu na Baba wao wa mbinguni na kufanyika waabudio Wake wa kweli.

Mtu aliye na hisia za kukataliwa maishani mwake ni lazima awasamehe waliomkataa na kisha kupokea uponyaji wa Mungu rohoni mwake.

Hofu

Hofu ya kufika mbele ya Baba imewazuia wengi kutokufanyika waabudio wa kweli Kwake. Lakini, badala ya

hofu, Mungu ameweka kwetu Roho wa kufanyika Wake ambapo tunaweza kuja kwake na kumwita Abba.

Warumi 8:15 Kwa maana hamkupokea roho ya utumwa iwaleteayo tena hofu, bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambaye kwa yeye twalia "Abba," yaani, Baba."

"Abba" ni kueleza kupendwa na, uhusiano wa karibu wa binafsi na Baba. Inaweza kutafsiri "Baba"

2 Wakorintho 6:18 "Mimi nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wanangu na binti zangu, asema Bwana mwenyezi."

Ni kwa upendo mkuu wa Baba ndipo alituchukuwa kuwa watoto Wake.

1 Yohana 3:1a Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu!

Kuelewa juu ya upendo mkuu wake Mungu huondoa hofu yetu.

Daudi, Mfano Wetu

Daudi alikuwa mtu aliyekuwa akitafuta roho ya Mungu. Alitafuta kuwa wa karibu sana na Baba yake wa mbinguni katika kuabudu.

Zaburi 27:4 Jambo moja ninamwomba Bwana hili ndilo ninalitafuta: niweze kukaa nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana na kumtafuta hekaluni mwake.

Daudi alitafuta kukaa katika uwepo wa Mungu kila siku maishani mwake. Alitafuta kuingia katika uwepo wa Baba, na kutazama urembo wake.

➢ *Alitoa Sifa na Kuabudu*

Zaburi 27:6b Nitatoa dhabihu kwa kelele za shangwe, nitamwimbia Bwana na kumsifu.

Daudi alijuwa jinsi ya kuimba sifa na kucheza mbele za Bwana akiwa "bustanini". Lakini, alitaka zaidi. Alitaka kuingia katika uwepo wa Baba na kutafuta uso Wake.

Zaburi 27:8 Moyo wangu unasema kuhusu wewe, "Utafute uso wake!" Uso wako, Bwana "Nitautafuta."

➢ *Alikuwa na Hofu ya Kukataliwa na Mungu*

Hata kama Daudi alitaka kumwabudu Baba, alipoingia katika uwepo wake Baba katika kuabudu, ghafla alirudi nyuma kwa hofu ya kukataliwa.

Zaburi 27:9 Usinifiche uso wako, usimkatae mtumishi wako kwa hasira, wewe umekuwa msaada wangu. Usinikatae wala usiniache, Ee Mungu Mwokozi wangu.

➢ *Kukataliwa na Baba wa Duniani*

Daudi aliteswa kwa kukataliwa na baba yake wa duniani akiwa kijana, na sasa hiyo hofu ya kukataliwa ilimuzuia kuingia mbele ya Baba wa mbinguni bila hofu.

Daudi alipokuwa kijana, nabii Samueli alikuja Bethlehemu kumpaka mafuta mfalme atakayefuata. Babake Daudi aliwakusanya watoto wake wote pamoja kwa matumaini kuwa mmoja wao atatiwa mafuta kama mfalme. Daudi hakualikwa mbele za Samueli siku hiyo.

Huu ungekuwa wakati ambapo Daudi angejisikia kukataliwa na babake wa dubiani. Hii iliweka hofu ndani ya Daudi kuwa atakataliwa na Babake wa mbinguni.

Ingawa alitaka sana kuja mbele za Baba yake wa mbinguni, kuutafuta uso wake, na kuuona urembo wake, wakati alianza kuingia katika kuabudu, hofu ya kukataliwa iliishika roho yake.

➢ *Kupata Uhuru Kutokana na Kukataliwa*

Daudi aligundua kuwa alikataliwa na baba yake na mama yake. Aliielewa shida, na kisha akafanya uamuzi dhidi ya hisia za kukataliwa.

Zaburi 27:10 Hata kama baba yangu na mama wataniacha, Bwana atanipokea.

Wakati huo, Daudi alitembea kwa ujasiri katika uwepo wa Mungu. Aliutazama uso Wake na kuhisi upendo na kukubalika na Baba rohoni mwake

YESU ANAMDHIHIRISHA BABA YAKE

Mojawapo ya kusudi la Yesu hapa duniani ilikuwa kumdhihirisha Baba Yake. Wakati huduma ya Yesu hapa duniani ilikaribia kukamilika, punde tu kabla ya Yeye kushikwa, kujaribiwa na kusulubiwa, Yesu alimtaja Baba Yake mara hamsini katika Injili kama alivyoandika Yohana, sura kumi na nne hadi kumi na saba.

Alisema kwa kurudia rudia kwa wanafunzi Wake, "Nataka mumfahamu Baba yangu!"

"Nifahamu Mimi – Mfahamu Baba Yangu"

Tukimfahamu Yesu, tutamfahamu Baba. Kadri tunapotumia muda kumjua Yesu kupitia Injili, ndipo tutamjua Baba zaidi.

Yohana 14:7 Kama mngenijua Mimi, mngemjua na Baba pia. Tangu sasa mnamjua Baba yangu tena mmemwona.

Katika Injili, tunaona upendo na huruma ya Yesu alipoendelea kuwafikia na kuwagusa watu, kukutana na

mahitaji yao, kuponya miili yao na kurejesha mioyo yao. Hii ilikuwa kielelezo cha upendo wa Baba.

Yohana 14:9b Mtu yeyote aliyeniona Mimi, amemwona Baba.

Upendo Wa Baba

Yesu alipowachukua watoto na kuwashika mikononi, alionyesha upendo wa Baba kwa watoto Wake.

Mathayo 19:14 Yesu akasema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa Mbinguni ni wa wale waliokama hawa."

Je, ni picha ya ajabu iliyoje ya kuonyesha jinsi Baba angependa kutuvuta ili tuwe karibu Naye na kuweka mikono yake kwetu.

Yesu alipowahudumia wale waliokuwa karibu Naye, alidhihirisha upendo wa Baba Yake.

Yohana 14:23 Yesu akamjibu, "Mtu yeyote akinipenda atalishika Neno Langu na Baba yangu atampenda, Nasi tutakuja kwake na kufanya makao Yetu kwake."

Je, ni ufunuo wa ajabu ulioje. Sema kwa sauti.

Baba yangu wa mbinguni ananipenda!
Anataka aje na Yesu na aishi pamoja nami!
Baba yangu anataka kujenga nyumba Yake pamoja nami!

➢ ***Kutoa Kwa Baba***

Yesu alisema kuwa tunaweza kumwuliza Baba yetu msaada.

Yohana 16:23b Amin, amin, nawaambia, kama mkimwomba Baba jambo lolote kwa jina langu, Yeye atawapa.

Hatuulizi katika jina la Yesu kwa sababu Baba anampenda Yesu na atamfanyia mambo. Tunauliza katika jina la Yesu kwa sababu kupitia kwa dhabihu ya Yesu ndipo uhusiano wetu na Baba unarejeshwa.

➢ ***Nyumba ya Baba***

Yesu alituambia kuhusu nyumba ya Baba Yake. Alisema kuwa ataenda na kutuandalia mahali katika nyumba ya Baba Yake.

Yohana 14:2 Nyumbani kwa Baba yangu kuna makao, mengi. Kama sivyo, ningeliwaambia. Nakwenda kuwaandalia makao.

Hapo baadaye, tunatakiwa kuishi katika Nyumba ya Baba. Hapa ndipo jamii huishi. Tunatakiwa kuwa na uhusiano wa karibu na Baba wa mbinguni.

"Nitawambia kwa Uwazi"

Yesu anataka kutuambia wazi kuhusu Baba Yake.

Yohana 16:25 Nimewaambia mambo haya kwa mafumbo. Saa yaja ambapo sitazungumza nanyi tena kwa mafumbo bali nitawaeleza waziwazi kuhusu Baba.

Hapa ni baadhi tu ya mara zile hamsini Yesu alitaja kuhusu Baba Yake katika sura hizi nne. Yesu alionyesha hamu kuu kuwa kila mmoja wetu atafika katika uhusiano wa karibu na Baba Yake.

MWANA MPOTEVU

Mara nyingi mfano wa Mwana Mpotevu hutumika katika jumbe za kiinjilisti kama mwito wa toba au kurejeshwa katika ushirika. Tumeelewa kuwa tunaweza kuja kwa Baba hata kama tumezushwa na kuzama katika hali yoyote.

Katika kuasi, mwana mpotevu alitoka nyumbani na kuharibu urithi wake wote katika maisha yasiyokubalika. Kisha ukame mkuu ukaja, akawa akiwalisha nguruwe na kula makanda waliyokula.

Mwana

Wengi wetu tunakubaliana na mwana. Tumejihisi, au tunaweza kuhisi, kutengwa na Baba wa mbinguni, hofu ya kukataliwa, au hisia za kutokuwa wa maana, kutokuwa na msamaha na kuhukumika.

Luka 15:17-20a "Lakini alipozingatia moyoni mwake, akasema, "Ni watumishi wangapi walioajiriwa na baba yangu ambao wana chakula cha kutosha na kusaza, bali mimi hapa nakufa kwa njaa! Nitaondoka na kurudi kwa baba yangu na kumwambia, "Baba, nimetenda dhambi mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili tena kuitwa mwanao, nifanye kama mmoja wa watumishi wako."

Alisema, "Mimi sistahili tena." Kijana huyu, kama vile waamini wengi leo, alijisikia hastahili. Aliona sura yake haifai. Na hata kama alikuwa na sura hiyo, alirudi nyumbani.

Baba

Mfano huu ni ufunuo wa ajabu kuhusu Baba yetu wa mbinguni.

Anatupenda

Mungu hapendelei.
Yeye si mkali
Yeye hangojei watoto wake waume kwa wake wamlilie kwa msamaha.

Je, Yesu alisema nini?
Luka 15:20b "Lakini alipokuwa bado yuko mbali, baba yake akamwona, moyo wake ukajawa na huruma. Akamkimbilia mwanawe, akamkumbatia na kumbusu.

Badala ya Baba yetu kugeuza uso wake mbali nasi kwa kukataliwa, Yeye anatusubiri tuje kwake. Anataka kuweka mikono yake kwetu na kutubusu kama ishara ya upendo Wake mkuu na wa ajabu.

Ms. 21 "Yule mtoto akamwambia baba yake, "Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili kuitwa mwanao tena."

Baba hata hakujadili kile mwanawe alikuwa amefanya, au kile alikuwa akisema.

Ms. 22-24 "Lakini baba yake akawaambia watumishi, "Leteni upesi joho lililo bora sana, mkamvike pete kidoleni mwake na viatu miguuni mwake. Leteni ndama aliyenona, mkamchinje ili tuwe na karamu, tule na kufurahi. Kwa maana huyu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai tena, alikuwa amepotea na sasa amepatikana!" Nao wakaanza kufanya tafrija.

Sura ya Mwana

Baba alijua kuwa ilimbidi aibadili sura ya mwanawe. Alimvalisha vazi nzuri. Aliiweka pete kwenye kidole na vyatu vipya miguuni mwake.

Punde tunapompokea Yesu kama mwokozi, Baba yetu wa mbinguni anatuona kama wanawe waume kwa wake. Tumevalishwa mavazi Yake ya haki. Tunayo pete ya mamlaka kwenye vodole vyetu.

Katika upendo, anasema, "jinsi napenda wafahamu wao ni nani ndani ya Yesu Kristo. Wao ni wamoja na Mwana wangu! Wao ni haki wa Mungu katika Yesu Kristo."

Mtume Paulo aliandika haya.
2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Mfano Wetu wa Kuumbwa Upya

Tunapomruhusu Yesu kudhihirisha Baba yake kwetu, sura na mifano mibaya tuliyo nayo kuhusu Baba wetu wa mbinguni itabadilika.

Tutakuwa, kama Daudi, tuuone urembo wa Bwana. Tutautafuta uso Wake. Tutamwabudu Yeye. Tutahisi kukubalika kwake. Tunapouona utukufu Wake Bwana, sura yetu ya Baba itabadilika, na pia sura yetu ya binafsi ya awali itabadilishwa na kuwa mfano wa kuumbwa upya.

Wengi wamekuwa wakitafuta mkono wa Mungu badala ya uso Wake. Wametumia muda wao kuja kwa Bwana wayatosheleze mahitaji yao.

Kubadilishwa

➢ *Kwa Kumtafuta Baba*

Badala yake ni sharti tuje mbele za Mungu na kutumia muda kuutafuta uso Wake na kuuona utukufu Wake. Kisha, tutabadilishwa katika mfano wake.

2 Wakorintho 3:18 Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tutabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.

Mwandishi wa Zaburi Daudi alieleza kama vile mtume Paulo.

Zaburi 17:15 Na mimi katika haki nitauona uso wako, niamkapo, nitaridhika kwa kuona sura yako.

➢ *Kwa Kumwabudu Baba*

Hatubadilishwi kwa mfano wake tunapojitazama na kutarajia mabadiliko yafanyike maishani mwetu. Tunabadilishwa kwa mfano wake tunapotumia muda na Baba yetu katika upendo wa karibu na kumwabudu Yeye jinsi alivyo.

Tunapoendelea kutumia muda kuutafuta uso wa Mungu, basi "tunaamka" tukiwa na nyuso zetu ziking'aa na utukufu wa Mungu. Sisi, kama Musa alishuka baada ya kuutumia muda wake na Mungu mlimani Sinai, tutang'aa katika utukufu wa Mungu.

Luka aliandika,
Luka 11:36 Basi ikiwa mwili wako wote umejaa nuru, bila sehemu yake yoyote kuwa gizani, basi utakuwa na nuru kama vile taa ikuangazavyo kwa nuru yake."

Basi, tutakuwa kile ambacho wanadamu waliumbwa wawe Mungu aliposema, "Hebu na tuumbe mwanadamu kwa mfano wetu."

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, ni kwa njia gani mfano wetu wa Baba wetu wa mbinguni hubadilishwa na maisha yetu ya utotoni?

2. Je, mfano wetu wa Baba wa mbinguni unaweza kubadilishwa ili kukubaliana na mfano wa kweli wa Baba jinsi inavyodhihirishwa katika Neno la Mungu?

3. Kulingana na 2 Corinthians 3:18, je, tunaweza kubadilishwa vipi kwa mfano wa Bwana?

Sura Yetu ya Mwana

MWANA WA MUNGU

Ili tuwe na ufunuo kamili kuhusu hali yetu kama viumbe vipya, ni lazima tuwe na ufunuo kuhusu Mwana wa Mungu.

Mtume Paulo aliandika kuwa Mungu alikusudia, akaandaa au kututenga ili tubadilishwe katika sura ya Mwana wa Mungu.

Warumi 8:29a Maana wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe.

Tunapobadilishwa kwa sura ya Mwanawe, tutaanza kutimiza uwezo wetu na kuanza kuishi kama viumbe vipya. Tunafahamu kuwa Yesu ni mmoja na Baba na Roho Mtakatifu, na kuwa kila mwenendo walio nao – tunao pia.

Ni Mungu

Mtume Yohana anatuambia mambo manne muhimu kuhusu Mwana.

- ➢ *Yeye mara yote alikuwepo.*
- ➢ *Yeye ni Neno la Mungu aishiye.*
- ➢ *Yeye ni muumba wa vitu vyote.*
- ➢ *Yeye alifanyika Mwili na akakaa nasi.*

Yohana 1:1-3,14 Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa.

Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu.

Aliwaumba Adamu na Eva

Yohana aliweka wazi kuwa vitu vyote vilumbwa na Mwana wa Mungu. Adamu na Eva waliumbwa Naye.

Mwanzo 1:27 Kwa hiyo Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake mwenyewe, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke aliwaumba.

Mwanadamu aliyekombolewa ni sharti aumbwe tena, ili kubadilishwa katika sura ya Mmoja aliyewaumba Adamu na Eva kwa mfano Wake.

Aliziacha haki zake kama Mungu

Yesu alizaliwa kwa bikra hapa duniani kama mwanadamu. Alikuwa angali Mungu kweli, lakini aliziacha haki zake kama Mungu na akaja hapa duniani kama mwanadamu. Alikuwa mwanadamu kweli, lakini hali Yake ya kiungu haikupotea.

Wafilipi 2:5-8 Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba!

Ni muhimu sana kuelewa kuwa Yesu aliziweka kando haki zake kama Mungu. Alijiweka kama mwanadamu. Yote aliyofanya Yesu alipoishi na kuhudumu hapa duniani, alifanya kama mwanadamu, wala sio kama Mungu.

Ufahamu wa Kupotosha

Tukimtazama Yesu alipotembea hapa duniani akitenda katika nguvu Zake kama Mungu, hatuwezi kuelewa jinsi tunaweza kubadilishwa katika sura Yake.

"Ndiyo!" tunaweza kusema, "Yesu angeweza kuwaponya wagonjwa, kukemea mapepo, na kutuliza dhoruba. Hata hivyo, alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa mwenye nguvu zote! Je, haya yanatuhusu vipi?"

Je, Yesu angekuwa mfano au mwongozo katika maisha yetu ikiwa alitenda kama Mungu? Ikiwa Yesu aliishi na kutenda katika ulimwengu usio wa kawaida, basi tutasema sisi ni wanadamu tu.

"Ni tumaini la kipekee tulilo nalo," tutawaza, "ni kuomba ili kupata msaada usio wa kawaida kutukomboa kutokana na mapigo, magonjwa na matatizo ya kifedha."

Tukichukua sura ya Yesu akitenda hapa duniani – akiziweka kando haki zake kama Mungu – akija kama mwanadamu katika mamlaka Mungu alimpa – basi tunaweza kujiona tukiyatenda mambo yale Yesu alitenda.

Mamlaka Duniani

Yesu alisema,

Yohana 5:24,25 "Amin, amin, ninawaambia, ye yote anayesikia maneno yangu na kumwamini Yeye aliyenituma, anao uzima wa milele, naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka mautini, na kuingia uzimani. Amin, amin, nawaambia, saa yaja, nayo saa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, nao watakaoisikia watakuwa hai.

Wale wanaoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, wataishi.

Kisha Yesu akaendelea akisema,
Yohana 5:26, 27 Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na na uzima ndani Yake. Naye amempa Mwanawe mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Adamu.

Ni wazi kutokana na kifungu hiki kuwa mamlaka Yesu aliishi na kuhudumu nayo alipokuwa hapa duniani, haikuwa mamlaka Yake kama Mwana wa Mungu. Yalikuwa mamlaka Yake kama Mwana wa Adamu.

Yesu ni kielelezo kwetu kama mfano. Kama viumbe vipya katika Yesu, mamlaka tuliyopewa na Mungu hapa duniani yamerejeshwa. Ni sharti tutenda katika mamlaka hayo kama Yesu, Mwana wa Adamu, alivyofanya. Tunapopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunaweza kutenda katika mamlaka hayo Yesu alitenda baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake.

Sasa, tunaposoma Injili, tunaweza kuona kuwa Yesu kwa kweli alikuwa mfano wetu na mwelekezi. Tunaweza kutenda katika mamlaka na nguvu zile Yesu alifanya akiwa hapa duniani. Wanadamu, kama viumbe wapya, wanaweza kuishi katika mamlaka hayo waliyoumbwa waishi ndani yake Mungu aliposema, “Hebu na wawe na utawala!”

Was Last Adam

Yesu alikuja kama Adamu wa mwisho.

1 Wakorintho 15:45 Kwa hiyo imeandikwa, “Mtu wa kwanza Adamu alifanyika kiumbe hai,” Adamu wa mwisho, Yeye ni roho iletayo uzima.

Kila kitu Adamu aliumbwa kufanya – Yesu alifanya. Mungu alisema, “Hebu na wawe na utawala” – Yesu alichukua utawala juu ya mapepo, juu ya viumbe vyenye uhai, juu vitu. Alitembea katika mamlaka.

Mathayo 7:28,29 Yesu alipomaliza kusema maneno haya, makutano ya watu wakashangazwa sana na mafundisho yake, kwa sababu alifundisha kama yeye aliye na mamlaka, wala si kama walimu wao wa sheria.

➢ *Alishiriki katika Ubinadamu wetu*

Yesu alishiriki katika ubinadamu wetu kama nyama na damu.

Waebrania 2:14a Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao.

➢ *Alipata Majaribu*

Alipata majaribu kama vile sisi tunapata.

Waebrania 4:15 Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuliana na sisi katika udhaifu wetu, kwani Yeye mwenyewe alijaribiwa, kwa kila namna, kama vile sisi tujaribiwavyo, lakini Yeye hakutenda dhambi.

Hata kama alipata majaribu kama mwanadamu yeyote, Yesu aliishi bila dhambi kama vile Adamu na Eva waliumbwa wawe.

➢ *Kazi zake – Kazi zetu*

Yesu alikuja kuwa na kutenda yote aliyowaumba wanadamu kuwa na kutenda. Aliziweka kando haki zake kama Mungu na akaishi na kuhudumu kama mwanadamu hapa duniani.

Yohana 14:12 Amin, amin, nawaambia, ye yote aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya, naam na kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa sababu mimi ninakwenda kwa Baba.

Yesu angesema, "yeye aaminiye atatenda kazi hii na hata kazi kubwa zaidi" ikiwa hii haikuwezekana.

➢ *Nguvu Zake – Nguvu zetu*

Kazi zote na huduma ya Yesu ilifanyika katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Luka 3:22a Roho mtakatifu akashuka juu Yake kwa umbo kama la hua.

Hakuna miujiza ya Yesu iliyoandikwa hadi baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake alipobatizwa. Huu ulikuwa mwanzo wa huduma ya Yesu duniani.

Yesu alisema, alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu ili kuhubiri Injili, kuwaponya wagonjwa, na kuwakemea mashetani.

Luka 4:18,19 "Roho wa Bwana yu juu Yangu, kwa sababu aminitia mafuta kuwaletea maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka huru wanaoonewa na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubarika."

Wakati Yesu alijiandaa kuondoka hapa duniani, Alizungumza juu ya kuja kwa roho Mtakatifu, na alisema kuwa Roho Mtakatifu atawapa wafuasi Wake nguvu.

Matendo 1:8a Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.

Tunayo nguvu hiyo iliyokuwa katika maisha ya Yesu alipofanya huduma duniani.

Luka aliyatumia maneno – "nguvu" na "Roho Mtakatifu" – alipoandika juu ya maisha ya Yesu.

Matendo 10:38 Jinsi Mungu alivyomtia Yesu wa Nazareti mafuta katika Roho Mtakatifu na jinsi alivyokwenda huku na huko akitenda mema na kuponya wote waliokuwa wameonewa na nguvu za shetani, kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye.

Yesu Alikuja

➢ *Kumdhihirisha Baba*

Yesu, Mwana wa Mungu, ni sura kamili ya Baba.

Yesu alisema,
Yohana 10:30 Mimi na Baba Yangu tu Umoja.

Yeye pia alisema,
Yohana 14:6,7 Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu. Kama mngenijua Mimi, mngemjua na Baba pia. Tangu sasa mnamjua Baba Yangu tena mmemwona."

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania alisema kuwa Yesu alikuwa sura ya Mungu kamili.

Waebrania 1:3a Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake .....

Paulo aliandika kuwa Kristo alikuwa sura ya Mungu asiyeonekana.

Wakolosai 1:15 Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.

Yesu alikuwa mzaliwa wa kwanza kwa sura a Jesus was the first-born in the image of His Father to be over all creation. We are born again to be conformed to His image as new creations.

➢ *Kutenda Mapenzi ya Baba*

Yesu alipokuja hapa duniani, aliacha mapenzi yake kwa Baba. Alipotembea hapa duniani, alifanya mapenzi ya Baba Yake.

Yohana 6:38 Kwa kuwa nimeshuka kutoka mbinguni si ili kufanya mapenzi yangu, bali mapenzi yake Yeye aliyenituma.

➢ *Kuharibu Kazi za Shetani*

Popote Yesu alihudumu, aliharibu kazi za shetani. Yohana anatuambia kuwa hii ilikuwa mojawapo ya kazi muhimu Alikuja hapa duniani.

1 Yohana 3:8b Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi.

Adhabu ya Dhambi

Dhambi ya Adamu na Eva iliwatenga na Mungu mtakatifu ambaye hangehuzishwa na ndambi. Mungu hangeamua, katika upendo, kuipuuza dhambi, kwa sababu Mungu pia yu mkamilifu katika haki. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu na mwenye haki, hangevumilia dhambi.

Mungu alisema,
Mwanzo 2:17b ... Kwa maana siku utakapokula matunda yake, hakika utakufa.

Adamu na Eva walipoteza uhusiano wao na Mungu. Roho wa Mungu ndani yao hangekaa walipotenda dhambi. Adamu na Eva hawangewapa watoto wao kile wasicho kuwa nacho. Asili ya Mungu ndani yao ilitoweka, na asili ya dhambi ilitawala. Asili ya dhambi ya Adamu ilipitishwa kwa vizazi vyake.

1 Wakorintho 15:22 Kwa maana kama vile katika Adamu watu wote wanakufa, vivyo hivyo katika Kristo wote watafanywa hai.

Asili ya dhambi hupitishwa kutoka kizazi hadi kikingine kupitia kwa mbegu ya Baba. Kwa kuwa kila mtu hapa duniani ana baba, mtume Paulo aliandika,

Warumi 3:23 Kwa kuwa wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Adhabu ya dhambi ni mauti ya kiroho, na hii ilisababisha mauti ya kimwili.

Warumi 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Warumi 5:12 Kwa hiyo kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja na kupitia dhambi hii, mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi....

Kuzaliwa Kwa Yesu

Yesu alikuja hapa duniani, akapajikwa kwa Roho Mtakatifu na kuzaliwa na bikra, ili kufanyika badala yetu. Kwa sababu ya kupajikwa kwake kwa kimiujiza, Yesu hakuwa na asili ya dhambi. Alikuwa na asili ya Mungu ndani Yake, ambayo mwanadamu alikuwa amepoteza.

Mathayo 1:20b "Yosefu mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Maria awe mke wako, kwa maana mimba aliyo nayo ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

Mathayo 1:23 "Tazama, bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli," maana yake, "Mungu pamoja nasi."

Mipango ya Mungu ya Upendo

Upendo wa Mungu kwa wanadamu haulinganishwi! Yohana na Paulo waliandika kuhusu hii.

Yohana 3:16 "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Warumi 5:8 Lakini Mungu aliudhihirisha upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.

Mpango wa upendo mkuu wa Mungu kwa wanadamu ulihuzisha kumtuma Mwana Wake wa pekee, Yesu, kuishi kama mwanadamu aliyekamilika, na kisha kwa Mwana Wake kuibeba adhabu ya dhambi za wanadamu.

1 Petro 3:18 Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu, mwenye haki kwa ajili ya wasio na haki, ili awalete ninyi kwa Mungu. Mwili wake ukauwawa, lakini akafanywa hai katika Roho.

Yesu alichukua nafasi yetu. Hukumu yote iliyokusudia kwetu, aliibeba. Alifanyika dhambi kwa ajili yetu ili tupokee haki Yake. Alizibeba dhambi zetu ili tusibebe sisi wenyewe.

2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Alichukua magonjwa yetu, maradhi na maumivu ili tusibebe sisi wenyewe.

Isaya 53:4,5 Hakika aliuchukua udhaifu wetu na akajitwika huzuni zetu, hata hivyo tulifikiri amepigwa na Mungu, amepigwa sana naye na kuteswa. Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.

YESU – MKOMBOZI WETU

Katika maandiko ya Agano la Kale, Ayubu alitoa unabii kuhusu Mkombozi atakayekuja.

Ayubu 19:25 Ninajua kwamba mkombozi wangu yu hai, naye kwamba mwishoni atasimama juu ya nchi.

Daudi aliandika,
Zaburi 19:14 Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako. Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu.

Isaya aliandika kuhusu Mkombozi mara kwa mara.

Isaya 44:6 "Hili ndilo asemalo Bwana, mfalme wa Israeli na Mkombozi, Bwana mwenye Nguvu: Mimi ni wa kwanza na Mimi ni wa mwisho, zaidi yangu hakuna Mungu."

Kukombolewa kutoka kwa Utumwa

Katika Agano la Kale, mtu akiwa katika matatizo ya kifendha angeweza kujiuza au jamii yake katika utumwa. Mtu huyu, au watu, angeweza kuwekwa huru ikiwa "angekombolewa" na jamaa au wao wenyewe iwapo wangepata fedha za kutosha. Wakati mwingine wangewekwa huru baada ya miaka ya kuhudumu, au kwa sababu ya tendo la ujasiri wangetenda.

Maandiko yanamtazama mwanadamu asiye na ukombozi kama mtumwa asiye na matumaini katika dhambi na shetani, bwana wao.

Kwa Damu Yake

Mwanadamu hangekombolewa na vitu vyovyote vyenye uasi. – si kwa fedha au dhahabu – si kwa tendo lolote wangetenda. Gharama ya ukombozi wao ilikuwa damu ya Mwana wa milele wa Mungu aliyefanyika mwili. Ilikuwa damu ya gharama ya juu mno, damu iliyo na uwezo mkuu mno hata kuziosha dhambi za wanadamu wote.

1 Petro 1:18,19 Kwa maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliuridhi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu viharibikavyo, yaani, kwa fedha na dhahabu, bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile ya Mwana kondoo asiye na dosari wala doa.

Kuwekwa Huru

Neno la Kigiriki la tafsiri "kukombolewa" katika msitari huu ilikazia kitendo cha kuweka huru au kurejeshwa kwa kununuliwa. Sisi, tulikuwa Wake katika kuumbwa, sasa tumekuwa wa mkombozi kwa kununuliwa.

Yohana 8:36 Hivyo mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli.

Yesu si tu alitukomboa, alituweka Huru! Alitununua kwa damu yake ya dhamani. Tulifanyika mali yake, na alikuwa na haki kisheria kutuweka huru.

Ili Kufanyika Wafalme na Makuhani

Neno la kiasili "agorazo" tafsiri yake "kukombolewa" katika msitari unaofuata maana yake ni "kwenda sokoni kununua." Yesu alitununua kutoka kwa utumwa ili kufanyika wafalme na makuhani ndani Yake.

Ufunuo wa Yohana 5:9,10 Nao wakaimba wimbo mpya wakisema: "Wewe unastahili kukitwaa kitabu na kuzivunja lakiri

zake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu Yako ukamnunulia Mungu watu kutoka katika kabila, kila lugha, kila jamaa na kila taifa. Wewe umewafanya hawa wawe ufalme na makuhani wa kumtumikia Mungu wetu, nao watamiliki katika dunia."

Hadi Milele

Neno la kijumla la, "exagorazo" tafsiri yake "kukombolewa" katika Wagalatia 3:13, maana yake "kununua kutoka kwa ili isirudishwe tena kamwe."

Wagalatia 3:13a Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria ...

Kwa kazi ya ukombozi ya Kristo kwa ajili yetu, tulinunuliwa kutoka kwa utumwa katika dhambi, kwa ukamilifu kabisa, hata tunaweza kuwa na ujasiri tusirejeshwe soko ya utumwa tena.

Hii hasa ilieleweka katika nyakati na siku za Kirumi ambao wangeuzwa kila mara kwa mnada na mabwana zao.

YESU – KITAMBULISHO CHETU

Kuunganishwa Pamoja Naye

Wakati tulipoweka imani yetu katika Yesu kama Mwokozi wetu, muujiza ulifanyika. Mungu Roho Mtakatifu alituunganisha pamoja Naye. Tulifanyika Mwili Wake.

1 Wakorintho 12:13 Kwa maana katika Roho mmoja wote tulibatizwa katika mwili mmoja, kama ni Wayahudi au Wayunani, kama ni watumwa au watu huru, nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.

Zababu ya kazi ya ukombozi wa Yesu haikuwa tu kuwa siku moja tuwe Naye mbinguni. Petro aliandika kuwa Yesu alitoa njia tunayoweza kuishi katika haki.

1 Petro 2:22,24 "Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana kinywani mwake. Yeye mwenyewe alizichukua dhambi, tupate kuishi katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa.

Alifanyika Dhambi Kwetu

Katika kazi ya ukombozi Yake kwa ajili yetu, Yeye "alifanyika" dhambi kwetu. Alizibeba dhambi zetu juu ya mwili wake msalabani.

2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Alifanyika Laana Kwa Ajili Yetu

Yesu alichukuwa laana iliyokuja kwa mwanadamu kwa ajili ya dhambi.

Wagalatia 3:13 Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, (kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti.")

Alizibeba Dhambi Zetu

Msalabani, Yesu alifanyika "mwanakondoo wa Mungu aondoaye dhambi za ulimwengu." Alizichukua dhambi zetu zote hadi chini ardhini ili sizikumbukwe na Mungu kamwe, daima.

Yohana 1:29 Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, "Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"

Zaburi 88:3,6,7 Kwa kuwa nafsi yangu imejaa taabu, na maisha yangu yanakaribia kaburi.

Umenitupa kwenye shimo lenye kina kirefu sana, katika vina vya giza nene. Ghadhabu imekuwa nzito juu yangu, umenigharikisha kwa mawimbi yako yote.

Tuliunganishwa pamoja Naye katika mauti Yake.

Warumi 6:6 Kwa maana twajua kwamba utu wetu wa kale ulisulibiwa pamoja naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa, nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi.

Kufanyika Hai

Baada ya kuzichukuwa dhambi zetu chini ya ardhi, Alifufuka kwa ushindi katika mauti, jehanamu, na kaburini. Alifanyika "mzaliwa wa kwanza katika kifo."

Wakolosai 1:18 Yeye ndiye kichwa cha mwili, yaani, kanisa, naye ni mwanzo na mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, ili Yeye awe mkuu katika vitu vyote.

"Alifanyika hai" katika Roho.

1 Petro 3:18 Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu, mwenye haki kwa ajili ya wasio na haki, ili awalete ninyi kwa Mungu. Mwili wake ukauwawa, lakini akafanywa hai katika Roho.

Wakati Yesu alipofanyika hai, tulifanywa hai pamoja naye.

Waefeso 2:5,6 Hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, (mmeokolewa kwa neema). Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu,

Wakati Yesu alipofanyika hai, alirejeshwa katika uhai kamili wa Baba. Alifanyika tena katika haki.

Warumi 3:26 Alifanya hivyo ili kuonyesha haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu.

Alifanyika Haki kwetu

Wakati wa wokovu, tulipewa haki ya Yesu. Tufanyika wenye haki kama vile Yesu alivyo mwenye haki.

Paul wrote,
2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Na sasa sisi tuliofanyika haki basi na "tuishi kwa haki."

Petro aliandika,
1 Petro 2:24a Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki.

Kama viumbe wapya katika Kristo Yesu, sisi si wenye dhambi tena. Tumefanyika wenye haki!

2 Wakorintho 5:17 Kwa hiyo kama nmtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

Kamwe hatutaishi katika hukumu na lawama. Tumefanyika wenye haki!

Basi hatuko tena katika mawazo ya dhambi. Bali tuwe na mawazo ya haki.

Basi tusimruhusu tena shetani kutuweka chini na kutushinda.

Tunatambua kuwa "sisi ni haki ya Mungu katika Yesu Kristo." Sisi tuko huru kutokana na lawama na hukumu.

Warumi 8:1 Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho.

Sisi tu viumbe vipya katika Kristo Yesu! Roho zetu ni zenye haki kama vile Mungu ni mwenye haki. Kila siku, roho zetu na miili yetu inabadilishwa katika sura ya Mwana Wake!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Yohana 5:24-27, ni kwa mamlaka gani Yesu alihudumu alipokuwa hapa duniani?

2. Eleza kazi ya Yesu kama Mkombozi wetu.

3. Je, tunawezaje kufanyika "wenye haki ya Mungu" katika Kristo?

Sura Ya Kuumbwa Upya

KATIKA KRISTO

Kulingana na mtume Paulo, tunampokea Kristo kama Mwokozi wetu, tunakuwa ndani ya Kristo. Tumefanyika viumbe vipya. Mambo yote yanafanyika upya maishani mwetu.

2 Wakorintho 5:17 Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

Punde tu tunapopokea Yesu kama Mwokozi wetu, Roho Mtakatifu anatuunganisha kwa Yesu Kristo. Tunaunganishwa pamoja Naye milele.

Mambo ya Zamani Yalipita

Tunapofanyika "katika Kristo," mambo ya zamani yanapita. Hii inamaanisha sehemu ya wengine wetu iliyokuwepo awali, haipo tena. Zile sehemu zilizotajwa kama "vitu vya zamani" hufa. Lakini pia, kunakuwa na kuzaliwa upya – mtu mpya wa kiroho huzaliwa.

Vitu Vyote hufanyika Upya

Mwamini mpya si yule mtu aliyekuwa awali. Yule mtu wa zamani hayupo tena. Yule mtu amepita. Vitu vyote vimefanyika upya.

Je, lingeshangaza vipi wakati tunasherehekea mtoto aliyezaliwa kisha mtu akauliza, "Vipi kuhusu maisha ya zamani ya mtoto huyu?"

Ungejibu, "Mtoto huyu amezaliwa vihi sasa. Hana maisha ya zamani!"

Ni vivyo hivyo ibilisi anapotukumbusha kuhusu kushindwa na dhambi za awali kabla ya kuzaliwa upya. Sehemu hiyo ya maisha yetu ya zamani imepita. Haipo tena! Kama viumbe vipya, hatuna zamani ambayo ibilisi anaweza kujenga mashtaka dhidi yetu. Paulo aliandika, "vitu vya zamani vimepita! Vitu vyote vimefanyika vipya!"

Kuzaliwa Mara ya Pili

Yesu aliponena na Nikodemo, Alisema ni lazima uzaliwe mara ya pili.

Yohana 3:7 Kwa hiyo usishangae ninapokuambia huna budi 'kuzaliwa mara ya pili'.

Kwanza, Nikodemo alifikiri kuwa Yesu anazungumzia kuhusu mwili wake kuzaliwa tena. Kisha, Yesu akaeleza kuwa sehemu ya mwili wa mwanadamu wa kupata kuzaliwa upya si mwili bali ni roho. Ilikuwa roho ya mwanadamu.

Yohana 3:5,6 Yesu akamwambia, "Amin, amin nakuambia, hakuna mtu yeyote anayeweza kuingia katika ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho. Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho.

Roho Mpya

Wakati wa wokovu, roho yetu mpya huwa kamilifu. Kamwe haitakuwa kamilifu au haki zaidi ya wakati huu.

Roho ni sehemu ndani yetu itakayoishi milele. Ni sehemu inayojali uwepo wa Mungu. Roho ya mwamini ni sehemu inayoshirikiana na Mungu kwa sababu ni ya haki kama vile Mungu ni mwenye haki.

"Roho ngumu" imeondoka! Mungu amutupatia "roho ya mwili." Ametupatia Roho isiyo gumu, nyepesi na yenye upendo. Ametupatia roho anayejali kuishi katika haki.

Ezekieli 11:19 Nitawapa moyo mmoja na kuweka roho mpya ndani yao, nitaondoa kutoka ndani yao moyo wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama.

Roho zetu zimekamilika katika Yesu. Mungu angependa kurejesha roho zetu kwa kuyafanya upya mawazo yetu. Mungu angependa kurejesha miili yetu katika afya kamili. Wakati wa wokovu, tulifanyika viumbe vipya. Mwili (mifupa, nyama, na damu) na roho (fikira, uwezo wa kuchagua, na hisia) havikubadilishwa kabisa, bali roho alifanyika upya na kamilifu wakati wa wokovu.

Paulo aliandika maneno ya kusisimua kwa Wafilipi – "Tenda wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka."

Wafilipi 2:12 Kwa hiyo, wapenzi wangu, kama vile ambavyo mmekuwa mkitii sikuzote, si tu wakati nikiwa pamoja nanyi, bali sasa zaidi sana nisipokuwapo. Utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka.

Tunajua kuwa wokovu ni bure; na msitari huu unahitilafiana na mingine hadi tunapoelewa kuwa wakati huo wa wokovu, roho zetu zimekamilika katika Kristo. Kutoka wakati huo, roho zetu hufanya kazi na Roho Mtakatifu ili kuyabadilisha mawazo na miili yetu katika sura ya Kristo. Inabadilishwa kila siku. Wokovu wetu unafanya kazi katika mawazo na miili yetu.

Paulo aliendelea,
Wafilipi 2:13 Kwa maana Mungu ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema.

Roho – Fedha – Afya

Ni vyema kuwa na ufunuo juu ya roho katika utu ni nini hasa katika Kristo Yesu. Ni bora tuelewe kuwa roho aliyeumbwa upya ni kamili na yenye haki kabisa machoni pa Mungu.

Kwa ufunuo huu na katika ufahamu wa kazi ya ukombozi ya Yesu kwa ajili yetu, tutaanza kutembea kwa afya katika roho na miili yetu.

Roho zetu zitaendelea wakati mawazo yetu yanafanywa upya kwa kusoma, kusikia, kutafakari, kuamini, kunena, na kulitenda Neno la Mungu.

Warumi 12:2 Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kufanya upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.

Wakati roho zetu zinabadilishwa – kufanana na sura Yake – tutafaulu, na mili yetu itakuwa na afya. Yohana aliandika kuhusu haya.

3 Yohana 1:2 Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako kama vile roho yako ifanikiwavyo.

HAKI YAKE MUNGU

Je, Mungu ni Mwenye Haki kiasi gani?

- ➢ *Yeye ni wa haki katika kuwa na katika njia zake zote.*
- ➢ *Haki Yake ni zaidi ya ukosefu wa dhambi au uwezo wa kutokutenda dhambi.*
- ➢ *Ni wema wa hali ya juu na usiokuwa na kifani amabo hauwezi kutazama dhambi au kuikaribia dhambi.*
- ➢ *Mungu hana uwezo wa kutenda dhambi.*

Mungu katika haki yake hangeweza kuipuuza dhambi ya Adamu na Eva na vizazi vyao, hata katika upendo Wake, angependa.

Warumi 3:25,26 Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu Yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki Yake, kwa sababu kwa ustahimili Wake alizichukua zile dhambi zilizotangulia kufanywa. Alifanya hivyo ili kuonyesha haki Yake wakati huu, ili Yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu.

Haki yake Mungu inaonekana katika imani.

Warumi 1:17 Kwa maana katika injili haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa, haki ile iliyo kwa njia ya imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa: "Mwenye haki ataishi kwa imani".

Haki Zetu

Hatuwezi kufanywa haki kwa matendo yetu wenyewe. Nabii Isaya anatoa picha nzuri ya haki zetu.

Isaya 64:6a Sisi sote tumekuwa kama mtu aliye najisi, nayo matendo yetu yote ya uadilifu ni kama matambaa machafu.

Chochote tufanyacho, hata tujaribu kwa bidii zote, bado itakuwa matambaa machafu machoni pa Mungu. Matendo yetu mema tuliyotenda kabla ya kuumbwa upya iliongeza tu matambaa machafu.

Haki Iliyoletwa

Yesu alipokufa msalabani, Alizichukua dhambi zetu zote – kukosekana kwa haki juu yake. Badala yake alitupatia haki yake. Je, ni ubadilishanaji ulioje!

Dhambi zetu zimewekwa Kwake.
Haki Yake kamili imewekwa juu yetu.

Wakati tulipoweka imani yetu juu ya Yesu Kristo kama Mwokozi wetu, roho zetu zilifanyika "haki ya Mungu."

Warumi 3:22 ...haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo kwa wote wamwaminio.

Neno "amini" ina maana kutegemea, kuegemea, na kutumainia kazi ya ukombozi ya Yesu kwa ajili yetu.

Paulo alitaja kuwa tulipozaliwa upya na kuumbwa tena, tulifanyika haki ya Mungu katika Yesu.

2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Tulipofanyika haki ya Mungu, si kuwa hatuwezi kutenda dhambi tu. Si kwa kuwa dhambi zetu zote zimesamehewa – hata kama inafurahisha hivyo. Tunapofanyika katika haki ya Mungu, ina maana kuwa roho zetu ni zenye haki kama vile Mungu mwenyewe ni mwenye haki.

Tumetangazwa kuwa wenye haki.
tumepokea haki kutoka kwa Mungu.

Sura ya Zamani ya Ukosefu wa Haki

Kuwa tuko na haki kama vile Mungu ni mwenye haki, ni vigumu kwa wengine kukubali. Tumefundishwa kwa utofauti sana na waalimu-wenye busara.

Wakristo wengi huishi maisha yao yote kwa kupigwa na kotosamehewa na lawama, bila kutambua kuwa wako ndani ya Kristo Yesu.

Kwa imani tunatakiwa kukubali na kuamini kuwa sisi ni haki yake Mungu. Tunapotambua zaidi kuhusu Mungu, tunakuwa tukitambua haki badala ya kutambua dhambi.

Tusijione tena kamwe kama "wenye dhambi waliookolewa kwa neema." Sisi si wenye dhambi tena! Sisi ni viumbe vipya!

Wakristo wengi hujikuta wakitenda dhambi kwa sababu wao huambiwa ni wenye dhambi.

Wamesikia mafundisho kuhusu dhambi mara kwa mara. Mawazo yao yameegemea dhambi kila mara. Hawajapokea ufunuo kuhusu haki, kwa hivyo dhambi bado inatawala maishani mwao. Kwa kupitia ufunuo wa haki yake Mungu, tunafanyika wenye ufahamu wa haki. Tunajiona kama vile Mungu anavyotuona. Tunajiona kama wenye ufahamu wa haki yaake Mungu kama vile Alivyo na haki. Kwa hivyo, dhambi haitawali tena miilini mwetu. Basi hatutendi dhambi tena kwa mazoea.

Tunaiona dhambi kama vile Mungu anaiona. Imepoteza mvutio kwa sababu tumepata ufunuo wa haki yake Mungu.

KWA KUBADILISHWA KWA SURA YAKE

Tunapoendelea kutembea katika ufunuo wa haki yake Mungu kama viumbe vipya katika Kristo Yesu, basi tunabadilishwa kwa kuyafanya upya mawazo yetu. Ni mafuatano ya mambo. Tunabadilishwa kila siku katika sura ya Mwanawe.

Warumi 8:29 Maana wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe, ili Yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.

Kukiri Dhambi

Sisi kama Wakristo tukitenda dhambi, tusiishi katika kushindwa, lawama na hukumu katika maisha yetu yote.

Punde tu tukigundua kuwa tumetenda dhambi, ni sharti tukiri dhambi hizo kwa Mungu, na kwa imani, kupokea msamaha Wake. Kisha tunaweza kuendelea kutembea katika haki, tukiwa huru kutoka kwa kutosamehewa na lawama.

1 Yohana 1:9 Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote.

Kukiri maana yake ni kukubaliana na Mungu kuhusu dhambi. Sisi, kama Mungu, lazima tuichukie dhambi. Tunakokaribia Mungu, ndipo tunapotembea katika ufunuo wa haki, basi tutaweza kujaribiwa mara chache kutenda dhambi.

Jifunze Kurejea

Tunapokosea katika sehemu fulani maishani mwetu, no sharti tujifunze kurekebisha na kurejea haraka. Kama bondia anapopigwa na kuanguka mkekani, tusilale hapo na kujihisi kushindwa. Bali, tujifunze kuruka toka kwenye mkeka kwa miguu yetu. Turejee na kuendelea mbele.

Tunapotenda dhambi, tusikubali mawazo ya hukumu, lawama, na kushindwa. Bali, kwa haraka tutubu dhambi zetu na kupokea msamaha. Kama bondia anayeshinda, tuamke na kuelekea katika ushindi.

Uweze Kubadilishwa

Roho zetu zina haki ya Mungu, lakini tutoe miili yetu kwa Mungu kila siku kama kafara inayoishi.

Warumi 12:1 Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana.

Roho zetu zinayo haki ya Mungu, lakini mioyo yetu ni sharti ibadilishwe kwa kuyafanya upya mawazo yetu katika ufunuo wa Neno la Mungu.

Warumi 12:2 Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.

Kuwa Na Ujasiri

Kwa ufunuo wa haki ya Mungu katika kuumbwa upya, tunaweza kwenda mbele ya kichi cha enzi cha Mungu kwa ujasiri. Tunajua kuwa Mungu atatusikia.

Waebrania 4:16 Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

Tunaweza kuja kwa Mungu kwa ujasiri bila shaka kwa sabau tunaielewa neema Yake. Tunatambua kile Yesu amefanya kwa niaba yetu. Tunajua kuwa tumesamehewa. Tunatambua kuwa sisi tu viumbe vipya katika Yesu Kristo. Tunajua kuwa sisi ni haki ya Mungu.

Uwe Hai

Kama viumbe vipya, tunayo maisha mapya ndani yetu. Maisha haya mapya ni maisha yale ya Kristo mwenye.

Waefeso 2:4,5a Lakini Mungu, kwa upendo wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu....

Ubinafsi wa awali uliotembea kulingana na njia ya ulimwengu huu haupo tena. Mtu mpya wa ndani amewekwa hai.

Waefeso 2:1-3 Kwa habari zenu, mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu, ambazo mlizitenda mlipofuatisha namna ya ulimwengu huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi ndani ya wale wasiotii. Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapo zamani, tukifuata tamaa za mwili na mawazo yake. Nasi kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu , kama mtu mwingine ye yote.

Ujazwe

Kama viumbe vipya, roho zetu zimejazwa na wema wa Mungu. Yote Alivyo – imetujaza. Utajiri Wake wote katika kipimo imefanyika yetu.

Waefeso 3:19 Na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wa Mungu.

Katika Biblia ya Ufafanuzi inasema,
... kuwa ujazwe (kila mahali ndani yako) kwa wema wote wa Mungu – [maana yake] ili upate utajiri kamili wa Uwepo wa Mungu, na kufanyika mwili uliojazwa kamili na kufurika na Mungu mwenyewe!

Kama viumbe vipya, hatuko na utupu tena. Badala yake, tumejazwa na Mungu! Tumefurika na Yeye.

Tunapoendelea katika njaa na kiu kwa ajili ya haki Yake, tutajikuta tumejazwa na haki zake Mungu hata katika roho na miili yetu.

Mathayo 5:6 Ni heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watatoshelezwa.

Kupokea Upendo Wake

Ni ufunuo mkuu ulioje kutambua kuwa Mungu hajakasirika nasi! Anatupenda! Hata tulipokuwa adui zake, alitupenda.

Yohana 15:12,13,14 Amri Yangu ndio hii: Mpendane kama mimi nilivyowapenda ninyi. Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi ni rafiki zangu mkifanya ninayowaamuru.

Kama viumbe vipya tukiwa na roho mpya ya nyama, tunafanya kwa haraka kile anatuamuru kufanya.

➢ *Kuwa Rafiki wa Mungu*

Je, ni furaha iliyoje kujua kuwa Mungu hakasiriki nasi. Sasa anasema, “ninyi ni marafiki zangu!” Sisi ambao awali tulikuwa adui Wake, tumerejeshwa Kwake katika Kristo. Sisi sasa tu rafiki zake na Yeye ni Rafiki yetu. Kama rafiki za Mungu, tunayo huduma ya kuunganishwa. Tungependa

wengine wakutane na Rafiki wetu, na kama sisi, wafanyike marafiki wake Mungu.

➢ *Kurejeshwa Kwake*

Kama viumbe vipya tumerejeshwa Kwake.

2 Wakorintho 5:17,18 Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya. Haya yote yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo na kutupatia sisi huduma ya upatanisho.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, nini maana ya kuumbwa kipya?

2. Eleza kwa kinaga ubaga haki Yake Mungu.

3. Eleza kwa kinaga ubaga haki ya kuumbwa upya.

Somo La Tano

Kuibadili Sura Yetu ya Kimwili ya Zamani

Uamuzi ni Wetu

Tunajifunza masomo haya, tutafika mahali ambapo itatubidi kufanya uamuzi. Je, tutaamini ufunuo wa Neno la Mungu, au tutashikilia mafundisho ya zamani ambayo tumepokea kwa miaka mingi?

Je, tutakubaliana na mtume Paulo alipoandika,
Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya. (2 Wakorintho 5:17)

Tumejifunza kuhusu jinsi tulivyoumbwa tuwe, kuhusu upendo wetu, Baba wa mbinguni, na kuhusu kazi ya ukombozi ya Yesu Kristo kwa niaba yetu. Sasa ni wakati wa kufanya uamuzi wa busara na kuingia katika yote ambayo Mungu ametuwekea.

Kuweka Kando Sura yetu ya Kimwili ya Zamani

Ni muhimu kuwa na sura nzuri ya kibinafsi. Tusimruhusu ibilisi kutupotosha kuwa hatufai kupokea baraka za Mungu. Tukifanya hivyo, tutapitia maisha bila ushindi. Tukiishi maisha ya kushindwa, hatutaweza kupigana na kuyanshinda mapepo. Hatutaweza kuishi katika maisha ya ushindi kama Wakristo na kuhudumu wengine vyema.

Kwa wengi wetu, lazima kuwe na wakati wa kuvua mtu wa zamani – mitindo ya zamani – na kuvaa sura ya kuumbwa upya kwa kuyafanya upya mawazo yetu.

Paulo aliandika kuhusu kuvua mtu wa zamani. Kitendo cha uamuzi.

Waefeso 4:22,23 Mlifundishwa kuuvua mwenendo wenu wa zamani, utu wenu wa kale, ulioharibiwa na tamaa zake za udanganyifu. Mfanywe upya roho ya nia zenu.

Kufaa Iliyo Mpya

Tunapovua mtu wa zamani, lazima tubadili mawazo yetu. Kufanya upya kutakuja tu ikiwa tutayabadili mawazo yetu kwa imani katika ufunuo wa Neno la Mungu.

Paulo aliendelea kusema katika msitari unaofuata.
Waefeso 4:24 Mkajivike utu mpya, ulioumbwa sawa sawa na mfano wa Mungu katika haki yote na utakatifu.

Tunapovua mtu wa zamani, sura ya kimwili ya zamani, na kufanya upya mawazo yetu katika ufunuo wa Neno la Mungu, tunavaa mtu mpya, kiumbe kipya.

Kiumbe kipya hajapungukiwa kwa kile ambacho anachoona katika hisia zile tano ufunuo mpya huishi katika imani. Kiumbe kipya hutambua kuwa yeye ameumbwa upya, ameumbwa kulingana na Mungu, katika haki na utakatifu.

Viumbe wapya hawajioni tena kama wenye dhambi. Wanatambua kuwa roho zao ni zenye haki na takatifu kama Mungu. Wanajua kuwa mioyo yao na mili inabadilishwa kwa sura ya Mwana katika haki ionekanayo na utakatifu katika matembezi yao kila siku.

NGOME ZA ZAMANI

Wakati wa kukua, Shetani aliweka ngome mbalimbali mawazoni mwetu. Sasa, hata tukiwa wazima, tunafikiri kuwa hatuwezi kufanya kitu fulani kwa sababu tuliambiwa tulipokuwa watoto kuwa hatuwezi. Maneno yanayoharibu yaliyonenwa kwa muda yamekuwa ngome inayotakiwa kuvunjwa.

Kutokutosheleza

Labda uliambiwa, “Aah, usijaribu kufanya hiyo; kakako mkubwa atalishughulikia.” Ulianza kuwaza, “Mimi sina uwezo kama kakangu.”

Kutokuwa wa Maana

Labda mwalimu alisema “Sielewi ni kwa nini hili ni tatizo kwako, wengine darasani hawana shida nalo.” Wazo lako la kwanza likawa “Mimi si mwerevu kama wengine darasani.”

Mtindo Ukufaao

Labda tumeamini yale wengine wamesema kuhusu asili yetu kijamii au kuhusu kundi la watu fulani tunaotambulika nao. Mambo haya ya kijumla huenda imekuwa mitindo itufaayo maishani mwetu.

Iwapo una nywele nyekundu, labda umesikia, “wenye vichwa vyekundu kila wakati wana hasira ya haraka.”

Mtindo mwingine labda ni, “Mama yangu alijawa na shaka kila wakati, kwa hivyo hivi ndivyo mimi nlivyo.”

Labda tulisikia na kuamini mambo mengi kuhusu utaifa au asili ya ujamaa wetu ambayo imetufanya kuamini kuwa hatuwezi kuwafikia wengine karibu nasi. “Wajerumani kila mara…” au Waholanzi kila mara…”

Ufunuo wa kuumbwa upya utatuweka huru kutokana na mawazo ya kutokuwa na maana au kutosheleza ambayo yameweka uvuli maishani mwetu hapo awali.

Chuki au Kupendelea

Ufunuo wa kuumbwa upya utatuweka huru kutokana na chuki ya utaifa. Tutaanza kuona waamini wenzetu wa kila taifa kama viumbe wapya katika Kristo.

Katika msitari unaofuata ufunuo wa Paulo kuhusu kuumbwa upya, aliandika,

2 Wakorintho 5:16a Hivyo tangu sasa hatumwangalii mtu ye yote kwa mtazamo wa kibinadamu.

Paulo pia aliwaandikia Wagalatia,
Wagalatia 3:26-28 Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani. Kwa maana wote mliobatizwa ndani ya Kristo, mmemvaa Kristo. Wala hakuna tena Myahudi au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani ya Kristo Yesu.

Ni lazima tujione pamoja na waamini wengine wote kama vile Mungu anavyotuona. Kama roho walioumbwa tena, sisi hatuko tena na utaifa wetu wa zamani au kundi la jamaa letu. Tumezaliwa katika jamii mpya, jamii ya Mungu. Basi hatutamtazama mtu mwingine kulingana na rangi ya ngozi yake. Tutajikubali wenyewe na wengine, kama viumbe wapya katika Yesu Kristo.

KUZIANGUSHA NGOME

Shetani angependa kuzitumia hisia za zamani za kudharauliwa, kutokuwa wa maana, na chuki kutushika katika utumwa. Sasa ni wakati wa kuziharibu ngome hizo.

Ziharibu

Ikiwa Mungu amedhihirisha ngome mawazoni mwako wakati wa mafundisho haya, unaweza kuzivunja sasa hivi. Sema kwa sauti,

Shetani, nakufunga katika jina la Yesu.
*Nakataa ngome hii ya ~ (*itaje*) ~ sasa,*
katika jina la Yesu.
Sitaikubali iendelee. Natoa fikira zozote na mawazo ambayo ni kinyume na ufunuo kutoka kwa Neno la Mungu kunihusu mimi,
kile naweza kutenda au kile naweza kupata kama kiumbe kipya katika Yesu Kristo!

Itachukuwa muda kuivunja tabia ya kuwaza au kusema mawazo ya zamani ya kinyume. Lakini, kila mara mawazo haya yanakuja mawazoni mwetu, lazima punde tuzikatae, tusizushe chini, na kuendelea kutangaza kile Neno la Mungu linaonyesha kuhusu kuumbwa upya. Kwa kufanya hivyo,

tabia hiyo itavunjwa na utakuwa huru. Anza kuwaza na kusema,

Neno la Mungu linasema mimi ni kiumbe kiumbe kipya
mimi ni katika jamaa ya Mungu na kuwa
hakuna_____ katika jamaa ya Mungu.
Vitu vya zamani vimepita.
Mimi mtu mpya katika Kristo!

Vunja Laana

Shetani huenda alishinda alipoweka laana juu ya jamii kupitia dhambi katika vizazi vilivyopita. Kwa mfano, mtu anapojitia kitanzi, roho wa kujiua husalia katika jamii hiyo hadi ivunjwe katika nguvu ya jina la Yesu.

Mtu anapoua mtu mwingine, kuna roho za uuaji zinazosumbua jamii hiyo kila kizazi.

Kuna laana za kizazi au roho wa kurithi ambayo hufungua mlango wa magonjwa aina fulani zinazojishikilia katika mili yetu. "Aah, ndiyo, matatizo ya moyo hupita katika jamii zetu." Au "Wanawake wote katika jamii yetu hupata saratani."

Laana ya kizazi ni rahisi kuivunja kama ngome katika akili zetu. Sema,

Shetani, nakufunga katika jina la Yesu!
Ninavunja laana ya _____, _____
na _____!
Ninaamuru laana zote za kizazi na kila roho mwovu wa kurithi ili kuvunjwa juu ya maisha yangu sasa hivi.

Mimi ni kiumbe kipya! Mimi ni mtoto wa Mungu!
mimi ni sehemu ya jamii mpya!
Mimi ni sehemu ya jamii ya Mungu!
na hakuna tena utumwa,
hakuna laana, hakuna magonjwa katika Jamii ya Mungu!

Wakati mawazo au dalili za utumwa huo, laana, au magonjwa hujaribu kukuja kwako, zikemee! Ikiwa umekuwa ukikubali dalili, zikemee mara moja na uanze kutangaza kwa ujasiri kile ambacho Neno la Mungu linasema kuhusu uhuru wako.

KUIBADILI SURA YA ZAMANI YA KIMWILI

Kuendelea kushikilia sura yetu mbaya ni dhambi. Hatutaki kuwa kama wale mtume Paulo alieleza.

Warumi 1:21,22 Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao

ya ujinga ikatiwa giza . Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga.

Sisi ni wale Mungu anasema tuko. Kwa sababu Yesu alikufa ili kutuweka huru kutokana na vitu hivi, kuendelea kuvishikilia ni matusi kwa Mungu.

Kutokuwa Wa Maana

Waamini wengi wanakuwa na ukosefu wa usalama kuhusu uwezo wao. Wanaugua kutokana na hofu mbaya ya kushindwa. Neno la Mungu lasema,

Wafilipi 4:13 Naweza kuyafanya mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.

2 Timotheo 1:7 Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na moyo wa kiasi.

Ni sharti tutangaze bila kukosa,

Ninaweza kutenda mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu.
Ninajua Mungu amenipa roho wa nguvu,
wa upendo na akili iliyo timamu.

Umbo la Nje

Wengi hujihisi kukosa usalama kuhusu umbo lao, wakiwaza na hata kusema, “Mimi niko mnene sana,” “Mimi ni mwembamba sana,” kama ttu nywele yangu ingekuwa rangi tofauti,” “ningependa sana iwe nyofu.” Wao wana aibu au huwazia sana juu ya umbo lao.

Utafiti unaonyesha kuwa karibu warembo wengi wanaoshindana katika mambo ya urembo na wanaotawala katika sinema huhusi kuwa kuna kitu wangependa kubadilisha kuhusu umbo lao.

Katika maeneo yetu, kuna mkazo juu ya umbo la nje. Lakini Neno la Mungu linadhihirisha kuwa sisi ni nafsi za kiroho tulioumbwa katika sura ya Mungu. Tuliumbwa ili kuonekana kama Mungu. Urembo wetu upo ndani ya roho ya mtu – mwu mwenyewe – roho wetu aliye ndani yetu. Tunaweza kuinu vichwa vyetu na kuachilia urembo na mng’aro wa Yesu kuonekana usoni mwetu.

Wakati nabii Samueli alipokuja Bethlehemu kumpaka mmoja wa watoto wa Yesse ili awe Mfalme atakayefuata, alistaajabika sana na urembo wa mtoto wa kwanza. Nafasi za heshima mara nyingi zilienda kwa mtoto wa kwanza wa kiume, na basi mara tu aliona kuwa yeye huenda achakuliwe na Mungu awe mfalme. Lakini Bwana alimzuia.

1 Samweli 16:7 Lakini Bwana akamwambia Samweli, “Usitazame sura yake wala kimo chake, kwa kuwa nimemkataa. Bwana hatazami katika vile vitu mwanadamu avitazamavyo.

Mwanadamu hutazama katika sura ya nje, lakini Bwana hutazama moyoni."

Kukosa Elimu

Wengine hujihisi kukosa usalama wanapokosa elimu; lakini, Neno la Mungu linaonyesha kuwa katika Kristo, tumepata hazina ya hekima na maarifa. Maarifa ya kweli ni kumjua Mungu.

Wakolosai 2:2,3 ...kusudi langu ni kuwa watiwe moyo na kuunganishwa katika upendo, ili wapate kujua ulivyo utajiri wa ufahamu kamili, waijue siri ya Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, ambaye ndani Yake kumefichwa hazina yote ya hekima na maarifa.

Hisia za Kukataliwa

Ni kwa nini tunawaona waamini wengi leo wanaoteseka katika kukataliwa, na hisia za kukataliwa, wakiwa na majeraha ya kimawazo rohoni mwao?

Mungu alisema,
Waefeso 1:5-7 ...alitangulia kutuchagua tuwe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo kwa furaha Yake na mapenzi Yake mwenyewe. Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake.

Ikiwa "tumekubalika katika Wapendwa," basi tusiruhusu hisia za kukataliwa kutujia. Basi lazima tuwe na ulinzi katika maarifa yetu ya kukubali katika Yesu Kristo.

Mungu Baba anatukubali na upendo ule kama vile anavyokubali Mwana Wake mwenyewe, Yesu. Lazima tuyaweke chini mawazo ya kukataliwa na kutafakari juu ya Neno hadi tuwe na hakikisho la kukubalika kwetu. Kwa sababu Mungu anatukubali, tunaweza kuwakubali wengine.

Unyenyekevu wa Uongo

Mara nyingi kuna kiburi cha kiroho ambacho kimejitokeza kwa miaka mingi ambacho kimakosa kimeitwa kunyenyekea.

Tunaimba nyimbo kwa maneno kama"Mimi ni mwenye dhambi aliyepotea na kuokolewa kwa neema." Hiyo si kweli. Mara tu tukiookoka hatuko tena wenye dhambi waliopotea"!

Kwa miaka tuliimba maneno ya wimbo maarufu wa zamani uliokuwa na msemo "kwa mdudu kama mimi." Hivi sivyo Mungu anavyotuona! Hii ni kinyume na Neno la Mungu. Sisi si wadudu maskini wa mavumbi. Sisi ni viumbe wapya! Tu ndani ya Kristo! Sisi tunabadilishwa kwa sura Yake.

Sura ya kibinafsi isiyo na maana kama vile kiburi inaweza kuleta kushindwa maishani mwetu.

Kuwaza jinsi tusivyo na maana inaweza kuwa kielelezo cha unyenyekevu, lakini inajenga ngome za kushindwa juu ya maisha yetu ambayo hutuzuia kugundua uwezo wetu katika Yesu Kristo.

Unyenyekevu Wa Kweli

Unyenyekevu wa kweli unatokana na kuitambua neema ya Mungu. Unyenyekevu ni kutambua kuwa katika siku za awali, tulipokuwa maadui wa Mungu, tusiostahili upendo Wake mkuu, Alitukomboa ili tufanyike wale Alivyotuumba tuwe.

Unyenyekevu wa kweli ni kuwaza mema kuhusu Mungu. Ni kutambua kuwa yote tuliyo na yote tutendayo ni kwa ajili ya neema Yake kuu na rehema juu yetu.

Ni kweli kuwa hatutakiwi "kuwaza juu yetu zaidi ya vile tunaitajika," na hata hivyo tusiwaze juu yetu wenyewe china ya vile tunaitajika kuwa.

Ikiwa tutajiona kama Yesu na kutenda kazi ya Yesu, ni lazima kwanza tuizushe chini ile sura ya zamani ya kutokuwa wa maana, "siwezi tenda" na kuzibadili na sura za kuumbwa upya.

KUIBADILI SURA YA UTUMWA

Wengi wanayo sura ya utumwa. Wanajiona wakiishi katika ufukara ya mtumwa. Hajajiona wakipokea baraka na mali kwa Mungu. Hajajiona kama wana wa Mfalme.

Mfano wa Wana wa Israeli

Misri, wana wa Israeli hawakujua chochote kando na utumwa kwa mamia ya miaka. Kama wana wa Mungu waliokombolewa, waliitaji ufunuo kuhusu wao ni nani kama wana wa Mungu wa agano.

➢ *Dhahabu, Fedha*

Mungu alitaka kuibadili sura yao ya binafsi kutoka umaskini ya mtumwa hadi ile ya viumbe wapya ya wana wa Mungu waliokombolewa. Aliwaamuru waulize Wamisri dhahabu na fedha na vitambaa na vipuli vyenye gharama ya juu.

Hawakutakiwa kuviweka dhahabu na fedha mbali katika masanduku. Hawakutakiwa kuweka vitambaa vyenye urembo na kwa ajili ya kuvitenga viwe salama waliposafiri katika jangwa. Mungu aliwaamuru waweke fedha, na dhahabu, na vitambaa juu ya watoto wao.

Kutoka 3:21,22a "Nami nitawapa hawa watu upendeleo mbele ya Wamisri, kwa hiyo mtakapoondoka nchini hamtaondoka mikono

mitupu. Kila mwanamke Mwisraeli atamwomba jirani yake Mmisri na mwanamke ye yote anayeishi nyumbani kwake ampe vyombo vya fedha, dhahabu na nguo, ambavyo mtawavika wana wenu na binti zenu."

Wana Waisraeli – watu wa Mungu waliochaguliwa – hawakutoka nje ya Misri wakiwa na matambara ya utumwa. Mavazi na vyatu, ambavyo havikuisha wakiwa njiani kuelekea nchi ya ahadi, yalikuwa mavazi na johari ya mali nyingi.

Mungu aliibadili sura ya binafsi ya zamani. Alikuwa akiivunja sura yao ya utumwa ya zamani.

➢ *Kupata Zaidi*

Baadaye, wakati ulipofika wa kujenga mahali patakatifu, palikuwa na dhahabu na fedha nyingi mikononi mwa wana Waisraeli hata na kuwa walitoa vingi mno. Wakamwuliza Musa kuwazuia wasotoe zaidi.

Kutoka 36:5-7 Ili kuja kumwambia Musa, "Watu wanaleta zaidi kuliko mahitaji kwa ajili ya kazi hii ambayo Bwana ameagiza ifanyike."

Ndipo Musa akatoa agizo, nao wakapeleka neno hili katika kambi yote: "Mtu ye yote mwanaume au mwanamke asilete tena kitu chochote kwa ajili ya sadaka ya mahali patakatifu." Hivyo watu wakazuiliwa kuleta zaidi, kwa sababu walivyokuwa navyo tayari vilitosha na kuzidi kuifanya kazi yote.

Katika njia hiyo hiyo Mungu aliibadili sura ya wana Waisraeli wenyewe, anataka kuibadili sura yetu ya zamani ya umaskini na utumwa katika dhambi. Angependa tupate furaha ya wokovu.

KUYAZUSHA CHINI MAWAZO

Je, tunawezaaje kuiondoa sura ya zamani ambayo haimpendezi Mungu?

Je, tunaweaje kukiondoa kifungo cha kutokuwa wa maana, kukosa usalama, hisia za kutokutosheleza, lawama, hukumu na kutokuwa wa dhamana?

Je, vipi tunaeweza kuyashughulikia mawazo haya ya kudhania katika maisha yetu?

Neno la Mungu linatupa jibu.

2 Wakorintho 10:5 Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.

Mawazo ya kudhania yapo akilini mwetu. Ni sharti tuyaongoze mawazo yetu na kuzusha chini kila wazo ambalo ni kinyume na Neno la Mungu.

Vita vipo akilini mwetu – katika roho zetu, katika fikira zetu na katika uwezo wa kuchagua. Ni katika sehemu hizi ndipo tutashinda vita au kushindwa. Mawazo yetu ni sharti yafanywe upya kwa Neno la Mungu.

Ni sharti tuzilete kwenye utumwa kila wazo na kulifanya kumtii Yesu. Ni sharti tuchukue uongozi na kuyafanya mawazo yetu kutii ufahamu wa sisi ni nani katika Kristo.

Kama Nyoka

Ikiwa nyoka wa sumu kali angeanguka kutoka mtini na kujikunja mkononi mwetu, hatutasimama hapo na kumwangalia anapojiandaa kutuuma na kuweka sumu ndani yetu. Hapana! Tutarusha mkono wetu mara moja na kwa haraka tuwezavyo. Litakuwa jambo la ghafla, la uamuzi, kitendo cha haraka. Tutamvuta chini nyoka huyo kabla aume.

Vivyo hivyo, ni lazima, kwa dharau, tuyavute mawazo yanayodhania chini ya sura ya zamani. Lazima tupige kelele, "nakataa wazo hilo katika jina la Yesu!"

Wakati mawazo yetu ya zamani inaposema,
"Huwezi kufanya hilo wewe ni mwoga sana."

Tunasema
"Nakataa wazo hilo katika jina la Yesu.
Ninaweza kufanya mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu."

Wakati akili zetu za zamani zinaposema,
"Wewe una saratani."

Tunasema,
"Nalikataa wazo hilo katika jina la Yesu.
Neno la Mungu linasema,
Hakuna pigo litakuja karibu na makao yangu.
Ninajua kuwa kwa mapigo ya Yesu mimi nimepona."

Silaha Kuu

Tunazo silaha kuu za kuvunja ngome juu ya maisha yetu.

Mtume Paulo aliandika,
2 Wakorintho 10:4a Silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu...

Tunasizusha na kukataa fikira zinazodhania na ambazo ni kinyume na ufahamu wa Mungu, tunaziharibu nguvu zake juu yetu.

KUIVUA SURA YA BINAFSI YA ZAMANI

Njia ya kuivua sura ya binafsi ya zamani inaelezwa na mtume Paulo kama katika kitabu cha Wakolosai.

Wakolosai 3:9,10 Msiambiane uongo kwa maana mmevua kabisa utu wenu wa kale pamoja na matendo yake, nanyi mmevaa utu mpya unaofanywa upya katika ufahamu sawasawa na mfano wa Mwumba wake.

Baadaye, kwa ufunuo wa Neno la Mungu, "kuvua mtu wa zamani" na "tunavaa mtu mpya," ambaye anafanywa upya ufahamu katika sura ya Muumba.

Kuyafanya Upya Mawazo Yetu

Hatuwezi kuibadili jinsi roho yetu inavyofanya kazi kwa hisia zetu wakati wa wokovu. Hiyo ni hatua ya kwanza tu. Tunayafanya upya mawazo yetu na kubadilishwa katika sura ya muumba tunapotafakari juu ya Maandiko.

Warumi 12:2 Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.

Paulo aliandika kuwa mwanadamu ni sura na utukufu wa Mungu.

2 Wakorintho 3:18 Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.

Ikiwa tuliumbwa katika mfano wa Mungu, na kama viumbe vipya tumerejeshwa katika sura ya Mungu, basi ni matusi kwa Mungu kuendelea kusema mambo yaliyo kinyume kutuhusu.

Tusiongee juu yetu kama vile tumefanya awali. Sisi ni viumbe vipya. Tunabadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu.

KUZUSHA CHINI SURA YA PANZI

Sura ya "Naweza-Kutenda"

Ikiwa tutaishi maisha ya Kikristo yenye ushindi, yanayofaulu, inatupasa kuyabadili sura yetu ya "siwezi-tenda" na ile ya "naweza-kutenda." Ni bora kuelewa kuwa tunaweza kutenda kile Neno la Mungu linasema tunaweza kutenda.

Mfano wa Majasusi Kumi na Wawili

Mungu aliahidi kuwapa wana Waisraeli nchi ya Kanani. Siku ikafika ambapo Mungu alisema atumwe mtu mmoja kutoka kwa kila kabila kuitembelea nchi na kuleta taarifa. Mwisho wa siku arobaini, wakarudi na taarifa yao.

Hesabu 13:27,28a,30-33 Wakampa Musa taarifa hii: "Tuliingia katika nchi uliyotutuma, nayo inatirika maziwa na asali! Hili hapa tunda lake.

"Lakini watu wanaoishi huko niwenye nguvu na miji yao ina ngome na ni mikubwa sana."

Sisi Tunaweza

Kisha Kalebu akawanyamazisha watu mbele ya Musa na kusema, "Imetupasa kupanda na kuimiliki nchi, kwa maana hakika tunaweza kufanya hivyo."

Sisi Hatuwezi

Lakini watu waliokuwa wamepanda pamoja naye wakasema, "Hatuwezi kuwashambulia wale watu, wana nguvu kuliko sisi." Wakaeneza taarifa mbaya miongoni mwa Waisraeli kuhusu nchi walioipeleleza. Wakasema, "Nchi tulioipeleleza hula watu waishio ndani yake. Watu wote tuliowaona huko ni majitu."

"Tuliwaona Wanefili huko (wazao wa Anaki wanatokana na Wanefili.) Tulijiona kama panzi machoni petu wenyewe, nao ndivyo walivyotuona."

Tofauti Ni Mungu

Kalebu na Yoshua walikuwa na ufunuo kuhusu Mungu alikuwa nani. Walinena kama watu walio viumbe wapya wanatakiwa kunena. Walisema, "hebu na twende mara moja na kuinyakuwa nchi na mali, kwa maana tunaweza kuishinda."

Waliendelea,

Hesabu 14:8,9 Ikiwa Bwana anapendezwa nazi, atatuongoza kuingia katika nchi ile, nchi itiririkayo maziwa na asali, naye atatupa nchi hiyo.

Ila tu msimwasi Bwana. Wala msiwaogope watu wa nchi hiyo, kwa sababu tutawameza. Ulinzi wao umeondoka, lakini Bwana yupo pamoja nasi. Msiwaogope.

Watu wengine kumi waliona hali hiyo hiyo kama vile Kalebu na Yoshua. Wao, hata hivyo, hawakuyaweka macho yao kwa ukuu wa Mungu. Walitazama uwezo wao wa kawaida na kujiona kama panzi. Wao walijiona kuwa na "sura ya panzi."

Uamuzi Wetu

Leo, tunaitajika kuzusha chini sura yetu ya panzi na kuibadilisha na sura ya kuumbwa upya. Kama Kalebu na yoshua, ni lazima tuweke imani yetu katika ukuu wa Mungu na kuanza kusema, “tunaweza kabisa kuichukua nchi yetu!”

Kwa wengi, sura yetu ya zamani imekuwa kizuizi kikuu kinachotuzuia kuwa, kupata, na kutenda yote Mungu amekusudia kwetu kama viumbe vipya.

Nilazima kwa ujasiri tunene kwa mlima wa hali tofauti na kusema, “Na uondoke na kutupwa baharini!”

Mathayo 21:21 Yesu akawajibu, “Amin, amin nawaambia, kama mkiwa na imani wala msiwe na shaka, si kwamba mtaweza kufanya tu yale yaliyofanyika kwa huu mtini, bali hata mkiuambia huu mlima, ‘Ng’oka, ukatupwe baharini,’ nalo litafanyika.

Silaha za vita vyetu ni kuu katika Mungu na kuvuta chini ngome. Ngome za sura yetu ya binafsi ambayo itaporomoka na kuanguka. Tutafanyika wale ambao Mungu amesema tuko. Kama viumbe vipya, sura ya binafsi ya zamani itapita na vitu vyote, na pia sura yetu tuliyogundua mpya, itafanyika upya.

2 Wakorintho 5:17 Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, nini baadhi ya ngome za zamani za sura ya kibinafsi ambazo ume “yavuta chini” baada ya masomo haya?

2. Eleza njia iliyotajwa katika Wakolosai 3:9,10 kama kuvua mtu wa zamani na kuvaa mtu mpya.

3. Je, tunawezaje kuyafanya mawazo yetu upya kama ilivyotajwa katika Warumi 12:2?

Sura Yetu Katika Kristo

JAMII YETU KATIKA KRISTO

Kuzaliwa Upya

Wakati tunapokea Yesu Kristo kama Mwokozi, "tumezaliwa mara ya pili" katika jamii ya mpya ya Mungu.

Yesu alimwambia Nikodemo,
Yohana 3:7 Kwa hiyo usishangae ninapokwambia huna budi 'kuzaliwa mara ya pili.'

Yesu alimfafanulia Nikodema kuwa Yeye hakuwa akizungumzia kuzaliwa kimwili, bali "kuzaliwa tena" maana yake ni kuzaliwa katika roho.

Yohana 3:5,6 Yesu akamwambia, "Amin, amin nakuambia, hakuna mtu yeyote anayeweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho. Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho."

Kabla ya kupokea Yesu kama Mwokozi, wakati tulikuwa hai katika miili yetu (mifupa, nyama na damu) na nafsi (akili, hangaiko la moyo na uwezo wa kuchagua) tulikuwa tumekufa kiroho. Wakati wa wokovu "tulizaliwa mara ya pili" kiroho. Roho zetu zilifanyika hai. Tulifanyika viumbe wapya katika Yesu Kristo.

Tulizaliwa katika jamii mpya, jamii ya Mungu. Tulipozaliwa katika jamii ya Mungu, tulifanyika Wana wake.

Wana wa Mungu

Mtume Yohana aliandika,
1 Yohana 3:1a Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu!

Tukielewa kuwa tu watoto wa kiume na wa kike wa yule aliye na nguvu sana, aliye na maarifa, Baba mwenye hekima nyingi duniani, basi tutagundua kuwa maisha yetu, vyeo, haki, manufaa, na mambo ya baadaye yamebadilika kabisa.

Kuelewa uhusiano wetu wa kijamii kama wana wa wa Mungu inaweza kuibadili jinsi tunavyowaza kutuhusu.

Paulo aliandika,
Warumi 8:14 Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu hao ndio watoto wa Mungu.

Tunapompokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi, tunafanyika wana wa Mungu.

Yohana 1:12 Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake.

Neno "haki" maana yake mamlaka. Mara tu tunapoamini, tunapata mamlaka kisheria kufanyika mwana wa kiume au wa kike wa Mungu.

Wana wa Urithi wa Mungu

Mungu hajatufanya tu watoto Wake, pia ametupatia urithi pamoja na zawadi kama vile Yesu. Sisi ni warithi pamoja na Kristo.

Warumi 8:17a ...basi ikiwa sisi ni watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja Naye Kristo....

Mali na vitu vya Baba ni zaidi ya kipimo, na vyote alivyo navyo Baba ni vya Mwana.

Je, linastaajabishaje kugundua kuwa sisi, baada ya kuzaliwa katika jamaa ya Mungu, tumefanyika warithi pamoja na Yesu Kristo. Urithi Wake wote umefanyika urithi wetu.

Utajiri wote wa mbinguni ni wa Yesu, na kwa sababu sisi tu warithi pamoja Naye, basi utajiri wote mbinguni ni wetu.

Waefeso 1:3 Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo.

Kupata Kushika Urithi Wetu

Kwa imani katika Yesu, tumezaliwa katika jamaa ya Mungu, na kufanyika wana wa Mungu. Kama wana wa Mungu, tunapokea urithi wa ahadi.

Wagalatia 3:26 Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani.

Ezekieli 46:16 "Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo: 'Ikiwa mkuu atawalaye atatoa zawadi kutoka kwenye urithi wake na kumpa mmoja wa wanawe, hiyo zawadi itakuwa pia kwa wazao wake, itakuwa mali yao kwa urithi."

Kama viumbe wapya, ni lazima tunyakue vitu vyetu. Lazima tupate kushika vyote vilivyo vyetu katika haki.

Kupokea Ufadhili Wetu

Ni jambo la kustaajabisha mno kugundua juu ya fadhili zetu kama wana wa kiume na wa kike wa Baba wa mbinguni. Je, ni furaha ilioje kugundua kuwa si lazima tungoje mpaka tutakapofika mbinguni ndipo tuanze kufurahia urithi wetu.

Mtume Paulo aliandika,
Wafilipi 4:19 Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.

Tunaweza kuanza kufurahia urithi sasa kama viumbe wapya, kwani tayari "tumezaliwa upya" "katika jamaa ya Mungu."

Kama viumbe wapya, watoto wa Mungu, na warithi pamoja na Yesu Kristo, hatustahili kulia na kumwomba Mungu kujibu maitaji yetu hapa duniani. Vyote alivyonavyo Mungu ni tayari vyetu. Kile tu tunaitajika kufanya ni kutambua jinsi ya kupokea utajiri wa Mungu kwa imani na kutii.

➢ *Nguvu ya Kupata Utajiri*

Musa alinena maneno haya kwa wana Waisraeli,
Kumbukumbu La Torati 8:18 Lakini kumbukeni Bwana Mungu wenu, ndiye ambaye huwapa uwezo wa kupata utajiri na hivyo kulithibitisha agano lake ambalo aliwaapia baba zenu, kama ilivyo leo.

➢ *Asili ya Kutoa*

Ni asili ya Baba kutoa.

Yohana aliandika,
Yohana 3:16a Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa .....

Kwa sababu tu watoto wa Baba, ni bora iwe ndani yetu asili mpya ya watoaji.

Yesu alisema,
Luka 6:38 Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa.

➢ *Nyumba ya Uekezaji Baraka*

Tunapotoa kwa Mungu kwa imani na kutii, tunampa Mungu kipimo cha kutumia kutubariki. Kwa hivyo maitaji yetu yote yanajibiwa kutoka kwa nyumba ya uekezaji ya urithi wetu wa milele.

Katika kitabu cha Malaki tunasoma,
Malaki 3:10 "Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Nijaribuni katika hili, asema Bwana Mwenye Nguvu, nanyi mwone kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka nyingi mpaka mkose nafasi ya kutosha au la."

Je, ni furaha ilioje kujuwa kuhusu kupokea baraka zetu kama viumbe vipya wana wa Mungu wa kiume na wa kike.

MWILI WA KRISTO

Kama viumbe wapya, sisi hatufanyiki tu sehemu ya jamii ya Mungu, bali kwa muujiza wa kuzaliwa upya, tunafanyika sehemu ya mwili wa Kristo.

Mtume Paulo aliandika,
1 Wakorintho 12:27 Sasa ninyi ni mwili wa Kristo na kila mmoja wenu ni kiungo.

Waamini wote, kwa jumla, wanajumlisha mwili wa Kristo. Sisi, kila mmoja, ni washirika wa mwili huo.

Sisi ni Sehemu ya Muhimu

Mungu anayo nafasi kwa kila mwamini katika mwili Wake. Anayo kazi itambulikayo tuikamilishe.

Ms. 18 Lakini kama ilivyo, Mungu ameweka viungo katika mwili, kila kimoja kama alivyopenda.

➢ *Tunawaitaji Wengine*

Kila mwamini katika mwili wa Kristo anawaitaji wengine.

Ms. 21,22 Jicho haliwezi kuuambia mkono, "Sina haja nawe!" Wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu, "Sina haja na ninyi!"Lakini badala yake, vile viungo vya mwili vinavyoonekana kuwa dhaifu, ndivyo ambavyo ni vya muhimu sana.

Ms. 26 Kama kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia pamoja nacho, kama kiungo kimoja kikipewa heshima, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.

Kila sehemu ya mwili wa Mungu ni muhimu! Kama vile mwili wa mwanadamu ulivyo na uwezo wa kulinda, kusaidia, na kuumba, basi pia mwili wa Kristo.

NAFASI YETU KATIKA KRISTO

Wakati wa wokovu, Roho Mtakatifu alitubatiza katika Yesu Kristo. Kwa muujiza kwa kuzaliwa upya, tulifanyika wa katibu na Yesu. Tuliunganishwa pamoja Naye.

1 Wakorintho 12:13 Kwa maana katika Roho mmoja wote tulibatizwa katika mwili mmoja, kama ni Wayahudi au Wayunani, kama ni watumwa au watu huru, nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.

Neno Ubatizo maana yake ni:

➢ *Ni kutambulika kabisa na*

Wakati wa wokovu, tunatambulika na Yesu Kristo.

Wakati kipande cha kitambaa cheupe kinapowekwa katika rangi nyekundu, kitambaa huchukua rangi hiyo. Inakubaliana na rangi hiyo kwa sababu "inabatizwa" ndani yake. Katika hali hiyo hiyo, roho zetu huchukua hali ya Mwana wa Mungu tunapobatizwa ndani Yake na Roho Mtakatifu wakati wa wokovu. Tunatambulika Naye kabisa – kushikamana Naye kwa karibu-sehemu ya mwili Wake-pamoja Naye.

Yote alivyo Yesu, sisi tupo!
Vyote alivyo navyo Yesu ni vyetu!
Yote tulivyo na kuwa navyo ni
kwa sababu tu ndani Yake.

Kama inavyofundishwa katika Waefeso

Paulo alitaja nafasi zetu na vilivyo vyetu "katika Kristo" mara nyingi katika sura tatu za mwanzo katika barua yake kwa Waefeso.

➢ *Kubarikiwa na Baraka za Kiroho*

Aliandika kuwa tumebarikiwa na kila baraka ya kiroho katika Kristo.

Waefeso 1:3 Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo.

Baraka zote za mbinguni zenye utajiri, utukufu, na zinazotosheleza zipo kwa ajili yetu ili tupokee na kufurahia maishani mwetu kila ziku.

➢ *Kuchaguliwa ndani Yake*

Baba alimchagua Yesu. Yeye ni yule Aliyechaguliwa. Kwa sababu sisi tu ndani Yake, basi tunashiriki katika kuchaguliwa Kwake.

Waefeso1:4 Kwa maana alituchagua katika Yeye kabla ya kuumbwa ulimwengu ili tuwe watakatifu na bila lawama mbele Zake.

Mungu hakutuchagua kwa ajili ya sura zetu, uwezo, au umuhimu wetu wa kibinafsi. Alituchagua kwa sababu mile tangu, alituona katika Kristo.

➢ *Kutengwa Ndani Yake*

Tunashiriki katika Mwisho Wake kwa sababu tu ndani Yake.

Waefeso 1:5 Kwa upendo alitangulia kutuchagua tuwe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo kwa furaha Yake na mapenzi Yake mwenyewe.

Hatujatengwa ili tuwe na Mungu milele kwa sababu Yeye anatupenda zaidi ya vile anawapenda wengine. Baba angetazama katika vizazi na kutuona katika Kristo. Alituchagua kwa sababu alimchagua Kristo, nasi tu wamoja Naye.

Urithi wetu na kutengwa kwetu ni kwa sababu ya nafasi yetu katika Yesu Kristo.

Waefeso 1:11 Katika Kristo sisi nasi tumepata urithi, tukiisha kuchaguliwa sawasawa na kusudi la Mungu, Yeye ambaye hufanya mambo yote kulingana na mapenzi Yake.

➢ *Kukubalika ndani Yake*

Tumekubalika katika Mpendwa. Kukubalika kwetu na Baba ni kwa sababu tuko ndani ya Kristo.

Waefeso 1:6 Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa.

Kukombolewa kwetu, kusamehewa, na utajiri wote wa neema Yake ni kwa sababu tuko ndani Yake.

Waefeso 1:7 Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake.

➢ *Tumefunikwa ndani Yake*

Tumewekwa na mhuri wa Roho Mtakatifu kwa sababu alituunganisha, na milele kutufanya moja na Yesu Kristo.

Waefeso 1:13 Ninyi pia mliingia ndani ya Kristo mliposikia Neno la kweli, Injili ya wokovu wenu. Mkiisha kuamini, ndani yake mlitiwa muhuri, kwa yule Roho Mtakatifu wa ahadi mliyeahidiwa.

➢ *Kuketi Pamoja Naye*

Kwa sbabu tu moja Naye, tumeketi pamoja Naye mbinguni.

Waefeso 2:6 Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu.

Hata kama tunaishi katika mili yetu hapa duniani, katika Kristo tumeketi mbinguni. Yesu alipokamilisha kazi Yake ya ukombozi, aliketi katika mkono wa kuume wa Baba.

Zaburi 110:1 Bwana amwambia Bwana wangu: "Keti mkono wangu wa kuume, mpaka niwafanye adui zako kuwa mahali pa kuweka miguu yako."

Paulo alidhihirisha kuwa tumeketi Naye mahali. Tunafurahia faida zote ya kazi Yake iliyokamilika hapa duniani. Sisi, kwa imani, tunafurahia kila wakati pumziko lipatikanalo kwa kila mwamini, hata katika dhoruba maishani.

➢ *Kazi Nzuri ndani Yake*

Tumeumbwa katika Kristo Yesu kwa kazi nzuri.

Waefeso 2:10 Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo.

Adamu na Eva waliumbwa kwa kusudi, nasi katika Kristo tumeumbwa kwa kusudi hilo pia. Tumeumbwa kutenda kazi Yake hapa duniani. Sisi ni mwili wa Kristo utendao kazi hapa duniani mahali Pake.

Yesu alipokuwa hai na akihudumu dunaiani, aliwaambia waamini Wake,

Yohana 14:12 Amin, amin, nawaambia, ye yote aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya, naam na kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa sababu Mimi ninakwenda kwa Baba.

Kama waamini katika Kristo, sisi tu mwili wa Yesu. Sisi tu miguu Yake, nyayo, na mikono Yake hapa duniani. Kama mwili wa Yesu sisi tunaendelea kutenda kazi Yake leo.

Mwili wa Kristo:

- *Huwakilisha Kristo ulimwenguni*
- *Huleta upendo wa Mungu ulimwenguni*
- *Huleta uponyaji wa Mungu na ukombozi*
- *Huleta watu katika ufahamu wa Mungu uokoao*

➢ *Kufanywa Kumkaribia*

Sisi, tuliokuwa adui wake na mabali sana Naye, "tumefanywa karibu" kwa damu Yake kwa sababu tu ndani Yake.

Waefeso 2:13 Lakini sasa katika Kristo Yesu, ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa mbali na Mungu, sasa mmeletwa karibu kwa njia ya damu ya Kristo.

Sasa tunaweza kufurahia, ushirika wa karibu unaoendelea pamoja Naye.

➢ *Kufanyika Moja*

Tunapoumbwa ndani Yake, uadui wote kati yetu na Mungu uliondolewa. Sisi wawili ghafla tukafanyika moja.

Waefeso 2:15 Kwa kuibatilisha ile sheria pamoja na amri zake na maagizo yake alipoutoa mwili wake, ili apate kufanya ndani yake mtu mmoja mpya badala ya hao wawili, hivyo akifanya amani.

Mtu aliyeumbwa upya hawezi kutenganishwa na Yesu na amani Yake, kadri anapoendelea kuwa ndani Yake.

➢ *Hekalu Takatifu*

Ndani Yake, tunajengwa pamoja kama hekalu takatifu, kama pahali anapokaa Mungu Mwenyewe.

Waefeso 2:20-22 Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ndiye jiwe kuu la pembeni. Ndani Yake jengo lote limeshikamanishwa ili kuwa hekalu takatifu katika Bwana. Katika Yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja ili mpate kuwa makao ambayo Mungu anaishi ndani yake kwa njia ya Roho Wake.

Je, ni furaha ilioje kugundua kuwa Mungu amechagua kukaa nasi hapa duniani. Amechagua kuishi ndani yetu kila mmoja na kuishi ndani yetu kama kanisa Lake.

Kwa sababu tu ndani Yake, pamoja Naye, kuunganika kabisa Naye, kama viumbe wapya tunashiriki katika yote alivyo na vyote Alivyo navyo..

Haki Yake imefanyika haki yetu. Mwisho Wake umefanyika mwisho wetu. Uhai Wake umefanyika uhai wetu.

Wakati tulipokea ufunuo wa kuzaliwa upya, tunaweza kusema kwa ujasiri,

Ninajua mimi ni nani katika Kristo!
Nnimefanyika pamoja Naye!
Sasa nina shiriki haki Yake,
Ajali Yake, na uhai Wake!

Mimi ni kiumbe kipya!
Mambo ya zamani yamepita!
Vitu vyote vimefanyika vipya!

Waefeso 3:12 Yeye ambaye ndani Yake na kwa njia ya imani katika Yeye tuweze kumkaribia Mungu kwa ujasiri na kwa uhuru.

Tunaweza kuja kwenye uwepo Wake kwa ujasiri kwa uhuru kwa sababu tu ndani Yake, basi hatuko tena katika hukumu au lawama. Sisi ni viumbe vipya. Sisi ni haki Yake Mungu katika Yesu Kristo.

Wana wa Mwanga

Yesu alikuwa Mungu katika mwili. Yesu alitumwa katika dunia hii ya giza la kiroho kama nuru ili kuonyesha upendo wa Mungu na nguvu kwa wale watakaoamini ndani Yake.

Yohana 8:12 Kisha Yesu akasema nao tena akawaambia, "Mimi ni nuru ya ulimwengu. Mtu ye yote akinifuata hatatembea gizani kamwe bali atakuwa na nuru ya uzima."

1 Wathesalonike 5:5 Ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa mchana. Sisi si wana wa giza wala wa usiku.

Waamini waishi kama wana wa mwanga. Inawapasa waishi katika ushindi kulingana na nuru ya ufunuo wa Neno la Mungu. Paulo anatuagiza kwa kusema,

Waefeso 5:8 Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, lakini sasa ninyi ni nuru katika Bwana. Enendeni kama watoto wa nuru.

Kuoshwa, Kutakaswa, kuthibitishwa

Kama viumbe wapya, tumewekwa huru kutoka kwa dhambi. Tumeoshwa, kutakaswa, na kuthibitishwa.

1 Wakorintho 6:10,11 ...wala wezi, wala wenye tamaa mbaya, wala wafiraji, wala walafi, wala walawiti, wala wanaodhihaki, wala wanyang'anyi. Baadhi yenu mlikuwa kama hao. Lakini mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa haki kwa jina la Bwana Yesu Kristo na katika Roho wa Mungu wetu.

Kuoshwa, ni kufanywa safi. Mungu hataruhusu uchafu mbele ya uwepo Wake. Haki kamili haiwezi kukaa na dhambi.

1 Yohana 1:7 Lakini tukienenda nuruni, kama Yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana Wake yatasafisha dhambi yote.

"Kutakaswa" hueleza uhusiano watu wanaweza kupata kwa Mungu kwa imani katika Kristo. Ina maana kuwa tumewekwa mbali na uovu, na kutengwa kwa ajili ya Kristo. Tumetengwa na ulimwengu, na tuna uhusiano na Mungu unaotokana na haki Yake ndani yetu.

Tumeoshwa na kutakaswa. Pia tumefanywa haki. Kuthibitishwa ina maana kutangazwa kisheria kuwa haki na Mungu. Tu wenye haki; roho zetu ni kamilifu mbele za Mungu. Katika Kristo sisi tu viumbe wapya. Dhambi za awali zimetoweka – zimeoshwa katika damu ya Yesu.

Warumi 3:28 Kwa maana twaona kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa njia ya imani wala si kwa matendo ya sheria.

Warumi 8:31b,33 Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani awezaye kuwa kinyume chetu?

Ni nani atakayewashtaki wale ambao Mungu amewachagua? Ni Mungu mwenyewe ndiye mwenye kuwahesabia haki.

Wakati Shetani na umati wake wanapokuja na kutukumbusha yaliyopita, lazima tuseme,

Sahau hayo, Shetani,
Nimeoshwa, kutakaswa, na kuthibitishwa!
Mimi ni kiumbe kipya!
Mambo ya zamani yamepita!
Vitu vyote vimefanyika upya!

URAIA WETU MPYA

Haki Zetu

Kama viumbe wapya, tunao uraia mpya.

Raia wa nchi amehakikishiwa haki fulani za kitaifa chini ya katiba ya taifa. Katiba ni sheria tamati ya nchi. Sheria zingine zote za taifa hutegemea haki za kimsingi za kikatiba. Tusipojua haki zetu, tunaweza kunyanyaswa na watu wapotovu.

Kama viumbe wapya, tumepewa haki za kitaifa nyingi, lakini tunaweza kunyanyaswa na shetani. Tunaweza kuteseka bila sababu. Kuwa kiumbe kipya haimaanishi kuwa tutafurahia baraka zetu zote za kiroho, lakini hutupatia haki kisheria kuziagiza.

Silaha Zetu

Katika dunia hii, Shetani amenyakuwa haki zetu kama viumbe wapya. Lakini, Mungu ametupatia silaha za kiroho tunazoitaji kurejesha haki hizo.

Paulo aliandika kuwa silaha zetu si za hapa duniani, na kuwa zina nguvu za kiungu, zenye nguvu hata kuvuta ngome chini.

2 Wakorintho 10:4 Silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome.down strongholds...

Ngome ni kama eneo lililotengwa kama boma. Inashikilia sana juu ya hali zote, fikira, watu au mashirika. Inaweza kuwa ngome ambayo Shetani amejenga juu ya afya au fedha. Hata iwe ngome ya aina gani, tuna silaha za kuizusha chini!

➢ *Ili Kutekelesha Kikamilifu*

Hakuna silaha iliyo kamili iwapo haitatumika.

Iwapo adui angemshambulia mtu aliyejihami, bado atamwumiza ikiwa mtu huyo hatatumia silaha zake. Mtu aliyeshambuliwa anaweza kujihami toka kichwani hadi vidole miguuni, lakini asipotumia silaha zake, anaweza kushindwa.

Ni vivyo hivyo kwetu sisi kama viumbe wapya. Tunaweza kufikia silaha tutakazoitaji kumshinda adui, lakini lazima tuzitambue na pia jinsi ya kuzitumia.

➢ *Kueleza kwa Wazi*

Paulo alieleza silaha na sana za vita kwa kiumbe kipya katika kitabu cha Waefeso.

Waefeso 6:11-17 Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba mweze kuzipinga hila za Shetani.

Kwa maana kushindana kwetu si juu ya nyama na damu, bali dhidi ya falme, mamlaka, dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.

Kwa hiyo vaeni silaha zote za Mungu ili mweze kushindana siku ya uovu itakapokuja nanyi mkiisha kufanya yote, simameni imara.

Kwa hiyo simameni imara mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani, nayo miguu yenu ifungiwe utayari tuupatao kwa Injili ya amani. Zaidi ya haya yote, twaeni ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu.

➢ *Silaha Moja Ya Kupigana*

Kuna silaha aina mbili za kawaida, za kujikinga na kupigana. Baadhi ya silaha ni za kujikinga

tunaposhambuliwa, na moja ni kwa ajili ya kumshambulia adui.

Upanga wa Roho – Neno la Mungu – ni silaha ya kupiga iliyotajwa katika kifungu hiki cha maelezo. Tunaponena Neno la Mungu kwa imani, ibilisi lazima aachilie. Yeye hana kinga dhidi ya silaha hii.

Mungu ametupatia silaha hii, lakini lazima tujifunze kuitumia. Kama viumbe wapya, lazima tunene Neno la Mungu kwa hali ambazo zinajaribu kutuvuta chini.

Kumalizia

Tunayo sura Mpya katika Kristo.

Kwa muujiza wa kuzaliwa upya, tumezaliwa katika jamii ya Mungu. Kama wana wa Mungu wa kiume na wa kike, tumefanyika warithi pamoja na Kristo. Vyote vilivyo vyake sasa ni vyetu kushiriki.

Tuko ndani Yake, na kwa sababu ya cheo chetu kipya, tumebarikiwa na baraka zote za kiroho, kuchaguliwa, kukusudiwa, kukubalika, kufunikwa, na kuketi pamoja Naye.

Tumeumbwa katika Kristo kutenda matendo Yake mema hapa duniani. Sisi, tuliokuwa adui Wake wakati fulani, tumeruhusiwa kuwa na ushirika wa karibu pamoja Naye. Sisi ni hekalu Lake takatifu. Tuna ujasiri mpya na uhuru kwa sababu ya imani yetu ndani Yake.

Sisi tuliokuwa gizani sasa tunaelezwa kuwa watoto wa nuru. Tumeoshwa, kutakaswa, na kuthibitishwa. Tunazo haki za utaifa kama viumbe wapya. Lazima tuvae silaha kamili ya Mungu ili kurejesha urithi wetu, faida zetu, na haki zetu kama viumbe wapya katika Yesu Kristo.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. je, ni nini maana ya kuzaliwa upya?

2. Je, ina maana gani kwako “ndani ya Kristo”?

3. Je, ina maana gani kwako kuwa sehemu ya watoto wa nuru?

Haki za Kuumbwa Upya

KAMA WATOTO WA IBRAHIMU

Mtume Paulo aliandika kuwa ikiwa sisi ni wa imani, sisi ni watoto wa Ibrahimu. Hii ni ya muhimu kwa sababu kama watoto wa Ibrahimu, tunazo haki nyingi na fursa za kihaki.

Wagalatia 3:6,7 ... Kama vile Abrahamu, "Yeye alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa haki." Hivyo basi mjue kwamba wale wanaomwamini Mungu hao ndio watoto wa Abrahamu.

Haki ya Ibraham

Mungu alimtazama Ibrahimu kama mwenye haki sio kwa sababu ya matendo yake mema, maisha ya kipekee, au faida yake kuu, bali kwa sababu Ibrahimu alikuwa na imani. Ibrahimu hakuwa amekamilika, lakini alikuwa mwenye haki kwa ajili ya imani yake.

Si lazima tuwe tumekamilika ili kuwa na haki yake Mungu. Hata hivyo, lazima tumwamini Mungu na kupokea haki Yake kwa imani, kama vile Ibrahimu alifanya.

Katika ulimwengu wa unaoonekana, sisi ni wa baba wetu wa hapa duniani, kuzaliwa katika jamii inayolibeba jina lake. Tunapozaliwa tena katika imani, tunazaliwa katika jamii ya imani na tunayo haki ya kutumia jina la jamii – jamii ya Ibrahimu.

Ahadi Zake Mungu kwa Ibrahimu

Mungu alipomwita Abramu (baadaye akaitwa Ibrahimu) kutoka Haran, alimpa ahadi nyingi; na kwa sababu tu katika jamii ya Ibrahimu, tunaweza kushiriki katika ahadi hizi.

Mwanzo 12:1-3 Bwana akawa amemwambia Abramu, "Ondoka katika nchi yako, waache watu wako na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha."

"Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki, Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka. Nitawabariki wale wanaokubariki, ye yote akulaaniye nitamlaani na kupitia kwako mataifa yote duniani yatabarikiwa."

Sisi tumehesabika katika baraka za Ibrahimu! Tunaweza kuzichukua ahadi hizi kuwa zetu.

Ukoo Wake

Mungu alimwahidi Ibrahimu idadi kubwa ya uzao. Mbegu yake ingekuwa kama nafaka ya mavumbi duniani – kwa kuguzia mbegu yake ya kimwili.

Mwanzo 13:16 Nitaufanya uzao wako uwe mwingi kama mavumbi ya nchi, hivyo kama kuna ye yote awezaye kuhesabu mavumbi, basi uzao wako utahesabika.

Mungu pia alimwambia Ibrahimu kuwa ukoo wake watakuwa wengi kama vile nyota angani – kuguzia mbegu yake ya kiroho kwa imani.

Mwanzo 15:5 Akamtoa nje na kusema, "Tazama juu kuelekea mbinguni na uhesabu nyota, kama hakika utaweza kuzihesabu." Ndipo akamwambia, "Hivyo ndivyo uzao wako utakavyokuwa."

Agano Linalodumu Milele

Mungu aliweka agano la kudumu na Ibrahimu na ukoo wake. Kwa imani, sisi ni ukoo wake na tu sehemu ya agano hili la kudumu.

Mwanzo 17:7 Nitalithibitisha agano langu kama agano la milele kati yangu na wewe na wazao wako baada yako na vizazi vijavyo niwe Mungu wako na Mungu wa wazao wako.

Yesu, mbegu ya Ibraham

Tukiwa ndani ya Yesu, sisi ni warithi katika ahadi za baraka ya Mungu kwa Ibraham. Sisi tu warithi katika agano la Ibrahamu.

Wagalatia 3:16 Ahadi zilinenwa kwa Abrahamu na kwa mzao wake. Maandiko hayasemi, "Kwa wazao," likimaanisha watu wengi, bali "Ni kwa mzao wako", yaani mtu mmoja, ndiye Kristo.

Wagalatia 3:29 Nanyi mkiwa ni mali ya Kristo, basi ninyi ni wa uzao wa Abrahamu na warithi sawasawa na ile ahadi.

BARAKA ZETU KATIKA IBRAHAMU

Sisi ni watoto wa Ibrahamu – ukoo wake wa kiroho – na kwa imani tunaweza kupokea baraka. Ikiwa ni lazima tupokee baraka hizi kwa imani, ni lazima tuzitambue.

Orodha ya Baraka

Kumbukumbu La Torati 28:1-14 Kama ukimtii Bwana Mungu wako kwa bidii na kufuata amri zake zote ninazokupa leo kwa bidii, Bwana Mungu wako atakuweka juu ya mataifa yote katika dunia. Baraka hizi zote zitakuja juu yako na kukupata, kama ukimtii Bwana Mungu wako:

Utabarikiwa mjini na utabarikiwa mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, mazao ya nchi yako na wanyama wako, wachanga wa kufugwa, ndama wa makundi yako ya ng'ombe na wanakondoo wa makundi yako. Kapu lako na vyombo vyako vya kukandia vitabarikiwa. Utabarikiwa uingiapo na utabarikiwa utokapo.

Bwana atakujalia adui wainukao dhidi yako watashindwa mbele yako. Watakujia kwa njia moja lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.

Bwana ataagiza baraka juu ya ghala zako na juu ya kila kitu utakachogusa kwa mkono wako. Bwana Mungu wako atakubariki katika nchi anayokupa. Bwana atakufanya kuwa taifa lake takatifu kama alivyokuahidi kwa kiapo, kama ukishika maagizo ya Bwana Mungu wako na kwenda katika njia zake. Kisha mataifa yote ya dunia wataona kuwa unaitwa kwa jina la Bwana, nao watakuogopa.

Bwana atakupa kustawi kwa wingi, katika tunda la uzao wa tumbo lako, wanyama wachanga wa mifugo yako na mazao ya ardhi yako, katika nchi aliyowaapia baba zako kuwapa.

Bwana atafungua mbingu, ghala zake za baraka, kukupa mvua kwa majira yake na kubariki kazi zako zote za mikono yako. Utakopesha mataifa mengi lakini hutakopa kwa ye yote. Bwana atakufanya kichwa, wala si mkia. Kama utazingatia maagizo ya Bwana Mungu wako ninayokupa siku hii ya leo na kuzifuata kwa bidii, daima utakuwa juu, kamwe hutakuwa chini. Usihalifu amri zangu zo zote ninazokupa leo, kwa kwenda kuume au kushoto, kwa kufuata miungu mingine na kuitumikia.

Zimepewa Kwetu

Ahadi hizi alipewa Ibrahimu kwanza, kisha kwa ukoo wake wa kimwili, na kisha zikapewa ukoo wake wa kiroho – wale ambao ni wa imani.

Wagalatia 3:6,7,14 .... Kama vile Abrahamu, "Yeye alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa haki." Hivyo basi mjue kwamba wale wanaomwamini Mungu hao ndio watoto wa Abrahamu.

... ili kwamba baraka aliyopewa Abrahamu ipate kuwafikia watu Mataifa kwa njia ya Kristo Yesu, ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Roho.

Kwa Leo

Gundua kuwa ahadi alizopewa Ibrahimu ni za sasa, sio tutakapofika mbinguni. Ni za leo.

Hebu tuchukue muda kumshukuru Mungu kwa ajili ya baraka zetu za kuumbwa upya.

Baba, nakushukuru kuwa nimebarikiwa jijini
na kubarikiwa mashambani.
nimebarikiwa popote nilipo.

Nakushukuru kuwa matunda ya uzao wangu
imebarikiwa,
watoto wangu wamebarikiwa.

Nakushukuru Bwana
kuwa mifugo wangu wamebarikiwa nawe.

Nakushukuru Bwana
kuwa kikapu changu kimejaa
kuwa nina chakula cha kila siku.

Nakushukuru Bwana kuwa nimebarikiwa
ninapoingia na kubarikiwa ninapotoka nje.
Ninajua kuwa adui anapojaribu kuja
dhidi yangu, tayari ameshindwa.
Atakuja dhidi yangu kutoka upande mmoja,
lakini atatimuka katika pande saba.

Bwana,nakushukuru kuwa yote nifanyayo itadumu.
Ninaenda kutembea katika njia zako,
kesho, na kila siku ya maisha yangu.

Nakushukuru Bwana kuwa watu wataona
jinsi ulivyo mkuu maishani mwangu.

Nakushukuru Bwana kuwa utanipa
maendeleo makuu.

Nakushukuru Bwana kuwa umefungua
nyumba ya baraka mbinguni,
na kuwa ninaweza kuipokea hapa duniani.

Nakushukuru Bwana kuwa numenifanya
niwe kichwa na si mkia –
umeniweka juu na wala si chini.

Ewe Baba, nakushukuru kwa baraka zako zote!
Sitaacha kukufuata, Bwana.
sitawatumikia miungu wengine.
Nitaziweka amri zako.
Katika jina la Yesu, Amina

UHURU KUTOKANA NA SHERIA YA DHAMBI NA MAUTI

Kuokolewa kwa Neema

Paulo alitaja kuwa dhambi haina tena mamlaka ya kisheria juu ya wale wanaokiri Yesu kama Bwana na Mwokozi wao.

Basi hatuishi tena chini ya sheria. Tumeokoka – kukombolewa – si kwa sheria, bali kwa neema.

Warumi 6:14 Kwa maana dhambi haitakuwa na mamlaka juu yenu, kwa sababu hampo chini ya sheria, bali chini ya neema.

Waefeso 2:8 Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Maelezo ya neema ni kuwa ni kupewa usichositahili – kitu tunachopewa tusichostahili.

Sio tu kuwa hatukustahili mapenzi ya Mungu, tulistahili kinyume cha hii. Waume kwa wake hawangeweza kuitimiza

sheria; na kwa hiyo, haingewaletea wokovu – ingeleta tu mauti.

Kuokolewa maana yake kuokolewa kutoka kwa kitu au kukombolewa kutoka kwa kitu. Je, tumekombolewa kutoka kwa kitu gani?

Huru Kutokana na Laana

Basi hatuko tena chini ya sheria ya dhambi na mauti, na hatuko tena chini ya laana ya sheria. Tumekombolewa kutokana na laana ya sheria; hata hivyo, tusipotambua haki zetu kama viumbe wapya, wakati Shetani au roho wa pepo wake wajapo kuweka laana juu yetu, tunaweza kushindwa. Lakini, tunapotambua haki zetu za kuumbwa upya, tunaweza kushinda kila vita.

Wakati mambo haya yanakuja dhidi yetu yakionekana kama sehemu ya laana, tunaweza kusema kwa ujasiri,

Nimekombolewa kutoka kwa laana ya sheria.

➢ *Yesu Alifanyika Laana*

Yesu alifanywa laana hii kwa ajili yetu! Yeye alichukua laana hizi juu ya mwili Wake kwa niaba yetu ili kutukomboa kutoka kwa laana hizi! Alituweka huru kutokana na kila aina ya laana hizi za kisheria alipolipia adhabu yetu msalabani.

Wagalatia 3:13 Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, (kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti.")

Yesu pekee ndiye aliyeweza kuiweka sheria kikamilifu. Aliishi maisha makamilifu chini ya sheria na akafanyika kafara iliyokamilika.

➢ *Kukombolewa Kutoka kwa Laana*

Ni muhimu kufahamu yanayojumlishwa chini ya laana. Je, Yesu alibeba nini kwa ajili yetu? Je, laana ya kisheria ni nini? Tunapojifunza sehemu hii, tutagundua kuwa tumekuwa tukikubali vitu kutoka kwa Shetani ambavyo haitupasi kupokea.

Musa aliorodheshwa kuwa vitu vilivyo sehemu ya laana katika Kumbukumbu la Torati 28:15-68. (Itakuwa bora kusoma sehemu hii yote) Musa pia aliorodhesha laana zitokanazo na kutokutii na ifuatayo ni kwa kifupi.

Kumbukumbu La Torati 28:15,20 Hata hivyo, kama hutamtii Bwana Mungu wako na kuzishika kwa bidii amri zake zote na maagizo ninayokupa leo, laana hizi zote zitakuja juu yako na kukupata:

Bwana ataleta laana juu yako, fadhaa na kukaripiwa katika kila kitu unachokigusa kwa mkono wako, mpaka umeangamia na

kuharibika ghafula kwa ajili ya maovu uliyoyafanya kwa kumwacha yeye.

Je, laana za sheria ni zipi? Je, adhabu ya kutokutii sheria ni ipi?

- ➢ *Maradhi*
- ➢ *Homa, inayowasha*
- ➢ *Joto kuu na kiangazi*
- ➢ *Uharibifu kwa mimea*
- ➢ *Anga ya shaba*
- ➢ *Ardhi ya chuma*
- ➢ *Mvua hugeuka vumbi na majivu*
- ➢ *Kushindwa*
- ➢ *Miili hufanyika chakula cha ndege na wanyama*
- ➢ *Ngozi kuwasha, upele, na maradhi ya ngozi*
- ➢ *Wazimu, upofu, kuchanganyikiwa akili*
- ➢ *Kushindwa katika yote tufanyayo, kuteswa, kuibiwa*
- ➢ *Kupoteza Wapendwa, nyumba, matunda ya kikazi*
- ➢ *Kupoteza mali, watoto*

Huu ni mwanzo tu wa orodha!

Kuangalia katika Maisha ya kawaida

Sasa, chukua muda usome laana za kisheria katika Kumbukumbu la Torati tena, lakini wakati huu kumbuka kuwa Yesu amekukomboa kutokana na laana ya sheria na uongeze maneno, "Yesu amenikomboa kutoka kwa _____ . Kwa mfano,

Yesu amenikomboa kutokana na magonjwa.
Yesu amenikomboa kutokana na maradhi yanayoua.
Yesu amenikomboa kutokana na homa na mwasho.
Yesu amenikomboa kutokana na jua kali na joto
Yesu amenikomboa kutokana na...

Tafuta katika Kumbukumbu la Torati 28 mambo ambayo Shetani ameweka juu yako. Hivi ni sehemu ya laana ya sheria na Yesu amekukomboa kutoka na laana hiyo!

Anza kukubaliana na Neno la Mungu,

Nimekombolewa na Yesu
kutokana na laana ya _____ .
Yesu alilipa adhabu ya dhambi.
ninaamuru kila dalili
ya laana hii kuniacha sasa!

Wakati Yesu alitundikwa msalabani, alifanyika laana kwetu ili tufanyike wenye haki. Yeye hakutupatia uzima wa milele

tu bali, Yesu alitupatia vyote ambavyo tunaitaji kuwa washindi katika maisha haya.

Wakati Shetani anapojaribu kuleta mojawapo ya laana hizo, tunasema,

Eeh, hapana Shetani!
Yesu ametukomboa kutokana na laana hiyo!

Uhuru juu ya Mambo ya Kale

Mara nyingi Shetani hutunasa katika kukubali mojawapo ya laana kwa kukubali kuwa tumetenda dhambi, na kuwa laana hii ni ya adhabu yetu kwa ajili ya dhambi hiyo. Tunaanza kuwaza kuwa tunastahili kile anaweka juu yetu.

Shetani husema kweli anapotwambia kuwa laana huja kwa ajili ya dhambi. Lakini Shetani hatukumbushi kuwa Yesu tayari alilipa adhabu ya dhambi hiyo, ili tusibebe dhambi hiyo tena au laana hiyo inayokuja baada ya dhambi hiyo.

2 Wakorintho 5:17 Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.

Kuishi Katika Ushindi

Kama viumbe wapya, tuko huru kutokana na sheria ya dhambi na mauti. Tumekombolewa kutoka kwa kila dhambi, kila adhabu, na kila laana.

Warumi 8:2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima katika Kristo Yesu imeniweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti.

Ikiwa tutatenda dhambi, lazima tukiri na kupokea msamaha.

1 Yohana 1:9 Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote.

Tunapokiri dhambi zetu, mara moja tunawekwa huru tokana na dhambi hiyo juu yetu. Tumeoshwa kutoka kwa wasio na haki. Shetani hawezi tena kutushinda katika mashtaka ya hukumu na laana.

Dhambi, laana zake, na sheria ya dhambi na mauti, haina haki ya kisheria kutushinda. Tunaweza kuishi na baraka za viumbe wapya maishani mwetu.

Tukiwa na Uwezo Kushinda

Ibrahamu alikuwa na imani na ikaesabika kwake kuwa mwenye haki. Kwa imani, tunaweza kupokea baraka alizopewa yeye.

Yesu alikuja na kuchukua laana ya sheria juu Yake mwenyewe. Kwa imani, tunapokea wokovu wetu. Kwa imani, tunaweza kuyashinda mambo ya ulimwengu huu. Imani inatupatia uwezo wa kushinda!

1 Yohana 5:4 Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu.

Kama viumbe wapya, tunakiri nguvu ya Mungu yenye ushindi ndani yetu. Uamuzi ni wetu kuruhusu nguvu hizi kutenda kazi ndani yetu au hapana. Tunaweza kuamua na kuliamini Neno la Mungu, au tunaweza kuamini hali na mazingira yetu.

Nguvu ya Mungu yenye ushindi inaachiliwa tunapoamini na kuachilia Neno Lake na kunena kwa ujasiri. Ni imani yetu katika Neno Lake ndiyo huleta ushindi kwetu.

Shetani hutuambia kuwa sisi tu wenye lawama, wenye dhambi wasio na manufaa, na kwamba hatuwezi dhidi ya magonjwa, maumivu, umaskini, na kuhangaika ambayo ni sehemu ya laana.

- ➢ *Mungu anasema sisi ni viumbe wapya, tukiwa huru kutokana na lawama, hukumu, na laana ya kisheria.*
- ➢ *Mungu anasema sisi tu warithi katika baraka za ahadi za Ibrahimu.*
- ➢ *Mungu anasema kama washindi, tunaweza kutembea katika baraka Zake tele.*

Tunaweza kuwa, tenda, na kuwa na vyote ambavyo Mungu ametoa kwetu kama waamini katika Yesu Kristo.

- ➢ *Ni lazima tuamue kumwamini Mungu badala ya uongo wa Ibilisi.*
- ➢ *Ni lazima tuamue kujiona kama vile Mungu anavyotuona.*
- ➢ *Lazima tuanze kutangaza yote ambayo Mungu amesema juu yetu.*

Kisha tunaweza kufurahia haki zetu kama viumbe wapya katika Yesu Kristo!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, kwa nini ni muhimu kufahamu kuwa sisi tunatoka katika jamii ya Ibrahimu?

1. Taja baadhi ya ahadi za agano Mungu aliweka na Ibrahimu ambazo ni muhimu kwako.

3. Kwa kutumia Kumbukumbu la Torati 28:15-68, andika ukurasa wa kutangaza ukitaja uhuru wako kutokana na laana za kisheria.

Faida Ya Kuumbwa Upya

Utangulizi

Ufunuo wa kuumbwa upya na haki yetu katika Yesu huleta faida nyingi kwa mwamini katika Yesu Kristo.

Zaburi 68:19a Sifa apewe Bwana, Mungu Mwokozi wetu, ambaye siku kwa siku hutuchukulia mizigo yetu.

USHIRIKA NA MUNGU

Mojawapo ya faida kuu ya kuumbwa upya ni kuwa tunaweza kutembea na Mungu kwa ujasiri na bila aibu katika uwepo Wake wa utukufu. Tunaweza kutembea pamoja Naye. Tunaweza kuwa na ushirika wa karibu Naye.

1 Yohana 1:3-7 Twawatangazia lile tulililoliona na kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo. Tunaandika mambo haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.

Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka kwake na kuwatangazia ninyi, kwamba Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza lo lote. Kama tukisema kwamba twashirikiana naye huku tukienda gizani, twasema uongo, wala hatutendi lililo kweli. Lakini tukienenda nuruni, kama Yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana Wake yatusafisha dhambi yote.

Ukiristo ni tofauti na dini zingine kwa kuwa tunampokea Kristo, tunaweza kuwa na uhusiano wa binafsi (kuwa sehemu ya jamii ya milele ya Mungu) na ushirika (wa karibu sana kila siku) na Mungu.

Kusudi la Mungu katika ukombozi ilikuwa kurejesha uhusiano Wake na mwanadamu, na kurejesha ushirika Naye.

Kufafanua

Kulingana na Kamusi (Webster's Unabridged Dictionary), baadhi ya maelezo ya ushirika ni:

- ➢ *Hali ya kuwa mwenza*
- ➢ *Uhusiano wa karibu kati ya watu wenye matakwa ya sawa na kirafiki*
- ➢ *Kuwa karibu sana*
- ➢ *Kuambatana pamoja*
- ➢ *Kufahamiana sana*
- ➢ *Kushirikiana kwa karibu*

Mwito

Tumeitwa kushirikiana na Mungu.

1 Wakorintho 1:9 Mungu ni mwaminifu ambaye mmeitwa naye ili mwe na ushirika na Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu.

Ni wazo la jabu lililoje. Mungu ametuita katika ushirika pamoja Naye. Mungu anataka kuwa na ushirika pamoja nasi!

Ushirika wetu wa karibu na Mungu ni bora utuelekeze kwa kiwango cha ushirika na ndugu na dada zetu katika jamaa ya Mungu. Mtume Yohana aliandika,

1 Yohana 1:3,4 Twawatangazia lile tulililoliona na kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo. Tunaandika mambo haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.

Huleta Furaha

Furaha ni matokeo ya ushirika wa karibu na Mungu usio na kizuizi, na pamoja na waamini wenzetu katika Yesu Kristo.

Zaburi 16:11 Umenijulisha njia ya uzima, utanijaza furaha katika uwepo wako, pamoja na furaha za milele katika mkono wako wa kuume.

Hakuna furaha iliyo kuu kuliko ile ipatikanayo katika ushirika wa karibu na Mungu Mwenyewe kupitia kwa Neno Lake. Yeremia aliandika,

Yeremia 15:16 Maneno yako yalipokuja, niliyala, yakawa shangwe yangu na furaha ya moyo wangu, kwa kuwa nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana Mungu, Mungu Mwenye Nguvu.

Mwamini, aliyepata ufunuo wa kuwa kiumbe kipya katika Yesu, amepata furaha.

Punde tu wale ambao waliosumbuliwa na mawazo ya kutokusamehewa, kuhukumiwa, na kutokuwa wa maana, wanapotambua ufunuo wa haki, wao hufunguliwa kutokana na utumwa hadi furaha iliyo kuu.

Ni wale tu ambao wana ustadi katika ufunuo wa kuumbwa upya wanaweza kupata furaha isiyo kifani ya ushirika wa karibu na Mungu bila hofu ya hukumu.

Daudi aliandika kuhusu furaha hii.
Zaburi 32:1,2 Heri mtu yule ambaye amesamehewa makosa yake, ambaye dhambi zake zimefunikwa. Heri mtu yule ambaye Bwana hamwesabii dhambi na ambaye rohoni mwake hamna udanganyifu.

Uhusiano Uliovunjika

Tunapotenda dhambi, uhusiano wetu na Mungu hauvunjiki. Tungali watoto Wake.

Kupitia dhambi, ushirika wetu Naye huvunjika. Kwa mara nyingine, dhambi imekuwa kizuizi kati yetu na Mungu. Lakini, kwa ajili ya rehema zake, Mungu alipata njia kwa ushirika wetu pamoja Naye urejeshwe mara moja.

Yohana aliandika,
1 Yohana 1:8-10 Kama tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu. Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote. Kama tukisema hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo na Neno lake halimo ndani yetu.

"Kukiri" maana yake ni kutaja. Tunaitajika kutaja dhambi zetu na wala si tujidanganye, kujaribu kuficha au kukataa kuwa tumetenda dhambi. Badala yake, kwa haraka tukubali na pia kwa Mungu kuwa tumetenda dhambi machoni pake na machoni petu.

Neno "dhambi" ina maana "kukosea alama". Tunatenda dhambi mara tu tunamokosea alama ya Mungu ambayo ni ukamilifu katika haki katika mawazo na matendo yetu.

The moment we recognize that we have "missed the mark," we must immediately confess our sin and receive God's forgiveness and cleansing from that unrighteousness.

➢ *Kutumia vibaya Neema ya Mungu*

Wengi wasio na ufunuo wa haki, wametumia vibaya neema ya Mungu. Wachukulia kimakosa kuwa ina maana wanaweza kutenda dhambi wanapotaka bora tu wakiri baadaye na kupokea msamaha wa Mungu.

Yohana aliweka wazi, alipoendelea katika msitari ufwatao, kuwa tusikubali dhambi iingie maishani mwetu.

1 Yohana 2:1 Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki.

Mwito wetu kwa Mungu ni mwito mbali na dhambi.

Faida nyingine ya mwamini aliyezaliwa mara ya pili - kiumbe mpya – ni ili tuwe na mafanikio ya kweli. Kuna aina mbili ya mafanikio, ile ya nafsi, na katika sehemu ya kifedha.

Kupitia mtume Yohana, Mungu aliandika kuwa anataka tufanikiwe na tuwe na afya nzuri – hata wakati nafsi zetu zinafanikiwa.

3 Yohana 1:2 Uzima huo ulidhihirishwa, nasi tumeuona na kuushuhudia, nasi twawatangazieni uzima wa milele, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao ukadhihirishwa kwetu.

Je, nini Mungu angependa zaidi ya yote? Kuwa tutafanikiwa na kuwa katika afya nzuri, hata wakati nafsi zetu hufanikiwa.

Je, nini maana "wakati nafsi yako hufanikiwa?"

Mafanikio ya Nafsi

Nafsi zetu ni fikira zetu, hisia zetu na uwezo wa kuamua kwetu. Mafanikio ya nafsi – mafanikio ya fikira na mafanikio ya hisio – hutokana na kujitolea kwetu maishani kama dhabihu inayoishi kwa Yesu, na kuyafanya upya mawazo yetu katika Neno la Mungu. Mafanikio ya nafsi ni mwanzo wa mafanikio na afya ya kimwili.

Warumi 12:1,2 Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana.

Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni Pake na ukamilifu.

Mungu anawataka watu Wake, viumbe Wake wapya, kufanikiwa katika nafsi na mwili. Viumbe wapya kamwe hawataishi katika mtindo wa ulimwengu huu. Wanatakiwa kufwata mtindo wa Neno la Mungu.

➢ *Ni Njia*

Viumbe wapya wako katika njia ya kubadilishwa na mabadiliko haya huja wakati mawazo yao hufanywa upya kwa kuendelea kusoma, kusikiliza, kutafakari, kuamini, na kutenda Neno la Mungu.

Hatua ya kwanza ya muhimu kuelekea kwa afya kamili na mafanikio ni kufika katika ufunuo wa kuumbwa upya. Ufunuo huu utamuweka huru mwamini kutokana na mawazo ya lawama, hukumu, na kutokuwa wa maana, ili

yeye aweze kupokea faida ya kuumbwa upya, na kuanza kutembea katika mafanikio na afya kamili.

➢ *Imefafanuliwa*

Mtoto wa Mungu "aliyefanikiwa" kwa kweli ameelezwa katika sehemu ya kwanza ya Zaburi.

Zaburi 1:1-3 Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu, wala hafuati njia ya wenye dhambi au kukaa katika baraza la wenye mizaha. Lakini huifurahia sheria ya BWANA, nayo huitafakari mchana na usiku. Mtu huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda yake kwa majira na majani yake hayanyauki. Kila afanyalo hufanikiwa.

Mtu aliyefanikiwa kwa kweli ni yule:

- ➢ *anatembea katika imani na utiifu kwa ufunuo wa Neno la Mungu*
- ➢ *anatembea katika upendo na anao ustadi katika ushirika wa karibu na Mungu na pia waamini wenza*
- ➢ *anao ustadi wa amani ya Mungu na kutosheka katika yote anayotenda*
- ➢ *anaendelea katika huduma kwa Bwana na kwa maitaji ya wengine*
- ➢ *maitaji yake ya kifedha yamejibiwa ili awe "ameandaliwa bora kwa kazi nzur"*
- ➢ *anaweza kutoa kwa ukarimu kwa Bwana na kwa maitaji ya wengine*

Mafanikio ya Kifedha

Kinyeme na vile tumefundishwa, pesa si uovu. Ni kupenda fedha ndio mwanzo wa uovu.

Fedha ni muhimu sana katika kutimiza Agizo Kuu. Ni lazima tutambue jinsi ya kupokea mafanikio ya Mungu ya kifendha ili tuwafikie waliopotea hapa duniani na injili ya Yesu Kristo.

Yohana alituonya kuwa ni sharti tuwe macho tusipende vitu vya hapa duniani. Tuendelee kuwa waangalifu dhidi ya uwongo katika utajiri, au kiburi katika maisha ambacho huleta tamaa juu ya vitu, au heshima ya wanadamu.

Mungu alisema tukitafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake, atatubariki na vitu.

Mathayo 6:33 Lakini utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake na haya yote mtaongezewa.

Mtu wa aliyeumbwa upya alikuwa na ufunuo wa haki, atapanua ufalme wa Mungu na haki yake Mungu juu ya

maitaji yake mwenyewe. Atamtafuta Mungu na haki Yake, na Mungu atampa "vitu hivi vyote."

➢ *Kumtolea Mungu*

Mungu hatafuti mahali pa kuhifadhi baraka Zake za kifedha. Badala yake, anatafuta mito, wale ambao ni watoaji katika ufalme Wake.

Yesu alisema,
Luka 6:38 "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa . Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa."

Tunapojitolea katika imani na utiifu kwa Mungu, Yeye ataizidisha kwetu ili tuendelee kuitoa Kwake.

Mafanikio ni mojawapo ya ahadi zilizoahidiwa kwa kiumbe kipya. Mungu ameweka agano la baraka za kifedha kwa watu Wake wanaomtii.

AFYA NA UPONYAJI

Faida nyingine ya kuumbwa upya ni mapato ya Mungu ya uponyaji ya mwili wake.

Ufunuo wa haki ya kuumbwa upya utawaweka huru baadhi ya wale waliofungwa na hisia za lawama, hukumu, na kutokuwa wa maana, ili waweze kupokea kwa ujasiri uponyaji wao kutoka kwa Mungu.

Katika kazi ya ukombozi ya Yesu kwa niaba yetu, Yeye alitoa kwa ajili ya wokovu wetu milele, na pia alitoa uponyaji kwa ajili ya mili yetu.

Kuponywa kwa Mapigo Yake

Katika unabii mkuu wa Isaya kuhusu kuja kwa Masiha, alinena kwa uwazi juu ya uponyaji wetu.

Isaya 53:5 Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona.

Petro alikubali ujumbe wa Isaya kuwa kweli alipoandika kuhusu kazi ya ukombozi ya Yesu akitumia yale maneno.

1 Petro 2:24 ... yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa.

Yehova Rafa

Punde tu baada ya wana wa Israeli walipotoka nje ya Misri, Mungu alijitokeza kama Yehova Rafa, Mungu aliye mponyaji wao.

Kutoka 15:26 Mungu akasema, "Kama mkisikiliza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wenu na kuyafanya yaliyo sawa machoni pake, kama mkiyatii maagizo yake na kuzishika amri zake zote, sitaleta juu yenu ugonjwa wo wote niliowaletea Wamisri, kwa kuwa Mimi ndimi BWANA, niwaponyaye."

Mungu kamwe habadiliki. Uponyaji ni wa leo!

Neno la Mungu huleta Uponyaji

Mfalme Suleimani anatuambia kuwa uhai na afya kwa mwili wote wa mwanadamu utoka kwa Neno la Mungu.

Mithali 4:20-22 Mwanangu, yasikilize kwa makini yale ninayokuambia, sikiliza kwa makini maneno yangu. Usiruhusu yaondoke machoni pako, yahifadhi ndani ya moyo wako, kwa sababu ni uzima kwa wale wanaoyapata na afya kwa mwili wote wa mwanadamu.

Ikiwa tutaligeukia Neno la Mungu na kulitafakari juu ya kile anasema juu ya kuishi katika afya, hili litakuwa jambo la kweli kuhusu afya inayoishi, litakuwa kweli maishani mwetu. Wakati akili zetu zinafanyika upya, mili yetu pia itakuwa.

Wakati ufunuo huu utaelekeza roho zetu akilini mwetu, tutaweza kunena kwa ujasiri Neno la Mungu kwa imani, na uponyaji na afya itakuwa ya kweli.

Kumbuka: Ili kupata mafunzo ya ndani kabisa juu ya uponyaji, soma *God's Provision For Healing* nao A.L. and Joyce Gill.

NGUVU YA MUNGU

Faida nyingine kuu ya kuumbwa upya ni uwezo wa kuachilia nguvu za Roho Mtakatifu kutoka ndani yetu.

Pingamizi Za Kinyume

Waamini wengi waliojazwa Roho Mtakatifu wameshindwa kuachilia nguvu za Mungu ambazo ziko ndani yao kwa sababu wameshikwa na mawazo ya kinyume na sura zao.

Wengi, wasio na ufunuo wa haki yake Mungu inayopatikana katika kuumbwa upta, wamezuiliwa kwa kukubali dhambi maishani mwao. Wamekuwa na hisia ya dhambi badala ya hisia ya haki. Wao wamejiona kama wenye dhambi, na kamwe hawajaweza kupata ushindi maishani mwao. Wameruhusu Roho Mtakatifu kuhuzunika, au kuzimwa maishani mwao.

Paulo aliandika,
Waefeso 4:30,31 Wala msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa huyo mlitiwa muhuri kwa ajili ya siku ya ukombozi. Ondoeni kabisa uchungu, ghadhabu, hasira, makelele na masingizio pamoja na kila aina ya uovu.

Mtu aliye macho juu ya dhambi ataendelea kutenda dhambi, na kwa sababu hii, atamhuzunisha Roho Mtakatifu na kuishi maisha yasiyo na nguvu na yenye kushindwa.

Ufunuo wa Haki

Waamini wenye ufunuo wa kuumbwa upya, watajiona kuwa wenye haki. Watajiona kama walivyoumbwa kuwa. Watajiona wakitenda kazi ya Yesu. Watajiona kuwa wenye haki, wakiwa na ushirika na Mungu, na kutumiwa Naye katika kuwahudumia wengine.

Watajiona wenyewe wakihudumu na upako wake Mungu unaoonekana maishani mwao. Kama vile Yesu alisema, mito ya maji ya uhai itatiririka bila pingamizi maishani mwao na katika huduma.

Yesu alisema,
Yohana 7:38 "Ye yote aniaminiye Mimi, kama maandiko yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake."

Nguvu ya Kushuhudia

Yesu alisema kuwa kusudi la nguvu, inayokuja baada ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni kutufanya tuwe mashahidi kamili wa Yesu Kristo.

Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na Samaria, hadi miisho ya dunia."

➢ *Ishara na Miujiza*

Mpango wa Mungu wa kuwafikia waliopotea ni miujiza ya uinjilisti. Ishara, maajabu, na miujiza kila wakati itakubaliana na Neno la Injili wakati tunashiriki au kulihumiri.

Maneno ya mwisho ya Yesu kwa waamini Wake kabla ya kuondoka hapa duniani kulingana na kitabu cha Mariko yalikuwa,

Marko 16:15-20 Akawaambia, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Ye yote aaminiye na kubatizwa ataokoka. Lakini ye yote asiyeamini atahukumiwa.

"Nazo ishara hizi zitafuatana na wale waaminio: Kwa Jina Langu watatoa pepo wachafu, watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka kwa mikono yao na hata wakinywa kitu cho chote cha kuua, hakitawadhuru kamwe, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapona."

Baada ya Bwana Yesu kusema nao, alichukuliwa juu mbinguni na kuketi mkono wa kuume wa Mungu.

Marko 16:20 Kisha wanafunzi Wake wakatoka, wakahubiri kila mahali, naye Bwana akatenda kazi pamoja nao na kulithibitisha neno Lake kwa ishara zilizofuatana nalo. Amen.

Kupitia kwa ufunuo wa kuumbwa upya, waamini wataweza kushuhudia kwa ujasiri kwa Yesu Kristo katika nguvu za Roho Mtakatifu.

➢ *Huru Kutokana na Hofu*

Wao hawatazuiliwa tena na hofu ya mwanadamu.

Watasema kwa ujasiri,
2 Timotheo 1:7,8a Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi. Kwa hiyo usione haya kushuhudia kuhusu Bwana Wetu ...

Waamini walio na ufunuo wa kuumbwa upya hatakuwa na hofu na bila haya ya kushuhudia kwa Yesu.

Wataweza kusema kwa ujasiri,
Wafilipi 4:13 Naweza kuyafanya mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu.

➢ *Nguvu Isiyozuiliwa*

Mwamini aliye na ufunuo wa kuumbwa upya atairuhusu nguvu ya Mungu isiyozuiliwa ionekane katika ishara, maajabu, na miujiza ya uponyaji.

Lawama na hukumu kamwe haitamzuia katika kuzikemea pepo au kuwekelea mikono yake juu ya wagonjwa na kuziachilia nguvu za Mungu katika maisha yao.

Mtu aliye na ufunuo wa kuumbwa upya atapata faida ya ushirika na Mungu: furaha, uponyaji na afya, mafanikio, na nguvu isiyozuiliwa ya Mungu. Faida hizi si kwa ajili ya kumfurahisha mwamini pekee. Ni sharti zitiririke nje kwa waliopotea na ulimwengu unaoangamia.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza jinsi hisia ya lawama, hukumu, na kutokuwa na maana kunaweza kuzuia ushirika katika ya mwamini na Mungu.

2. Ni kwa njia gani ufunuo wa kuumwa upya na haki unaweza kumweka huru mtu ili aweze kupokea uponyaji wake kutoka kwa Mungu?

3. Ni kwa njia gani ufunuo wa kuumbwa upya na haki unaweza kumweka huru ili awe na ujasiri na kushuhudia Yesu?

Wanaoshiriki katika Hali ya Kiungu

HALI YA MUNGU

Tunampokea Yesu binafsi kama mwokozi wetu, tunafanyika kiumbe kipya. Tunapokea hali mpya kabisa. Ni hali ya Mungu Mwenyewe. Je, ni jambo la kufurahisha kukundua kuwa sisi tunashiriki katika hali Yake Mungu.

2 Petro 1:4a Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi Zake kuu na za thamani kupitia hayo mpate kuokoka na upotovu ulioko duniani .....

Je hali ya Mungu ni ipi?

Kuna sehemu ya hali ya kiungu, sifa zake Mungu, ambazo zimehifadhiwa kwa Mungu pekee. Nazo ni:

- ➢ *Milele – bila mwanzo au mwisho*
- ➢ *Asiyebadilika – kamwe habadiliki*
- ➢ *Mwenye nguvu – nguvu zote*
- ➢ *Anapatikana kote – yupo kila mahali*

Imewekwa kwetu

Lakini, kuna hali fulani za Mungu ambazo zimewekwa kwetu wakati wa wokovu. Hizo hufanyika sehemu ya muhimu sana ya kuumbwa upya ndani yetu. Sisi tumepewa:

- ➢ *Haki*
- ➢ *Utakatifu*
- ➢ *Upendo*
- ➢ *Wema, Neema, na rehema*

Sehemu hizi za hali yake Mungu zimewekwa ndani ya roho wetu mpya wakati wa wokovu.

Imedhihirishwa na Ahadi Zake

Petro aliandika kuwa kwa nguvu za Mungu tumepewa vitu vyote mbavyo ni muhimu maishani na katika mambo ya Mungu. Tunafanyika washiriki katika hali ya kiungu kwa ufunuo wa Neno la Mungu. Haya yametolewa kwetu na ahadi zile kuu na zilizo bora.

2 Petro 1:2-4 Neema na amani iwe kwenu kwa wingi katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Uwezo Wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima wa uchaji wa Mungu, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu Wake wa wema Wake mwenyewe. Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi Zake kuu na za thamani kupitia mambo haya,

ili kwa kupitia hayo mpate kuokoka na upotovu ulioko duniani kwa sababu ya tamaa mbaya.

Kufanyika Washiriki

Inawezekana kupata hali yake Mungu ndani ya roho zetu bila kufanyika mshiriki katika hali Yake katika ustadi wetu.

Mtume Paulo aliandika,
Wafilipi 2:12,13 Kwa hiyo, wapenzi wangu, kama vile ambavyo mmekuwa mkitii sikuzote, si tu wakati nikiwa pamoja nanyi, bali sasa zaidi sana nisipokuwapo. Utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka, kwa maana Mungu ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi Lake jema.

Wakati wa wokovu, tunapokea sifa hizi za Mungu ndani ya roho zetu, lakini ni kupitia muda ndipo zinafanya kazi na kuwa sehemu ya akili na mili yetu. Waamini wote wamefanyika washiriki katika hali Yake ya kiungu ndani ya roho zao. Lakini, ni kupitia tu ufunuo wa kuumbwa upya ndipo tunaweza kuwa washiriki katika hali Yake ya kiungu katika nafsi na mili yetu.

Waamini wanaweza kuwa washiriki na kufurahia kile amabcho tayari ni chao kwa ufunuo wa kweli ambao huonyesha tayari wamepokea hali ya kiungu ya Mungu.

Ni wakati tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, na kwa imani kudai ahadi za Neno Lake, ndipo tunaweza kuwa washiriki katika hali Yake Mungu katika nafsi na mili yetu.

Wakati roho zetu mpya zimepokea hali yake Mungu, katika somo hili tutajifunza jinsi ya kuwa washiriki katika hali Yake katika sehemu ya nafsi na mili yetu.

KUFANYIKA KAMA YEYE

Tumetengwa na Kristo ili tubadilishwe katika sura Yake.

Warumi 8:29a Maana wale Mungu aliowajua tangu mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate kufanana na mfano wa Mwanawe ....

Roho wa kuumbwa upya imeumbwa katika mfano na sura ya Mungu, na Wakristo wako katika mpango wa kubadilishwa kwa sura katika sehemu ya mili na nafsi zao.

Mbinu Inayobadilisha

Mtume Paulo aliandika kwa Warumi,
Warumi 12:1,2 Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana. Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha

ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni Pake na ukamilifu.

Kama viumbe wapya, basi hatuwezi kubadilishwa na ulimwengu huu. Ni sharti tuishi katika mbinu ya kubadilishwa wakati tunabadilishwa kwa sura ya Mwana wa Mungu.

➢ *Kutoa Mili Yetu*

Tunaanza mbinu ya kubadilishwa kwa kukata shauri ya mili yetu kwa Mungu kabisa. Mili yetu ni hekalu la rRoho Mtakatifu na inatupasa kuitoa kama "dhabihu inayoishi kwa Mungu."

Ili kufanyika mshiriki katika hali ya kiungu ambayo tayari tunayo katika Yesu, ni lazima tuyatoe maisha yetu kwa uongozi wa Yesu Kristo kila siku.

➢ *Kuyafanya Upya Mawazo Yetu*

Hata wakati mili yetu hubadilishwa, nafsi zetu ni lazima zibadilishwe kwa mbinu inayoendelea iitwayo kuyafanya upya mawazo.

Mbinu hii ibadilishayo hufanyika wakati tunaendelea kusoma, kusikia, kutafakari juu ya, kuamini, na kulitenda Neno la Mungu. Ni kazi ya ajabu ya Roho Mtakatifu.

Kwa mbinu hii ya ajabu, mili na nafsi zetu hushiriki katika hali ya kiungu.

Mungu Kufanya Kazi ndani Yetu

Paulo aliomba, pamoja na hali ya mama anapojifungua mimba, kwa waamini Wagalatia kuwa Kristo atafanyika ndani yao.

Wagalatia 4:19 Watoto wangu wapendwa, ambao kwa mara nyingine ninawaonea utungu, ninatamani kwamba Kristo aumbike ndani yenu...

Aliwaambia waamini Wafilipi kuwa Mungu alikuwa akitenda kazi ndani yao.

Wafilipi 2:13 Kwa maana Mungu ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi Lake jema.

Mungu anaendelea kutenda kazi katika maisha ya viumbe Wake wapya, hadi wabadilishwe na kuwa sura ya Mwanawe.

Kadri tunapomuruhusu kutenda kazi Yake ndani yetu, ndipo tunakuwa kama Kristo.

> **Kumbukumbu Maalum:** Tumejifunza tayari juu ya haki yake Mungu na jinsi ilivyowekwa kwetu. Haki ni mojawapo ya sifa zake Mungu. Katika somo hili, tutachukua kuwa unaelewa juu ya haki

Yake na jinsi imewekwa kwetu wakati wa wokovu na kuendelea kwa sifa zake Mungu zingine.

KUSHIRIKI KATIKA UTAKATIFU WAKE

Mungu ni Mtakatifu

Utakatifu wa Mungu ni wa ajabu, wenye usafi kabisa na ukamilifu usioweza kuelezwa. Huleta kutengwa kabisa kutokana na dhambi na uchafu.

Mungu ni mtakatifu kabisa katika hali yake na katika njia zake zote. Malaika wana tangaza utakatifu wake.

Isaya 6:3 Nao walikuwa akiitana kila mmoja na mwenzake: "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni BWANA Mwenye Nguvu, Dunia yote imejaa utukufu wake."

Amri ya Kuwa Watakatifu

Roho wetu mpya wa kuumbwa upya ni mtakatifu kama vile Mungu mwenyewe ni mtakatifu.

Mtume Paulo aliandika,
Waefeso 1:4 Kwa maana alituchagua katika Yeye kabla ya kuumbwa ulimwengu ili tuwe watakatifu na bila lawama mbele Zake.

Kumbuka, mili yetu na nafsi zetu ziko katika mbinu ya kubadilishwa kwa mfano wa Kristo. Ni lazima tuchague na kuwa watakatifu katika maisha yetu ya kila siku. Huu ni utakatifu katika ustadi wetu.

Mambo Ya Walawi 19:2b 'Iweni watakatifu kwa sababu Mimi ni Mtakatifu, BWANA wenu niliye mtakatifu.'

Ni lazima tuchague kuwa watakatifu katika mienendo yetu. Ni lazima tuyaweke maisha yetu kama vyombo vitakatifu kwa Mungu. Ni lazima tujiangalie kama wafu kwa dhambi na hai kwa Yesu.

Huu ni ustadi wa kutakaswa, mbinu ya kutengwa na mipango ya hapa duniani na kwa Yesu Kristo Mwenyewe. Ni kufanyika kama Yesu katika maisha na mienendo yetu kila siku.

1 Petro 1:15,16 Bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote, kwa maana imeandikwa: "Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa Mimi ni mtakatifu."

Tumeamuriwa kuwa watakatifu na tunaweza kufanya haya kwa kushiriki katika hali ya utakatifu Wake Mungu.

KUAHIRIKI KATIKA UPENDO WAKE

Mungu ni Upendo

Mungu katika hale Yake ni Upendo. Yeye ni chanzo cha upendo wote.

1 Yohana 4:16 Hivyo nasi twajua na kuutumainia upendo wa Mungu alio nao kwa ajili yetu. Mungu ni Upendo. Kila akaaye katika upendo hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake.

Njia kuu ambayo Mungu alionyesha upendo Wake kwa mwanadamu ilikuwa kupitia kwa zawadi ya Mwanawe wa dhamana.

Warumi 5:8 Lakini Mungu anaudhihirisha upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.

Yohana 3:16 "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Aina Nne za Upendo

Kwa sababu katika dunia ya kisasa neno "upendo" mara nyingi huelezwa vibaya, itakuwa bora kufahamu maneno manne yanayotumika katika lugha ya Kigiriki.

➢ *Erosi*

"Erosi" ni pendo kati ya mke na mume. Haipo katika agano Jipya. Inagusia upendo kati ya mke na mume kama inavyoelezwa katika Wimbo Ulio Bora. Imepingwa na Mungu nje ya mapenzi kati ya mume na mke.

➢ *Upendo wa kijamii*

"Storge" ni upendo wa kijamii. Inatokana na maelezo ya kuvutiwa na. katika ya watu wa jamii moja

Warumi 12:10 Pendaneni ninyi kwa ninyi kwa upendo wa kidugu. Waheshimuni na kuwatanguliza wengine.

Storge is the affection that family members show for one another both within natural families and within the family of God.

➢ *Marafiki*

Huu ni upendo wa ndani sana kati ya mtu mmoja na mwingi. Pia unagusia kubusu. Upendo mkuu wa joto na wa kuvutia.

Yohana 5:20a Baba ampenda Mwana na kumwonyesha yale ambayo Yeye Baba mwenyewe anayafanya.

Upendo wa marafiki (Philia) ulitumika kueleza upendo wa uhusiano kati ya Yesu na Lazaro.

Yohana 11:3 Hivyo hawa dada wawili walituma ujumbe kwa Yesu kumwambia, "Bwana, yule umpendaye ni mgonjwa."

Pia kuna neno "Philos," mbalo ni mtu fulani aliye mpendwa sana kwa hisia za upendo kwa mtu mweingine.

Yohana 15:13 Hakuna mtu mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.

This is the intimate type of love that a husband and wife have for one another (philandros) .

In addition to the close and warm love relationship that Jesus had for Lazarus, it is also seen in the love relationship between David and Jonathan. It is a special love limited to a few very close relationships between two people.

➢ *Upendo wa Mungu*

Upendo (agape) huu wa Mungu ambao unatolewa kama tunda la Roho Mtakatifu katika maisha ya mwamini.

Wagalatia 5:22,23 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.

Upendo wa agape ni wa ajabu, ni upendo wa Mungu unaoletwa na Roho Mtakatifu mioyoni mwetu, katika maisha yetu na vitendo vyetu kwa wengine.

Kwa sababu upendo huu unatoka kwa Mungu, ni upendo ambao ulimwengu unaweza kupata tu katika kuumbwa upya – kupitia kwetu. Ni upendo kwa jirani zetu, marafiki wetu, na hata kama ni la ajabu kwa ulimwengu, na kwa adui wetu.

1 Yohana 3:16 Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu, kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai Wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu.

Kwa Ufupi

Erosi imepimwa na sheria za Mungu kwa mke au mume tu.

Storge imewekwa kwa jamii wa kawaida au wa kiroho.

Philia umewekwa kwa ajili ya mke au mume na pia rafiki wa karibu.

Lakini, katika kuumbwa upya, upendo mkuu wa Mungu unaonyeshwa kwa wote, hata kwa adui wetu.

Upendo wa Mungu katika Kutenda

➢ *Pendana mmoja kwa mwingine*

Kwa kujazwa hali Yake Mungu ndani yetu, na kama tunda la Roho, viumbe wapya wanakuwa na upendo mmoja kwa mwingine.

Warumi 13:8 Msidaiwe kitu na mtu ye yote, isipokuwa kupendana, kwa maana yeye ampendaye mwenzake, ameitimiza sheria.

Yesu alisema,
Yohana 13:34,35 "Amri mpya nawapa: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane. Kama mkipendana ninyi kwa ninyi, kwa njia hii, watu wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu."

Kitu juu ya mengine yote ambacho huwatofautisha wanafunzi wa Yesu ni upendo walio nao mmoja kwa mwingine.

➢ *Mwanafunzi wa Upendo*

Mwanafunzi ni yule aliye chini ya nidhamu ya Yesu. Yeye ni zaidi ya Mkristo. Yeye ni, ambayo kwa imani na kutii, anabadilishwa kwa hali ya upendo na sura ya Yesu. Mwanafunzi atasema pamoja na mtume Yohana,

1 Yohana 4:7 Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anamjua Mungu.

Viumbe wapya, wale ambao ni washiriki katika hali ya kiungu, watatembea katika upendo (agape) wa Mungu.

Warumi 5:5b ... Mungu amekwisha kumimina pendo Lake mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye ametupatia .

➢ *Upendo umeamuriwa na Sheria*

Sheria ya Musa iliamuru kuwa tupende mmoja kwa mwingine.

Mambo Ya Walawi 19:18 Usijilipizie kisasi wala kuwa na kinyongo dhidi ya mmoja wa jamaa yako, lakini mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe ...

Waume kwa wake wasiobadilishwa hawakuweza kutimiza sheria. Wao wenyewe hawangependa jirani wao kama wenyewe.

Yesu alitoa amri mpya ya upendo kwa viumbe Wake wapya.

Warumi 13:9 Kwa kuwa amri hizi zisemazo, 'Usizini," "usiue," "usiibe," "usitamani," na amri nyingine zote, zinajumlishwa katika amri hii moja: "Mpende jirani yako kama nafsi yako."

➢ *Sheria Kutimizwa na Upendo*

Upendo ni timizo la sheria.

Warumi 13:10 Upendo haumfanyii jirani jambo baya. Kwa hiyo upendo ndio utimilifu wa sheria.

Paulo aliwaandikia Waglatia,
Wagalatia 5:14 Kwa maana sheria yote hukamilika katika amri moja: "Mpende jirani yako kama nafsi yako."

Kupenda Adui Wetu

Mungu, katika hali Yake ya upendo mkuu, alitupenda tulipokuwa adui wake. Kama viumbe wapya, nasi pia tuko na hali ya upendo wa Mungu. Nasi pia ni lazima tuwapende waliopotea hapa duniani na kushiriki nao upendo mkuu Wake Mungu na pia huruma zake.

Kwa sababu sisi tu viumbe wapya, tunashiriki katika hali ya upendo wake Mungu. Kwa Roho Mtakatifu, tunaweza na ni lazima tuwapende hata wale ambao ni adui wetu.

Mathayo 5:44 Lakini mimi ninawaambia: Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi.

Yesu hangetuamuru kutenda jambo ambalo haliwezekani kwetu kutenda. Tunaweza na ni lazima tuwapende adui wetu kwa upendo wa mungu.

➢ *Kuonyesha Upendo mkuu*

Yesu aliwaagiza wafuasi Wake jinsi ya kuonyesha upendo mkuu kwa wengine – hata pia kwa adui zao.

Luka 6:27-30 "Lakini nawaambia wale wanaonisikia, wapendeni adui zenu. Watendee mema wanaowachukia. Wabarikini wale wanaowalaani, waombeeni wale wanao watendea mabaya. Kama mtu akikupiga shavu moja mgeuzie na la pili. Mtu akikunyang'anya koti lako , usimzuie kuchukua joho pia. Mpe kila akuombaye na kama mtu akichukua mali yako usitake akurudishie.

Mtume Paulo aliandika,
Warumi 12:20 Badala yake: "adui yako akiwa na njaa, mpe chakula, akiwa na kiu, mnyweshe. Maana ukifanya hivyo, utampalia makaa ya moto yanayowaka kichwani pake."

➢ *Mfano wa Upendo Mkuu*

Stefano alikuwa mfano mkubwa wa upendo wa ajabu katika vitendo alipokuwa akipigwa mawe na adui zake.

Matendo 7:59,60 Walipokuwa wakimpiga mawe, Stefano aliomba, "Bwana Yesu, pokea roho yangu" kisha akapiga magoti, akalia kwa sauti kubwa akasema, Bwana usiwahesabie dhambi hii." Baada ya kusema haya akalala.

Mtu anayeishi kwa hisia zake kamwe hataona ustadi wa upendo huu. Inaweza tu kuonekana na kuonyeshwa na wale ambao wamepata ufunuo wa Mungu ndani yao.

➢ *Kuchagua Kupenda*

Kwa sababu kupenda adui zetu ni kinyume na hisia zetu na nafsi zetu za kawaida, sisi tulio na ufunuo wa upendo Wake Mungu ni lazima tuchague kupenda kama vile Mungu apendavyo.

1 Petro 1:22 Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni.

Wanaompenda Mungu

Wale ambao wamepata ufunuo wa kuumbwa upya na kuwa wako ndani ya Kristo, na wamefanyika washiriki katika hali Yake ya kiungu, basi, juu ya yote, watakuwa wapenzi wa Mungu.

Watatenda yote wakimfurahisha Mungu kwa kutii Neno Lake. Watakuwa waabudu wa Mungu.

Viumbe wapya wataendelea kumsifu Mungu kwa baraka Zake zote za jabu. Watamsifu Mungu kwa jinsi alivyo. Sifa zake Mungu zitaendelea kuwa juu ya vinywa vyao.

Viumbe wapya watakuwa na upendo wa ndani na wa karibu zana na Mungu.

Zaburi 42:1,2 Kama vile paa aoneavyo shauku vijito vya maji, ndivyo nafsi yangu ikuoneavyo shauku, Ee Mungu. Nafsi yangu inamwonea Mungu kiu, Mungu aliye hai. Ni lini nitaweza kwenda kukutana na Mungu?

Viumbe wapya watatembea katika upendo mkuu wa Kristo kwa waamini wenza, adui zake, na kwa Mungu Mwenyewe.

KUSHIRIKI KATIKA WEMA NA REHEMA ZAKE

Mungu Ni Mwema

Mungu katika hali Yake ni mwema.

Zaburi 52:1b Wema wake Mungu unavumilia kuendelea.

Wema Wake Mungu ni moja ya ukamilifu kabisa. Wema Wake unaonyeshwa kwa viumbe Wake wote kwa rehema na neema Zake.

Rehema na Neema Zake Mungu

Rehema Zake Mungu kwa wanadamu wenye dhambi zilionyeshwa kwa wazi na kamili wakati alimtoa Mwanawe ili afe kwa niaba yetu. Mojawapo ya maelezo ya rehema ni:

➢ *kuvvumilia kutokutoa adhabu kwa anayevunja sheria*

Rehema zake Mungu ni wema wake Mungu uonekanao katika mahitaji yetu. Mungu amejawa na rehema!

Waefeso 2:4 Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi , ambaye ni mwingi wa rehema...

Mungu anaitwa Baba wa rehema.

2 Wakorintho 1:3 Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa huruma na Mungu wa faraja yote.

➢ *Kuokolewa kwa Neema*

Maelezo ya neema ni:

➢ *Ni upendo wa Mungu kwa kuwajali wanadamu.*

Ni njia nyingine ya kuonyesha upendo Wake mkuu.

Waefeso 2:5,8 Hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, (yaani, mmeokolewa kwa neema)...

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu.

➢ *Kiti cha Enzi cha Neema*

Sasa, kama viumbe wapya, tunaweza kuja kwa ujasiri mbele ya kiti cha enzi cha neema.

Waebrania 4:16 Basi na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

KUSHIRIKI KATIKA MSAMAHA WAKE

Mungu Anasamehe

Njia kuu ya kuonyesha neema na rehema zake Mungu inapatikana katika msamaha Wake. Msamaha Wake umeelekezwa kwa kila wenye dhambi wanapompokea Yesu kama mwokozi wao – kwa niaba yao binafsi.

Waefeso 1:7 Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake.

Msamaha Wake umeelekezwa kwa waamini wanapokiri dhambi zao.

1 Yohana 1:9 Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote.

Katika Agano Jipya, msamaha ina maana:

➢ *kupeleka mbali na*

➢ *kulipa deni au dhambi kwa kuifutiliwa mbali kabisa*

➢ *kuweka upendo au kujali, kwa kuziachilia kutokana na, kuachilia au kupuuza dhambi au kuruka mipaka.*

Mungu anasamehe na kusahau! Msamaha Wake unaegemea kazi ya ukombozi ya Yesu, ambayo mbali na kulipa adhabu ya dhambi zetu, pia alizibeba dhambi zetu hadi chini ya ardhi, zisije zikakumbukwa au kuhesabiwa dhidi yetu tena.

Waebrania 8:12 "Kwa kuwa nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena!"

Ni Lazima Tusamehe

Kama washiriki katika hali Yake Mungu, sisi kama viumbe wapya, tutatembea katika rehema na neema za Mungu kwa wengine. Tutasamehe kama vile Mungu husamehe.

Waefeso 4:32 Iweni wafadhili na wenye kuhurumiana ninyi kwa ninyi, mkisameheana, kama vile naye Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.

➢ *Endelea Kusamehe*

Hata kama mtu ataendelea kutenda dhambi dhidi yetu, ni lazima tuendelee kusamehe.

Mathayo 18:21,19 Ndipo Petro akamjia Yesu na kumwuliza, "Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Je, hata mara saba?"

Yesu akamjibu, "Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini."

Kama viumbe wapya, tunaweza kusamehe kwa sababu tu washiriki katika asili Yake Mungu. Tunaweza na ni lazima tusamehe kwa sababu Yesu alisamehe.

➢ *Chagua Kusamehe*

Msamaha ni chaguo. Ni tendo la kumtii Mungu. Tusisubiri kusamehe hadi tujihisi hivyo. Ni lazima tumtii Mungu na kufanya uamuzi wa kusamehe kwa sababu Mungu katika rehema na neema Zake ametusamehe.

Yesu alitundikwa msalabani mbele ya adui Zake. Walimpiga, kumtemea, kumdhihaki, kusema uwongo juu Yake, kuweka taji la miba kichwani Mwake, na hata kumsulubisha. Na bado, hata alipokuwa msalabani, aliwasamehe.

Luka 23:34a Yesu akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!"

Yesu ni mfano wetu. Kwa sababu alisamehe na yu ndani yetu, nasi pia tunaweza kusamehe.

Samehe Ili Usamehewe

Huyu Yesu alisema,
Marko 11:25 Nanyi kila msimamapo kusali, sameheni, mkiwa na neno na mtu ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.

Kama viumbe wapya katika Yesu Kristo na tukiwa na asili ya upendo Wake Mungu, rehema, na neema, nasi pia tunaweza kuwasamehe wote waliotenda dhambi dhidi yetu au dhidi ya wapendwa wetu. Tumeamuriwa kusamehe ili tusamehewe.

Kumalizia

Kama viumbe wapya, tunao uhai na asili ya Mungu ndani ya roho zetu. Nafsi na mili yetu hushiriki katika asili ya Mungu kama vile tunabadilishwa katika sura ya Mwanawe.

Sehemu yetu ni kuleta mili yetu kama dhabihu inayoishi kwa Mungu, ili kutumia muda katika Neno la Mungu, na kuwasikiliza walimu Wake ili nafsi zetu zibadilishwe kwa ufunuo wa Neno la Mungu.

Ni sharti tuwe washiriki katika haki Yake Mungu, upendo, na wema Wake. Tunashiriki katika rehema na neema Zake hadi sisi, kama Yeye, tuwe wanaowasamehe wengine.

Kama viumbe wapya, roho zetu hupokea asili Yake Mungu ndani yetu. Nafsi zetu na mili yetu hushiriki katika sili ya kiungu kwa kubadilishwa kwa nguvu ya Neno la Mungu maishani mwetu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza njia ambayo tunaweza kuwa washiriki katika asili Yake Mungu.

2. unapofanyika mshiriki katika asili Yake Mungu, ni mabadiliko gani unayotarajia katika mienendo yako, uhusiano, na vitendo kwa wengine?

3. Ni kwa nini ni muhimu kuwasamehe wote waliotenda dhambi dhidi yetu?

Neno la Mungu na Kuumbwa Upya

NENO LA MUNGU

Utangulizi

Ufunuo wa kuumbwa upya unapatikana katika Neno la Mungu. Neno Lake linaweka wazi Yesu na nafasi yetu ndani Yake. Mabadiliko ya roho na mili yetu inawezekana tu kwa kufanya upya mawazo yetu katika nguvu ya Neno la Mungu.

Mmbinu hii ya mabadiliko huja tu tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, na kujiona kama vile Mungu anavyotuona. Tunapoanza kutangaza Neno la Mungu mara kwa mara kwetu wenyewe, fikira zetu zitaanza kuwa kama mfano wa Mungu. Imani yetu, itaachiliwa na tutaanza kujiona tukiwa, kutenda, na kuwa na yote Mungu anasema kutuhusu kama viumbe wapya katika Mwana Wake.

Yesu, Neno Linaloishi

Yesu na Neno ni moja. Kulijua Neno Lake ni kumjua Yeye.

Yohana 1:1,14 Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu... Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.

Yesu ni Neno la Mungu, na Neno ni ufunuo wa Yesu. Yesu anaonekana katika kila kitabu cha Biblia. Kutafakari juu ya Neno ni kama kuwa na yesu.

Wakati Yesu anaonekana kwetu, tutakuwa kama Yeye!

1 Yohana 3:2 Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo.

Ni kwa kulielewa Neno la Mungu ndipo tunagundua ufunuo ubadilishao maisha wa kuumbwa upya.

Limetolewa kwa Kuvuviwa

Biblia imeanzishwa na Mungu. Sio tu mkusanyiko wa vitabu vilivyoandikwa na watu tofauti katika nyakati nyingi, limetiwa pumzi na kuvuviwa na Mungu.

2 Timotheo 3:16,17 Kila andiko, lililovuviwa na Mungu lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kutenda kila kazi njema.

Maneno ya asili ya tafsiri “kuvuviwa na mungu” maana yake ni “kutiwa pumzi na Mungu.”

Mungu alipopumua pumzi Yake kwa Adamu, Adamu alifanyika roho anayeishi. Adamu alikuwa na uhai ule wa Mungu mwenyewe ndani yake.

Kwa njia hiyo hiyo, Mungu alipumua pumzi Yake kwa Neno Lake. Neno la Mungu halina makosa na limekamilika kwa sababu limevuviwa kwa Roho Mtakatifu.

2 Petro 1:20,21 Awali ya yote, yawapasa mjue kwamba hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa kama apendavyo mtu mwenyewe. Kwa maana unabii haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Linaishi na Lenye Uwezo

Neno la Mungu li hai na uhai wa Mungu. Neno la Mungu ni kuu katika kuyabadilisha maisha yetu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Waebrania 4:12 Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Lina Uhai wa Mungu

Uhai wa Mungu, ambao ulivuviwa katika Neno la Mungu, bado u hai katika upewo wa Mungu na uwezo kama vile ile siku lilivyoandikwa. Uhai wa Mungu, ulio katika Neno Lake, unaendelea katika maisha ya wale wanaotumia muda katika uhai huo.

Mithali 4:20-22 Mwanangu, yasikilize kwa makini yale ninayokuambia, sikiliza kwa makini maneno yangu. Usiruhusu yaondoke machoni pako, yahifadhi ndani ya moyo wako, kwa sababu ni uzima kwa wale wanaoyapata na afya kwa mwili wote wa mwanadamu.

Kuishi kwa Neno

Kiumbe kipya huishi kwa Neno la Mungu.

Mathayo 4:4 Lakini Yesu akajibu, “Imeandikwa, ‘Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

Kuumbwa upya ni kuishi katika Neno, kulitegemea usiku na mchana.

Yoshua 1:8 Usiache kitabu hiki cha Torati kiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, ili upate kuwa mwangalifu kufanya kila kitu sawasawa na yote yaliyoandikwa ndani yake. Ndipo utakapoifanikisha njia yako na kisha utasitawi sana.

Neno Linalodumu

Tunaposoma, kutafakari, kuamini, kukiri, na kulitenda Neno la Mungu, litashinda kama vile lilishinda katika mji wa Efeso.

Paulo alifundisha Neno la Mungu kila siku katika shule ya Tirana.

Matendo 19:10-12 Jambo hili likaendelea kwa muda wa miaka miwili, kiasi kwamba Wayahudi na Wayunani wote walioishi huko Asia wakawa wamesikia neno la Bwana.

Mungu akafanya miujiza mingi isiyo ya kawaida kwa mkono wa Paulo, kwamba leso au vitambaa vilivyokuwa vimegusa mwili wa Paulo viliwekwa juu ya wagonjwa, nao wakapona magonjwa yao na pepo wachafu wakawatoka.

Paulo alipoendelea kufundisha na kuhubiri Neno kule Efeso, mambo makubwa yaliendelea kutendeka.

Matendo 19:17-20 Habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawajaa wote, nalo jina la Bwana Yesu likaheshimiwa sana. Wengi wa wale waliokuwa wameamini wakati huu wakaja na kutubu kuhusu matendo yao maovu waziwazi. Idadi kubwa ya wale waliofanya mambo ya uganga wakaleta vitabu vyao na kuviteketeza kwa moto hadharani. Walipofanya hesabu ya thamani ya vitabu vilivyoteketezwa ilikuwa drakamu 50,000 za fedha. Hivyo neno la Bwana likaenea sana na kuwa na nguvu.

Ikiwa tutadumu katika Neno la Mungu, kulisoma na kutafakari kila siku, kuamini, kulinena, na kutenda kwa ijasiri, ufunuo wa Neno la Mungu utakua sana na kushinda maishani mwetu na miji yetu kama vile Efeso katika Asia.

UMUHIMU WA NENO MAISHANI MWETU

Hulisha Roho Zetu

Neno la Mungu huweka imani ndani ya roho zetu, na hujenga upendo wetu kwa Mungu na mmoja kwa mwingine. Neno la Mungu, kulisha roho wa kiumbe kipya, ni muhimu zaidi ya kula chakula cha kawaida ili kulisha mwili.

Ayubu 23:12 Sijaziacha amri zilizotoka midomoni mwake, bali nimeyathamani maneno ya kinywa chake kuliko chakula changu cha kila siku.

Yeremia 15:16a Maneno yako yalipokuja, niliyala, yakawa shangwe yangu na furaha ya moyo wangu.

Mathayo 4:4 Lakini Yesu akajibu, "Imeandikwa, 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Huleta Kukubalika

Mungu anatutazamia kujifunza na kufahamu Neno Lake kama vile Paulo alimwamuru Timotheo kutenda.

2 Timotheo 2:15 Jitahidi kujionyesha kwa Mungu kuwa umekubaliwa na Yeye, mtenda kazi asiye na sababu ya kuona aibu, ukilitumia kwa usahihi neno la kweli.

Hujenga Imani yetu

Imani huja kwa kulisoma na kusikia Neno la Mungu.

Warumi 10:17 Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo.

Wakati imani inakuja kwa kulisikia Neno, imani hiyo itaanza kunena, kukiri, na kutangaza Neno la Mungu kama kweli.

KUTAFAKARI JUU YA NENO LA MUNGU

Ni muhimu kuwa tutafakari juu ya Neno la Mungu, si kwa asili yetu, upunguvu wetu, kukosa uwezo, hali mbalimbali, au matatizo. Ikiwa tutaendelea kuweka mawazo yetu juu ya vitu hivi vya kinyume, mawazo yetu haiwezi kufanywa upya.

Wafilipi 4:8,9 Hatimaye, ndugu zangu, mambo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo na sifa njema, yo yote yaliyo na haki, yo yote yaliyo safi, yo yote ya kupendeza, yo yote yenye staha, ukiwako uzuri wo wote, pakiwawepo cho chote kinachostahili kusifiwa, tafakarini mambo hayo. Mambo yote mliyojifunza au kuyapokea au kuyasikia kutoka kwangu, au kuyaona kwangu, yatendeni hayo. Naye Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.

Kutafakari juu ya Neno la Mungu ni muhimu kwa kubadilishwa kwetu kwa kuyafanya mawazo yetu upya.

Zaburi 1:1-3 Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu, wala hafuati njia ya wenye dhambi au kukaa katika baraza la wenye mizaha. Lakini huifurahia sheria ya BWANA, nayo huitafakari mchana na usiku. Mtu huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda yake kwa majira na majani yake hayanyauki. Kila afanyalo hufanikiwa.

Wakati mtu aliyeumbwa upya anatafakari juu ya Neno la Mungu usiku na mchana, mabadiliko huja maishani mwake.

Mstari wa tatu hutaja matokeo yatakayokuja wakati mtu anaendelea kutafakari juu ya Neno la Mungu.

- **Ustawishaji –** Mizizi yao itapata maji ya uzima isiyokatika.

- **Kutoa Matunda –** Watazaa matunda kwa wakati unaofaa.
- **Kutegemea –** Tawi lao halitanyauka**.**
- **Mafanikio** – Chochote wafanyacho kitafanikiwa

Kwa Kuyafanya mawazo yetu Upya

Tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, basi "tunabadilishwa kwa kuyafanya upya mawazo yetu."

Warumi 12:2a Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuze kwa kufanywa upya nia zenu....

Kwa kutafakari juu ya Neno la Mungu, mabadiliko hufanyika. Nafsi zetu (fikira, hisia, na uwezo wa kuamua) hubadilishwa na kuwa kile roho zetu huwa wakati wa wokovu.

Mfalme Suleimani aliandika,
Mithali 23:7a ... Jinsi anavyofikiri moyoni mwake, ndivyo alivyo.

Tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, mabadiliko ya ajabu hufanyika. Nafsi zetu za awali hubadilishwa na kuwa kipepeo chenye urembo, na kuwa katika mfano wa Kristo Mwenyewe.

Mbinu za Kutafakari

➢ *Fwatilia kwa Makini*

Tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, tunafuatilia kwa makini maneno ambayo Mungu amenena. Tunayarejelea kila mara kwetu wenyewe.

1 Timotheo 4:15 Uwe na bidii katika mambo haya, jitolee kwa ajili ya mambo hayo kikamilifu, ili kila mtu aone kuendelea kwako.

➢ *Leta Katika Ufahamu*

Tunapoendelea kutafakari juu ya Neno la Mungu, tunaanza kuwa na picha na ufahamu kuumbwa upya. Tunaanza kujiona kama vile Mungu anavyotuona,

- *kuwa kile Anasema tuko*
- *kutenda kile Anasema tunaweza kutenda*
- *kuwa na kile anasema tunacho*

Mtume Paulo alimwandikia Timotheo kuwa alipotafakari juu ya Neno, maendeleo yake yataonekana kwa wote.

1 Timotheo 4:15 Uwe na bidii katika mambo haya, jitolee kwa ajili ya mambo hayo kikamilifu, ili kila mtu aone kuendelea kwako.

Yoshua aliandika kuwa kwanza tunaitajika kutafakari juu ya Neno mchana na usiku, na pia kutenda linavyosema, na

mwisho njia yetu itakuwa na mafanikio na tutakuwa na ushindi bora.

Yoshua 1:8 Usiache kitabu hiki cha Torati kiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, ili upate kuwa mwangalifu kufanya kila kitu sawasawa na yote yaliyoandikwa ndani yake. Ndipo utakapoifanikisha njia yako na kisha utasitawi sana.

Tunapoanza kumwona Yesu jinsi alivyo, kufahamu kuwa sisi tu viumbe wapya ndani Yake, tutaanza kujiona kama vile Yeye alivyo. Yohana aliandika kuwa tutakuwa kama Yeye. Je, ni ahadi ya ajabu iliyoje!

1 Yohana 3:2 Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo.

Tunapotafakari, tutaanza kunena kile Neno la Mungu linasema kutuhusu kila wakati hadi lifanyike kweli ndani yetu.

➢ *Kulisema kwa Upole*

Neno la Kieburania kutafakari ni "kusema kwa upole". Tunaposema kwa upole, au kutangaza Neno la Mungu kila mara kwetu wenyewe, linaachilia nguvu za Neno la Mungu katika vitendo maishani mwetu.

Isaya 59:21 "Kwa habari yangu mimi, hili ni agano langu nao," asema BWANA "Roho wangu, aliyeko juu yenu na maneno yangu ambayo nimeyaweka katika vinywa vyenu hayataondoka kinywani mwenu, wala kutoka vinywani mwenu mwa watoto wenu, wala kutoka vinywani mwa wazao wao kuanzia sasa na hata milele," asema BWANA.

➢ *Wazia Dhania*

Tunapoendelea kutafakari juu ya kweli za kuumbwa upya za Neno la Mungu, linaachilia dhamira zetu ili kufanya sura za kiungu. Tunaanza kuwaza mawazo ya Mungu na kujiona kama viumbe wapya katika macho ya Mungu.

Isaya 55:8,9 "Kwa kuwa mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu," asema BWANA. "Kama vile mbingu zilivyo juu kuliko dunia, ndivyo njia zangu zilivyo juu kuliko njia zenu na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.

➢ *Kufahamu*

Tutaanza kutafakari au kuelewa hekima na ufunuo wa Mungu.

Waefeso 1:17,18 Nazidi kumwomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awajalieni ninyi roho ya hekima na ya ufunuo, ili mpate kumjua zaidi. Ninaomba pia kwamba

macho ya mioyo yenu yatiwe nuru ili mpate kujua tumaini mliloitiwa, utajiri wa urithi wa utukufu Wake kwa watakatifu.

Neno la Mungu

Kuna maneno mawili ya muhimu katika Agano Jipya la Kigiriki ambayo hutumika kueleza Neno la Mungu.

La kwanza ni Logosi (lililoandikwa), ambalo ni Neno la Mungu lililoandikwa. La pili ni Rhema, ambalo ni Neno la Mungu linalonenwa.

➢ *Logosi*

Logosi ni jina litumikalo katika Biblia yote. Ni maneno ya jumla ya Mungu yaliyotolewa kwa watu Wake wote.

➢ *Rhema*

Rhema ni Neno la Mungu linenwalo kwangu mimi binafsi.

Rhema ni ufunuo wa ajabu ambao huja kwetu binafsi kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu tunapotafakari juu ya Neno lililoandikwa.

Wakati Neno la Rhema huja, kama nuru huingia katika roho zetu. Tunajua kuwa Mungu amenena kwetu Yeye binafsi. Ni Neno la Rhema, neno la Logosi linenalwo kwetu kwa Roho Mtakatifu, ambalo huachilia imani yetu.

NGUVU YA KUTANGAZA NENO LA MUNGU

Mtume Paulo aliandika kuwa imani huja kwa kulisikia na kwa kusikia Neno la Mungu. Tunalisikia Neno la Mungu kwa kulisoma sisi wenyewe, kulirudia sisi wenyewe, na kwa mafundisho mazuri.

Ikiwa kuna hitaji fulani maishani mwetu, tunatakiwa kupata mistari katika Neno la Mungu ambayo hujibu hitaji hilo na kisha kuyasoma huku ukiyarudia, punde hayo hufanyika kweli zaidi kwetu kuliko hali hiyo. Imani imefika.

Neno la Logosi hufanyika Neno la binafsi la Mungu au Neno la Rhema kama linavyodhihirishwa na kunenwa kwa roho zetu kwa Roho Mtakatifu. Mara tunapopokea ufunuo huo, imani huingia katika roho zetu.

Warumi 10:17 Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo.

Wakati ufahamu wetu huangaziwa na Rhema la Mungu, tutafikia ufahamu kuhusu ukweli juu yetu katika Yesu. Tutabadilishwa na kuwa viumbe wapya.

Kulitangaza Neno la Mungu

Kitendo cha kutangaza Rhema la Mungu inaitwa pia kukiri Neno la Mungu. Neno la Kigiriki ambalo tafsiri yake ni kukiri ni “homo-logeo.” Kukiri Neno la Mungu ina maana:

➢ *Kunena kitu kile kile*

➢ *Kukubaliana na*

➢ *Kukuwa katika hali kukubaliana*

Hii ndiyo ilifanyika kwa kila mmoja wetu wakati tulipokea ufunuo wa neno la Rhema la Injili. Tulipokea na kukiri kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, kuwa alikufa kwa niaba yetu, na kuwa alifufuka kutoka kwa wafu.

Warumi 10:9,10 Kwa sababu kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba "Yesu ni Bwana," na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini na hivyo kuhesabiwa haki, tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo kupata wokovu.

➢ *Ninaamini – Ninanena*

Wakati tunaamini, tunaitajika kunena, kukiri kile kimedhihirishwa kwetu. Kuna roho ya imani na inasema, ninaamini, basi ninanena!

2 Wakorintho 4:13 Imeandikwa, "Niliamini, kwa hiyo nimesema." Kwa roho yule yule wa imani pia tuliamini na hivyo tukasema.

➢ *Kuelewa Vibaya juu ya Kukiri*

Wengi wamekosea juu ya ukweli huu na wamejaribu kukiri mara kwa mara kitu ambacho wametaka. Wametafuta maandiko kwa ajili ya neno ambalo linaangazia mapendekezo yao katika kumlazimu Mungu ili awatosheleze wao wenyewe.

Ni Rhema, kile Mungu amenena na kuweka wazi Yeye binafsi kwetu, ambalo litaachilia imani yetu ili kukiri na kudai kwa ujasiri kile kilicho cha haki kwetu. Ni Rhema, ambalo sisi kama viumbe wapya, tunaweza kutangaza kwa ujasiri. Tunaponena maneno haya ya Mungu, mambo yenye nguvu huanza kutendeka.

Mungu Aliumba kwa Kunena

Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Mungu ni Muumba na aliumba kwa kunena maneno.

Waebrania 11:3 Kwa imani tunafahamu kwamba ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, vitu vyote vinavyoonekana viliumbwa kwa vitu visivyoonekana.

Tunaona nguvu ya Mungu katika uumbaji ikitenda kazi katika sehemu ya kwanza ya Mwanzo ambapo kifungu "Na Mungu akasema," imerudiwa mara nyingi.

Tunaumba kwa Kunena

Sisi, kama viumbe wapya, pia tunaumba kwa maneno tunayosema.

Mithali 18:20 Tumbo la mtu litajaa kutokana na tunda la kinywa chake, atashibishwa mavuno yanayotakana na midomo yake.

➢ *Nguvu katika Ulimi*

Maneno yetu yanaweza kuwa maneno yaletayo laana juu yetu, au yanaweza kuwa maneno ya uhai.

Mithali 18:21 Mauti na uzima viko katika uwezo wa ulimi, nao waupendao watakula matunda yake.

Kama viumbe wapya, walioumbwa kwa mfano wa Mungu, tunaumba kwa maneno. Kwa nguvu ya ulimi, tunaachilia aidha maneno ya uhai au ya mauti.

Kama viumbe wapya, ni lazima tuchunge midomo yetu na kuwa waangalifu kuhusu kile tunasema. Labda tunaitajika kubadili njia ya mazungumzo yetu. Kamwe tusiyaachilie maneno ya kifo au uovu kutoka vinywani mwetu.

Kulitangaza Neno

Tunapotafakari juu ya Neno la Mungu, imani itaruka ndani ya roho zetu; na Mungu atadhihirisha Neno Lake kwetu. Kisha tutatangaza kwa ujasiri kile Mungu amenena kwatika Neno Lake.

1 Petro 4:11a Ye yote asemaye hana budi kusema kama mtu asemaye maneno ya Mungu mwenyewe.

➢ *Sema kwa Mlima*

Yesu alionyesha umuhimu wa imani inayonena, hulitangaza Neno la Mungu.

Marko 11:22-24 Yesu akawajibu akawaambia, "Mwaminini Mungu. Amin, amin nawaambia, mtu ye yote atakayeuambia mlima huu 'Ng'oka ukatupwe baharini,' wala asione shaka moyoni mwake, bali aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake."

Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mmeyapokea nayo yatakuwa yenu.

Neno la Mungu na Kumbwa Upya Wakati tunapokea ufunuo wa neno la Rhema la Mungu katika roho zetu za kuumbwa upya, tutaamini kuwa tunapokea kile Mungu amenena kwetu. Tutaanza kuambia mlima wa hali maishani mwetu. Mtu aliye kiumbe kipya atapata kile anasema.

MATANGAZO YA KUUMBWA UPYA

Wale ambao wamepokea ufunuo wa kuumbwa upya wataanza kutangaza haki zao za kuumbwa upya.

Tangaza kwa Ujasiri

Ninajua mimi ni nani katika Yesu Kristo!
mimi ni kiumbe kipya!

Mambo ya kale yamepita!
Mambo yote yamekuwa mapya!

Mimi ni haki Yake Mungu katika Yesu Kristo!
basi hakuna tena lawama sasa
kwa sababu niko ndani ya Kristo Yesu!

Mimi ni mbegu ya imani ya Ibrahimu.
baraka zote za ahadi za Ibrahimu ni zangu.

Mungu hajanipa roho wa hofu,
lakini wa nguvu, na upendo, na wa akili timamu!

Ninaweza kutenda mambo yote katika Kristo anipaye nguvu! Kazi ambayo Yesu alitenda, Naweza pia kutenda!
Furaha ya Bwana ni nguvu yangu!
Neno linasema, "hebu na mnyonge aseme, mimi nina nguvu." Basi, mimi ni mwenye nguvu!

Hakika, Yesu alibeba magonjwa yangu, na maumivu,
na basi sitaitajika kuzibeba tena!

Kwa mapigo ya Yesu nimeponywa!
Sitashikwa na magonjwa yoyote kati ya haya!
Ni mapenzi ya Mungu juu ya vyote kuwa nitafanikiwa
Nitafanikiwa na kuwa katika afya!

Mungu wangu atakutana na maitaji yangu yote
kutokana na utajiri Wake katika utukufu!
ni Mungu ambaye amenipa nguvu na mali!

Nimemtolea Mungu,
na atazidisha mafanikio ya kifedha kwangu katika hali ya ukamilifu na yenye kufurika! Chochote nilichopanda, kile ndicho pia nitavuna!

Nimebarikiwa ninapoingia
na nimebarikiwa niendapo nje!
Chochote ninaweka mikono yangu kufanya kitabarikiwa na mungu!
Sitashindwa!
Mimi ni kiumbe kipya katika Yesu Kristo!

Kumalizia

Tunaposoma, kusikia, kujifunza, na kutafakari juu ya Neno la Mungu, imani hujengwa ndani ya mioyo yetu. Kama viumbe wapya, tunaanza kuachilia nguvu ya Neno la Mungu lijengalo. Kwa imani, tunatangaza neno hilo tunaponena.

Neno la Mungu linaishi na lina nguvu. Linao uhai wa Mungu. Tunapotangaza ufunuo wa kuumbwa upya, tunakuwa washiriki katika asili Yake Mungu.

Tunapoendelea kutangaza Neno la Mungu, tunajikuta kama viumbe wapya,

Kuwa yote ambayo Mungu amesema tuko,
kutenda yote ambayo Mungu amesema tunaweza kutenda,
Kuwa na vyote ambavyo Mungu amesema tunaweza kupata.
ufunuo wa kuumbwa upya
hufanyika kweli maishani mwetu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza jinsi tunaweza kutafakari juu ya Neno la Mungu.

2. Eleza tofauti kati ya Neno lililoandikwa na linalosemwa.

3. kwa nini ni muhimu kutangaza, kusema au kukiri Neno la Mungu kutoka kwa kinywa chako?